Nipashe
Jumamosi Aprili 13, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579891
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper




UKURASA 13

**KESI MAUAJI MWANAFUNZI**
SHAHIDI wa tatu katika kesi ndani ya kesi, askari wa upelelezi wa Jeshi la Polisi, Hashim... UKURASA 3



**MAITI YAVULIWA NGUO**
WATU wasiojulikana wamevunja kaburi na kutoa mwili wa aliyekuwa mtumishi... UKURASA 2

# Ripoti ya CAG gumzo bungeni

**WABUNGE** washangaa kutopewa nakala, Chenge atoa neno, uwezo wa kifedha PSSSF giza totoro... *Endelea ukurasa wa 2*



## Mengi amwagia mamilioni familia za polisi

UKURASA 3



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (kulia), akiwapongeza baadhi ya maofisa wa Jeshi la Polisi, wakati wa hafla ya kutunuku sifa na zawadi kwa askari waliofanya vizuri zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kulinda usalama wa raia na mali zao kwa mwaka 2018, iliyofanyika katika viwanja vya Kituo cha Polisi Oysterbay, jijini humo jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA.**

## RC Makonda ataka magari ya wahalifu yabinafsishwe

UKURASA 2




MICHEZO DK. MENGI AWATANGAZIA NEEMA SERENGETI BOYS UK. 32
MAONI, KATUNI UK.6

# Ripoti ya CAG bado gumzo bungeni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Kibamba, John Mnyika (Chadema), amehoji bungeni sababu za wabunge kutopewa ripoti ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18 wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) iliyowasilishwa bungeni na serikali Jumatano.

Mnyika alihoji suala hilo mara tu baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni jana asubuhi, akieleza kuwa ni utaratibu wa kawaida na unaoruhusiwa na Kanuni za Bunge, ripoti ya CAG kugawiwa kwa wabunge ili waisome na kuielewa kwa lengo la kuisaidia serikali.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, Aprili 8, mwaka huu, serikali iliwasilisha hapa bungeni hati mbalimbali ikiwamo ripoti ya CAG. Tulipoiomba ripoti hiyo pamoja na nakala zingine zilizowasilishwa kama Kanuni ya 37 inavyotaka, Kiti cha Spika kilisema kimepokea kauli zetu na kitazifanyia kazi.

"Lakini, leo (jana) asubuhi nimeangalia kwenye maboksi yetu ya nyaraka za Bunge sikuona kitu. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja ili Bunge lijadili namna ya kugawiwa ripoti hizo," Mnyika alisema.

Katika mwongozo wake kwa mbunge huyo, Mwenyekiti wa Bunge, Andrew Chenge, aliyekuwa anaongoza kikao hicho, alisema nyaraka hizo haziwezi kugawiwa kwa wabunge kama Mnyika anavyotaka na badala yake zitapelekwa katika kamati husika za Bunge.

"Kwanza kabisa, hebu Mheshimiwa Mnyika naomba uniambie ni kifungu gani cha Kanuni za Bunge kinachotaka nyaraka zinazowasilishwa hapa, lazima zigawiwe kwa wabunge?

"Lakini pia, nyaraka zote zinazowasilishwa hapa zina utaratibu wake na hizo za CAG kwa kawaida huwa zinapelekwa katika kamati husika (PAC na LAAC), kwani kuzichapisha ili kuzigawa kwa wabunge wote ni gharama kubwa.

"Kwa hiyo, mwongozo wangu hapa ni kwamba, serikali itawasilisha nyaraka hizo kwa wabunge kwa wakati unaofaa," Chenge alisema.

Mbunge wa Iringa Mjini, Mch. Peter Msigwa (Chadema), pia alisimama na kuomba mwongozo akitaka kujua sababu za kila maeneo anakopita Rais John Magufuli wakati wa ziara zake mikoani, bendera za vyama vya upinzani zinashushwa na kupandishwa bendera za Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Akijenga hoja yake, Mch. Msigwa alisema tukio hilo limetokea mkoani Iringa ikiwamo jimboni kwake Iringa Mjini.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, Chenge alisema hawezi kuzungumzia suala hilo kwa kuwa halikuwa limetokea bungeni kwa wakati huo.

**GIZA NENE PSSSF**

Prof. amesema ukwasi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) uko hatarini kutokana na mfuko huo kubeba madeni ya mifuko iliyoungana

INAENDELEA UK 8

## Maiti yafukuliwa Dar, yavuliwa nguo za ndani

**Na Mary Geofrey**

WATU wasiojulikana wamevunja kaburi na kutoa mwili wa aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Madini, Mary Maramo, aliyefariki dunia mapema wiki hii na kuzikwa juzi katika makaburi ya Pugu Mwakanga, jijini Dar es Salaam.

Mwili huo ulikutwa ukiwa umevuliwa nguo za ndani na kutanuliwa miguu na kisha kuachwa juu ya jeneza kabla ya waliotenda tukio hilo kutimka.

Akizungumza jana katika eneo la tukio, kaka wa marehemu, Deogratius Maramo, alisema juzi walimzika dada yake lakini usiku wa kuamkia jana watu wasiojulikana walivunja sehemu ya kaburi na kuingia ndani.

Maramo alisema watu hao waliingia na kutoa mwili wa marehemu ndani ya jeneza na kufanya shughuli walizokuwa wamelenga kuzifanya na baadaye waliutelekeza mwili huo juu ya jeneza.

"Asubuhi tulipata taarifa kuwa kaburi limekutwa wazi. Tulipofika tulikuta kweli kaburi limevunjwa, mwili umetolewa kwenye jeneza na ukawekwa juu yake lakini hakuna kitu

INAENDELEA UK 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 11/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe 14/04/2019 kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **KAGER**A kuelekea MTIBWA gari hilo lenye namba za usajili:
**T785 CAD/T 166 ADN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21.80 |
| Upana | - | mita | 4.60 |
| Kimo | - | mita | 5.10 |

3.NJia itakayotumika **KAGERA hadi MTIBWA** kupitia **MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215176202




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (kulia), akijadiliana jambo na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Ltd, Dk. Reginald Mengi, wakati wa hafla ya kutunuku sifa na zawadi kwa askari polisi waliofanya vizuri zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kulinda usalama wa raia na mali zao kwa mwaka 2018, iliyofanyika katika Viwanja vya Kituo cha Polisi Oysterbay, jijini humo jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Makonda ataka magari ya wahalifu yataifishwe

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametangaza kusukuma mabadiliko ya sheria ili kuruhusu magari ya wahalifu, hasa wa dawa za kulevya yaliyokaa vituo vya polisi muda mrefu, yataifishwe na kutumiwa na Jeshi la Polisi.

Makonda alisema hayo jana wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti na zawadi kwa askari polisi waliofanya vizuri kazini katika kipindi cha mwaka jana.

"RPC (Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa) jana (juzi) usiku wa saa nane nilipita hapa kituo cha polisi Oysterbay nikaona magari mengi yameegeshwa, nikauliza nikaambiwa ni magari ya watuhumiwa na wengine ni watuhumiwa waliokimbia," alisema.

Makonda alisema kuna haja ya kuiangalia sheria kama mtuhumiwa amekimbia nchi, hasa wa dawa za kulevya, halafu gari lake limekamatwa, litumike kukamata wahalifu wengine badala ya kuendelea kukaa kituoni likakamate wahalifu.

"Tuangalie utaratibu wa hiyo sheria kama ni vielelezo, taarifa ziandikwe tuchukue magari tuingie nayo mtaani tuendelee kukamata wahalifu wengine badala ya kuyaacha hapa yanaharibika halafu tunakosa vitendea kazi wakati wengine walijipatia mali kwa njia ya udanganyifu na utapeli.

"Wengine wamejipatia kwa dawa za kulevya. Hizi mali ni za kuzichukua na kuzitaifisha zifanye kazi za kuwatafuta wenzao ili mwisho wa siku tuwe na mkoa wenye amani," alisema.

Makonda alilitaka Jeshi la Polisi liiangalie sheria hiyo na kama itakuwa na changamoto, atamfuata Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, au Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ili Bunge liibadilishe na kuongeza ufanisi wa mali hizo.

"Nafahamu yako magari mengi yameharibika yamekaa vituo vya polisi na wahusika wameshakimbia. Tuyatumie Jeshi la Polisi kuongeza ufanisi katika kazi zetu," alisema.

Katika hatua nyingine, Makon-

INAENDELEA UK 8

## HABARI ZA KITAIFA

# Shahidi adai mshtakiwa alikiri kumuua mwanafunzi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHAHIDI wa tatu katika kesi ndani ya kesi, askari wa upelelezi wa Jeshi la Polisi, Hashim, ameieleza Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi kuwa mshtakiwa wa kwanza wa kesi ya mauaji ya mwanafunzi wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari Scholastica, Hamisi Chacha, alikiri kumuua mwanafunzi Humphery Makundi.

Kesi hiyo ya mauaji ya kukusudia, inamkabili Hamisi Chacha ambaye ni mlinzi wa shule hiyo, Edward Shayo na mwalimu wa nidhamu, Labani Nabiswa.

Akiongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Omari Kibwana, kutoa ushahidi wake mbele ya Jaji Firmin Matogolo anayesikiliza kesi hiyo namba 48 ya mwaka 2018, alipewa kazi ya kumhoji mtuhumiwa Chacha na Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kilimanjaro.

Alidai kuwa Novemba 17, 2017 alipewa maelekezo na RCO (Mkuu wa Upelelezi wa mkoa) kumhoji mtuhumiwa wa mauaji Hamisi Chacha aliyekuwa mahabusu ya Polisi katika

**INENDELEA UK. 7**

# Mengi atoa kifuta jasho kwa askari

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, ameahidi kuzifuta machozi familia 11 za askari waliokufa kwenye mapambano ya uhalifu mwaka jana kwa kuzipatia Sh. milioni mbili kila moja.

Ahadi hiyo ilitangazwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kwa niaba ya Dk. Mengi wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti na zawadi kwa askari polisi waliofanya vizuri ambapo awali familia hizo kila moja zilipatiwa na Jeshi la Polisi Sh. 500,000.

"Namshukuru Dk. Mengi naye ameongeza Sh. silioni mbili kwa kila familia, kwa kweli wanastahili kutiwa moyo. Askari mahali popote anakopita anatakiwa aheshimike, amekubali kufa ili Dar es Salaam iwe salama," alisema.

Makonda alisema Dk. Mengi ameahidi kuwafuta machozi familia hizo kwa kuzipatia Sh. milioni mbili kila moja kutokana na wapendwa wao kuondoka wakiwa wanapambana na wahalifu.

Naye Makonda aliahidi kuwasomesha watoto wa askari hao kama sehemu ya kuwaenzi baba zao.

"Naomba nifahamu familia zote ambazo Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, awali amezipa zawadi ya Sh. 500,000 kila moja kama mkono wa pole kwa kufiwa na waume zao, nataka kupata taarifa za watoto wa marehemu ili na mimi nihangaike na elimu zao," aliahidi Makonda.

Makonda alisema jana asubuhi alikuwa akizungumza na mtu asaidie kujenga makao makuu ya wajane ambapo itajengwa pia ofisi ya kisasa ili nao wapate heshima.

Akizungumzia kuhusu askari waliopata zawadi mbalimbali zikiwemo mabati, pikipiki na saruji, Makonda aliwapongeza na kuahidi kutoa magari mawili kwa askari wa kike na wa kiume ambao wamefanya vizuri zaidi.

"leo (jana) jioni tutakuwa na chakula cha pamoja Mlimani City na askari hawa pamoja na wasanii na wageni wengine, nitakabidhi magari mawili kwa askari wa kike na wa kiume waliofanya vizuri zaidi," alisema.

Naye, Kamanda Mambosasa alisema askari 72 waliofanya vizuri kwa mwaka jana wamewapatia vyeti na zawadi mbalimbali.

Kadhalika alisema askari wengine 100 wamewapatia zawadi ya vyombo vya ndani ikiwa ni katika kuhamasisha utendaji kazi wenye ufanisi wa hali ya juu.

"Wapo askari wanne ambao walijeruhiwa wakati wa mapambano na wahalifu hawa tunawapa Sh. 500,000 kila mmoja na familia 11 za askari walipoteza maisha nazo tunazipatia Sh. 500,000, wapo watumishi raia watatu ambao wamebahatika kupata mabati na wengine pikipiki," alisema.

**MBATIA AMFAGILIA**

Katika hatua nyingine,

Mbunge wa Vunjo, James Mbatia (NCCR-Mageuzi), amempongeza Dk. Mengi kwa juhudi zake katika kuwainua watu wenye ulemavu.

Mbatia alitoa pongezi hizo kwa Dk. Mengi bungeni jijini Dodoma jana alipochangia hoja ya makadirio ya bajeti ya wizara mbili zilizopo chini ya Ofisi ya Rais (Tamisemi na Utumishi) kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema bajeti iliyotengwa na serikali kwa ajili ya watu wenye ulemavu ni kidogo, hivyo kuna haja serikali kuangalia upya na kuongeza bajeti ya kundi hilo kwa kuwa lina uhitaji mkubwa.

"Lakini, katika jambo hili ni lazima tuangalie hawa wenzetu ni walemavu, lakini na sisi miongoni mwetu kuna walemavu wa fikra na ulemavu wa fikra ni mkubwa kuliko ulemavu mwingine.

"Katika hili, naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Ndugu Reginald Mengi kwa namna ambavyo amekuwa akihangaika kwa kuwasaidia hawa ndugu zetu walemavu, Ndugu Mengi nakupongeza sana," Mbatia alisifu.

Mbunge huyo pia aliitaka serikali iwe na utaratibu wa kuwapa mafunzo viongozi inaowateua kwa kuwa baadhi yao wanafanya kazi bila kufuata utaratibu kutokana na kutokuwa na mafunzo ya uongozi.





**13.04.1948 – 31.10.2018**

Leo ni siku ya kuzaliwa kwa *Mama* yetu mpendwa.
Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia *Mama* aliyetupenda na sisi tukampenda, aliyetufunza na sisi tukamfuata, aliyetunusuru na sisi tukamshukuru.

Eh MUNGU, ingawa *Mama* hayupo nasi hapa duniani, ndani mwetu tumejawa na mapenzi yake, mafunzo yake na hata tabasamu lake.

Tunamkumbuka sana *Mama*, lakini kwa jina lako na rehema zako, tunaamini ipo siku tutaonana naye, ipo siku tutakutana naye, ipo siku tutafuta yaliyofichika ndani ya nyoyo zetu na kutabasamu naye tena.

Eh MUNGU, tunashukuru kwa yote uliyotenda na unayozidi kutenda kwetu.

Mungu Baba, umetupatia nguzo ya ndugu, jamaa na marafiki waliokuwa nasi siku za uhai wa *Mama* na mpaka sasa. Tunapenda kushukuru kila mmoja kwa upendo wao kwetu wakati wa maisha ya *Mama* na tunazidi kushukuru kwa kushirikiana nasi na kuendelea kutufariji haswa ndani ya kipindi cha majaribio.

Mwenyezi Mungu, tunaomba roho ya *Mama* yetu mpendwa iendelee kupumzika mahali pema peponi na ikikupendeza, salamu zetu zimfikie.

**Ma,**
**Leo tunasherehekea maisha yako. Tunakushukuru kwa yote.**
**Tunakukumbuka sana sana sana. Tunakupenda....siku zote za maisha yetu.**
**AMEN.**

# TRA yashikilia mabasi 70 ya mwendokasi bandarini

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema bado inaendelea kuyashikilia mabasi 70 ya kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (Udart), ambayo hadi sasa ni zaidi ya miezi 13 tangu yakwame katika Bandari ya Dar es Salaam.

Februari 13, mwaka jana, Udart ilitangaza kupokea mabasi hayo makubwa 70 yenye thamani ya Dola za Marekani 270,000 kutoka China, lakini hadi sasa wakala huo umeshindwa kuyalipia kodi ili kuyakomboa bandarini.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipa Kodi TRA, Richard Kayombo, aliliambia Nipashe juzi kuwa mamlaka inaendelea kuyashikilia mabasi hayo na upigaji mnada utatokana na uamuzi wa kisheria na kiutawala wa kodi.

"Bado hayajalipiwa na tunaendelea kuyashikilia ila kiasi gani cha kodi ambacho tunadai ni mawasiliano kati yetu na mteja tu," alisema.

Kayombo alipoulizwa ukomo wa kuyashikilia na suala la kuyapiga mnada alisema, "Hayo ni maamuzi ya kisheria na kiutawala wa kodi," alisema.

Februari 16, mwaka jana Udart ilitangaza kupokea mabasi makubwa 70 yenye thamani ya Dola za Marekani 270,000 kutoka China ambayo yangeongeza nguvu ya kupunguza msongamano wa abiria vituoni.

Mabasi hayo yalipokelewa siku hiyo Bandari ya Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Charles Newe, ambaye alisema kuwa mabasi hayo ni yale yenye urefu wa mita 18 ambayo yameunganishwa katikati hivyo kufanya idadi yake kwa wakati huo kufikia 109.

"Awali tulikuwa na mabasi marefu 39 na mabasi mafupi 101, ujio wa mabasi haya marefu tunayoyapokea leo (jana) yanafanya idadi ya mabasi marefu kufikia 109. Kwa ujumla mradi una mabasi 210 kwa sasa," alisema siku hiyo.

Alisema gharama ya mabasi 70 waliyopokea ni Dola za Marekani 270,000 ambayo yameingia nchini kwa meli ya Mv. Treasure. Alisema mabasi hayo yatakwenda kuongeza nguvu kwenye njia zote za mradi wa mwendo kasi ili kupunguza changamoto ya abiria kukaa muda mrefu vituoni wakisubiri usafiri.

"Kulikuwa na changamoto baadhi ya watu walikuwa wakilazimika kuendelea kutumia magari binafsi kutokana na mabasi yetu kujaa, tunaamini kwa sasa watayaacha nyumbani na kupunguza gharama," alisema.

Alisema ujio wa mabasi hayo utapunguza tatizo la uharibifu wa mabasi hayo kwa sababu yaliyokuwapo yalikuwa yakiharibika kutokana na kubeba abiria wengi kupita kiasi.

"Badala ya basi kukaa miaka minane, yamekuwa yakikaa minne tunaamini uharibifu huu utapungua. Utaratibu wa abiria kusimama utaendelea kwa kuwa ndio utaratibu wa usafiri wa majiji katika miji yote duniani," alisema.

Juzi, Udart ilitangaza kuwa inafanya matengenezo makubwa na madogo kwa mabasi 58 baada ya kupata hitilafu na yatakayoendelea kutoa huduma ni 82 tu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Meneja Uhusiano wa Umma Udart, William Gatambi, kutokana na matengenezo hayo upungufu wa mabasi yatakayotoa huduma utasababisha usumbufu kwa abiria.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa idadi ya mabasi inayotoa huduma kwa siku hiyo katika mfumo wa Dart ni 82 tu na hayo 58 yakiendelea kufanyiwa matengenezo.

Hivi karibuni, watumiaji wa mradi huo walilalamika kuwepo kwa upungufu wa mabasi na kusababisha idadi kubwa ya abiria kujazana vituoni na hata yaliyokuwapo yalikuwa yakiwapita abiria.

Oktoba 10 mwaka jana, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda alitembelea kituo cha mabasi cha Kimara na mara baada ya kusikiliza kero za wananchi, aliagiza madereva hasa wa Express kuacha kuruka kusimama kwenye baadhi ya vituo.

Makonda alikwenda kituoni hapo baada ya kuwapo kwa mrundikanao wa abiria kituoni hapo na kusababisha wengine kuingia ndani ya mabasi hayo kwa kutumia madirisha ya mabasi hayo.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (kulia), akikabidhi madawati 100 yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Mkoani Singida, Doreen Lutahanamilwa, katika hafla iliyolifanyika katika halmashauri hiyo, jana, kwa ajili ya shule mbili za Mjimpya na Pentagon za wilayani humo. **PICHA: NMB**

# Ofisa polisi kortini kwa tuhuma utapeli mil. 489/-

**Na Hellen Mwango**

MRAKIBU Msaidizi wa Polisi (ASP) Lydia Ngua (43), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, akikabiliwa na mashtaka 22 ya kujipatia Sh. milioni 489.6 kutoka kwa watu tofauti wakiwamo maofisa wenzake kwa lengo ya kuziwekeza kwenye Vicoba.

Ngua alisomewa mashtaka ya kujipatia fedha hizo kwa njia ya udanganyifu juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustina Mmbando.

Wakili wa Serikali, Ester Martin, alidai kuwa katika tarehe tofauti mwaka jana, mshtakiwa alijipatia Sh, milioni 48 kutoka kwa Happy Mhando, Elicia Kisoma na Mariam Yohana.

Katika shtaka la tano mpaka la nane, ilidaiwa kuwa tarehe tofauti jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alijipatia Sh. 50,126,000 kutoka kwa Jenifer Fokanya, Jane Martine, Mary Ambayoo na ASP Imelda Tweve.

Pia ilidaiwa kuwa katika shtaka la tisa mpaka la 12, katika tarehe tofauti jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alijipatia Sh. 218,937,000 kutoka kwa Inspekta Richard Minja, ASP Sarah Komba, Shukuru Makaranga na Henry Rwiza.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa shtaka la 13 mpaka la 17, katika tarehe tofauti mshtakiwa alijipatia Sh. 119,080,000 kutoka kwa Edna Mbeto, Sabrina Mwakitalu, Lusiana Mwakitalu, Mwanahamisi Issa na Mkemimi Abdulkareem.

Katika shtaka la 18 mpaka la 22, katika tarehe tofauti, ilidaiwa mshtakiwa alijipatia Sh. 52,872,000 kutoka Monica Boniface, Zidadu Hassan, Innocent Nunuo, WP Happy na Halima Nabala.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alijipatia fedha hizo kwa nia ya kuwekeza kwenye Vicoba lakini alizitumia kwa matumizi yake binafsi. Mshtakiwa alikana mashtaka yote.

Hakimu alimtaka mshtakiwa kuwasilisha nusu ya fedha anazodaiwa kujipatia au hati ya mali isiyohamishika.

Pia alimtaka mshtakiwa kuwa na wadhamini wawili kutoka taasisi zinazotambulika watakaowasilisha hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo ya fedha. Mshtakiwa alishindwa kutimiza masharti hayo, kesi itatajwa Aprili 24, mwaka huu.

# Wahitaji miguu bandia wafikia 570

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya watu wanaofika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kupewa miguu bandia bure imeongezeka na kufika 574 hadi jana.

Mtaalam wa Viungo Bandia wa MOI, Dk Geofrey Mwakasungura, aliieleza Nipashe jana kuwa watatoa miguu 600 bure kwa wenye uhitaji lakini hadi jana watu walikuwa wanaendelea kumiminika katika taasisi hiyo.

"Tangu tumetangaza kuanza kutoa huduma hii ya miguu bandia bure, mwanzoni mwa mwezi huu, tumeshapokea watu 574 hadi leo (jana), alisema Dk. Mwakasungura.

Alisema watu wanaofika katika taasisi hiyo wanafanyiwa vipimo kwanza ili kufahamu kama wanaweza kupewa huduma hiyo na wale ambao bado miguu yao ina vidonda wanashauriwa kusuburi hadi wapone.

"Kati ya wagonjwa waliofika ambao hawana sifa za kupewa miguu bandia ni asilimia moja tu lakini wengine wote wanatakiwa kupewa miguu bandia," alisema Dk. Mwakasungura.

Pia alisema wagonjwa walioko nje ya mkoa wa Dar es Salaam, wanachukuliwa maelezo na kuingizwa kwenye orodha ya kupewa miguu bandia kupitia simu za mkononi. "Watu wa mikoani tunawasiliana nao kwa simu tu kwa sababu si jambo jema kuwaita MOI kuja kusikilizwa tu. Tunawapunguzia gharama hizo kwa kuwasikiliza kwa njia ya simu," alisema.

Kuhusu watu wasio na vigezo vya kupewa miguu bandia itakayotolewa mwezi ujao, alisema ni wale ambao vidonda bado vibichi kwa sababu mbalimbali.

Dk. Mwakasungura alisema kwa mtu ambaye amekatwa mguu kwa sababu ya ajali mguu wake huchukua miezi miwili hadi mitatu kupona na wenye kisukari huchukua miezi sita kupona. Pia aliwasihi watu wengine wenye uhitaji kuendelea kujitokeza kwa ajili ya kupata huduma hiyo na endapo idadi itazidi lengo wataingia kwenye orodha ya kupewa wakati mwingine.

Tangazo la ugawaji wa miguu bandia lilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface na kuwasihi watu wenye uhitaji kufika kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa, mpango huo ni sehemu ya mkakati wa MOI na Serikali wa kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora kwa wakati kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi.

"Ni azma yetu MOI na Serikali kuhakikisha huduma zote zinawafikia wananchi hususani wa kipato cha chini, hivyo miguu hii bandia itatolewa bure kwa watu wenye uhitaji, tunafahamu wapo Watanzania wengi ambao walishindwa kupata miguu hii bandia kutokana na kukosa fedha hivyo tumeona ni vyema tukawaondolea changamoto hii," alisema Dk. Boniface.

Alisema wapo Watanzania wengi ambao wameshindwa kuendelea na maisha yao ya kila siku ya uzalishaji kwa kukosa miguu bandia.

"Wapo wenzetu ambao walipoteza viungo na wakakata tamaa wakidhani huo ndio mwisho wa maisha yao, sisi MOI pamoja na serikali tunawatia moyo kwamba wakipata miguu bandia wanaweza kurudi katika shughuli zao za uzalishaji kama kawaida hivyo wajitokeze ili kupata miguu bandia," alisema.

## HABARI KITAIFA



Afisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Maji Safi na Taka mkoa wa Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto), akifungua maji toka kwenye chanzo cha Mkuranga, mkoani Pwani juzi. DAWASA imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa tanki na usambazaji maji utakaokamilika Mwezi Desemba mwaka huu. **MPIGAPICHA WETU**

# Usafirishaji taka hatarishi nje wapigwa 'stop'

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imezuia usafirishaji wa taka hatarishi nje ya nchi, baada ya kubaini baadhi ni malighafi zinazoweza kutumika kwenye viwanda vya ndani na kwamba imebaini zimekuwa zikinufaisha viwanda vya nchi hizo.

Akizungumza juzi na gazeti hili, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc), Dk Samuel Gwamaka, alizitaja taka hatarishi kuwa ni pamoja na vyuma chakavu, betri zilizotumika na zile za kielektroniki.

"Mfano taka za vyuma chakavu zikitumiwa vyema hapa nchini na viwanda vya kuzalisha nondo vitanufaisha wananchi kwa kuwa inaweza kusaidia kuuzwa kwa bei rahisi ambayo wengi watamudu," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema kuwa pia baadhi ya wasafirishaji wa taka hizo wamekuwa wakikiuka taratibu za kusafirisha kwa kutoomba kibali kutoka kwenye mamlaka husika, hivyo Nemc imeona umuhimu wa kukutana na wadau husika.

"Kwa kutambua umuhimu wa jambo hilo, Nemc imeandaa mkutano April 14 (kesho) wa wadau wanaofanyabiashara ya taka hatarishi ili kujadili suala la usimamizi na udhibiti.

Ofisi ya Makamu wa Rais imepewa mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira nchini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake.

Kwa muktadha huo mwezi Machi iliagiza watu wote wenye leseni za kukusanya taka hatarishi wapeleke leseni zao halisi (original certificates) katika Ofisi za Kanda za NEMC zilizoko karibu yao kwa ajili ya uhakiki, ambazo hazitahakikiwa kufikia mwishoni mwa mwezi huu, zitakuwa zimefutwa.

Pia ofisi hiyo ilitoa onyo kwa wananchi wote kuwa yeyote atakayejihusisha na ununuaji au uuzaji wa vyuma chakavu vinavyotokana na miundombinu ya taifa atashitakiwa chini ya Sheria za Uhujumu Uchumi.

Februari, mwaka huu, Bunge lilipokea taarifa ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira iliyohusu Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu utekelezaji wa mkataba wa Basel kuhusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka za sumu.

Ilibainishwa kuwa majadiliano yalifanyika chini ya Umoja wa Mataifa na hatimaye mkataba wa Basel ulipitishwa, unahusu udhibiti wa usafirishaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi na utupaji wake.

# Wafurahia kupata maji safi kwa mara ya kwanza

**Na Frank Monyo**

ZAIDI ya wakazi 30,000 wa kata ya Bonyokwa jijini Dar es Salaam, kwa mara ya kwanza wameanza kupata huduma ya Majisafi baada ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), kukamilisha mradi wa ulazaji bomba kubwa.

Akizungumza jana baada ya kutembelea na kukagua mradi huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema Bonyokwa ni moja ya kata ambazo zilikuwa korofi kwa mamlaka hiyo kufikisha huduma ya maji.

Alisema kazi ya kuunganisha wateja wapya katika kata hiyo inaendelea na mpaka sasa zaidi ya wateja 2,500 wameunganishiwa mabomba kwenye nyumba zao.

Mhandisi Luhemeja aliwataka wananchi wa kata hiyo ambao hawajaunganishiwa maji safi kujitokeza kwa ajili ya kupata huduma hiyo na kwa wale ambao hawana uwezo watakopeshwa na kuingia makubaliano ya kulipa ndani ya miezi sita au 12.

Mmoja wa wakazi wa kata hiyo, Saumu Ally, alisema kupatikana kwa huduma hiyo kutawasaidia kufanya shughuli zingine za maendeleo baada ya kuwa wanatumia muda mwingi kutafuta maji.

"Kwa kweli sisi tunashukuru sana kupata maji kwa muda mrefu tulikuwa tunaangaika kutafuta maji, sasa hata tukioga tutapendeza maana tumekuwa tukinywa maji ya visima ambayo tulikuwa tunayanunua kwa kwa bei kubwa," alisema Saumu.

Naye Athanas Masaka amesema ni historia kwa wakazi wa Bonyokwa kushuhudia maji ya bomba yakitoka katika eneo hilo kwa kuwa ni muda mrefu hawajapata huduma hiyo na kusababisha wahangaike na kuingia gharama kubwa kupata huduma hiyo.

"Tunamshukuru sana kiongozi wa Dawasa kwa kutuletea maji katika kata yetu kwani kwa muda mrefu tumekuwa tukihangaika kununua maji kwenye magari, lakini leo tunashuhudia maji yakitoka kwenye mabomba yetu kwa kweli tunashukuru sana." alisema Masaka.

# Polisi yatumia Tehama kutoa fomu

**Na Salome Kitomari**

JESHI la polisi chini ya kitengo cha tekonolojia ya habari na mawasiliano (Tehama), limenzisha mfumo wa upatikanaji wa fomu ya upotevu wa vitu na mali kwa njia ya mtandao

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana jijini Dar es Salaam na Msemaji wa Jeshi la Polisi, Ahmed Msangi, ilieleza kuwa anayetaka kutoa taarifa kwa sasa anaweza kufanya malipo kwa mfumo wa malipo serikalini (GePG).

Alisema mfumo huo ulianza Machi, mwaka huu, lengo lilikuwa kupunguza gharama na kurahisisha upatikanaji wake katika vituo vya polisi na kumwezesha mtu yeyote kufanya maombi na malipo kwa mtandao.

Aidha, alisema baada ya kukamilisha malipo mwombaji atatakiwa kwenda kituo cha polisi ili kukamilisha huduma hiyo.

"Mwombaji wa fomu ya upotevu kwa njia ya mtandao, atatakiwa kujaza fomu kupitia mtandao na kutoa maelezo ya upotevu na kupatiwa

INAENDELEA UK 8



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Dua zote kwa Serengeti Boys majaribuni AFCON*

**IMEBAKI** siku moja kuelekea fainali za vijana za umri chini ya miaka 17 (AFCON U-17) ambazo zinafanyika kwa mara ya kwanza hapa nchini.

Fainali hizo zinazoendeshwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zitachezwa kuanzia kesho Jumapili hadi Aprili 28 mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa na Azam Complex, vyote viko jijini Dar es Salaam.

Michuano hiyo itashirikisha timu nane ambazo ni pamoja na wenyeji Tanzania (Serengeti Boys), Angola, Uganda, Nigeria, Morocco, Senegal, Cameroon na Guinea.

Serengeti Boys ambayo inashiriki fainali hizo kwa mara ya pili, itafungua pazia la mashindano hayo dhidi ya wenzao kutoka Nigeria, mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini kuanzia saa 10:00 jioni.

Katika kujiandaa na fainali hizo, Serengeti Boys inayofundishwa na Mzalendo, Oscar Mirambo imecheza mechi za kirafiki na kushiriki mashindano mbalimbali ndani na nje ya Tanzania, yaliyokuwa na lengo la kuwaimarisha na kuwajenga wachezaji.

Mirambo aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake kimecheza mechi 21 na kila kilichokuwa kinatokea katika mechi hizo walikifanyia kazi kwa sababu michezo yote ilikuwa ni sehemu ya kujifunza na kuwa uzoefu wachezaji wake.

Ili timu hiyo na mashindano hayo yafanyike kwa ufanisi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Pombe Magufuli, alitoa kiasi cha Sh. bilioni moja ili kufanikisha maandalizi ya timu na kusaidia gharama nyingine za uenyeji wa michuano hiyo.

Haya yote yanaweza yasionekane kama mchezaji namba 12 ambaye ni shabiki hatajitokeza uwanjani kuwashangilia wachezaji hawa.

Yosso hawa wanahitaji kupewa hamasa kama waliyopewa kaka zao, Taifa Stars ambao wao walifanikiwa kukata tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Afrika (AFCON 2019), au zaidi ili kutimiza malengo yao.

Kama iliwezekana kwa Taifa Stars na kwa klabu ya Simba kuujaza uwanja huo wenye uwezo wa kuingiza mashabiki 60,000 kwa wakati mmoja, inawezekana pia ikafanyika kwa Serengeti Boys na hatimaye ndoto za kushiriki mashindano mengine makubwa ya dunia zikatimia.

Mbali na kutakiwa kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo, Serengeti Boys inahitaji kupata matokeo mazuri na kuweka rekodi nyingine ya kukata tiketi ya kushiriki Fainali za Vijana za Dunia.

Timu nne zitakazofanya vema katika fainali hizi, zitapata nafasi ya kuiwakilisha Afrika kwenye Fainali za Vijana za Dunia zitakazochezwa baadaye mwaka huu nchini Brazil.

Nipashe linawaomba wadau wa soka wa jijini na mikoa jirani kufika kwenye Uwanja wa Taifa kuwashangilia vijana wetu ambao kwa kutwaa makombe mengine, wameonyesha kuwa wanataka kulitangaza vema jina la Tanzania katika medani ya soka ulimwenguni.

Huu ni wakati mwingine wa kusema kila mtu atashinda nyumbani. Nyumbani kwa Serengeti Boys ni hapa, hivyo mashabiki mnapaswa kujitokeza kwa wingi kuwashangilia vijana katika mechi zao zote watakazocheza.

Hakuna kisichowezekana, kila la kheri Serengeti Boys, kila la kheri Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kila la kheri Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# *Twaitakia Simba kila la heri*

Na Barnabas Maro

**LEO** ni kufa au kupona kwa timu ya Simba dhidi ya TP Mazembe zitakaporudiana kule Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) baada ya kutoka suluhu katika mchezo wa kwanza uliochezwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam.

Si rahisi kubashiri mshindi kwani mchezo wa mpira una matokeo ya ajabu. Wakati mwingine umdhaniye ndiye huwa siye na adhaniwaye siye huwa ndiye! Kwa kuwa mpira hudunda, kosa moja laweza kuiathiri timu yoyote. Msemaji wa Simba, Haji Manara ametamba kuwa hakuna timu yoyote itakayokuja kupambana na Simba kwenye uwanja wa Taifa iondoke na ushindi.

Wahenga walisema "Maneno fedha, majibu dhahabu" wakiwa na maana maneno tusemayo ni kama fedha lakini majibu ni kama dhahabu. Twashauriwa tuwe na tabia ya kutoa majibu yanayoweza kuonesha kuwa tunazitumia akili zetu. Yafaa kutafakari kabla ya kujibu jambo fulani.

Hakika Simba ina timu iliyoenea kila sehemu. Hapana shaka ina timu pana, kwa maana ya wachezaji wanaojua kusakata (fanya jambo kwa umahiri) kabumbu ipasavyo na la kuvutia. Hivyo hawapaswi kuwa na wasiwasi wala woga bali kila mmoja atimize wajibu wake. Wachezaji wasiwe wachoyo kupeana mpira bali wacheze kwa kushirikiana kwani umoja ni nguvu utengano ni udhaifu na penye nia pana njia.

Twajua kucheza ugenini kuna ugumu wake. Kuzomewa na wenyeji na kufanyiwa mambo yasiyopendeza. Wachezaji wa Simba hawatakiwi kusikiliza maneno yasemwayo nje ya uwanja. Muhimu ni kucheza kwa bidii na ari wakiwa na shauku (hamu ya kutaka kupata ushindi) ya ushindi bila kujali kelele na kuzomewa. Hii ni kawaida kwa timu ngeni inapocheza ugenini kwa hiyo hakuna sababu ya wachezaji wa Simba kutetema wala kukata tamaa wanapokuwa uwanjani.

Watanzania tunapaswa kuwaombea dua maalumu wachezaji wa Simba ili wafanye kile kinachodaiwa kutowezekana mbele ya TP Mazembe ingawa yasemwa ni vigumu kuwashinda kwao. Hayo ni maneno ya kuwakatisha Simba tamaa kwani "hakuna mume wa waume." Maana yake hakuna mtu mmoja anayeweza kuwashinda wanaume wenzake wote.

Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu anayejitia ubabe au anayejidai kuwa na nguvu (kwa muktadha huu TP Mazembe) kama njia ya kumnyamazisha. Simba wanapaswa kuwa makini kulinda lango lao na wakati huo huo washambuliaji wajitume ipasavyo na kutokuwa na uchoyo kwa maana ya kila mmoja kutaka kufunga hata pale asipoweza kufanya hivyo.

Nawanasihi wachezaji wa Simba kutocheza kwa woga wala papara na uchoyo bali wacheze kwa ushirikiano na bidii wakifuata maelekezo ya walimu wao. Watambue kuwa wanaiwakilisha Tanzania na wananchi wake.

Hebu! (tamko la kumtaka mtu asikilize). "Kaa mkuu ng'ombe wa maji akiinua gando mwelemeze nanda." Kaa mkubwa ni mfano wa ng'ombe, akiinua mguu mwelemeze kigongo cha panda.

Methali hii yatufunza kuwa hatupaswi kumdharau mtu mwenye uwezo au nguvu fulani katika mazingira yake hata kama anaonekana dhaifu na mnyonge. Pia hutumiwa kutunasihi kuwa yeyote mwenye nguvu anaweza kushindwa mradi tuwe na maarifa na mbinu.

Nawakumbusha Simba kuwa "Mja hatindi rehema ali hai duniani." Maana yake binadamu hapaswi kukata tamaa akiwa bado anaishi. Methali hii hutumiwa kutunasihi tusikate tamaa katika mambo yoyote tuyafanyayo hata kama ni magumu kiasi gani; tuvumilie tu hatimaye tutafanikiwa.

Msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Naweka wazi kuwa hapa nyumbani siipendi Simba inapocheza na timu yoyote ya Tanzania lakini inapopambana na timu ngeni kutoka nnje ya Tanzania, huwa upande wao (Simba) kwani damu ni nzito kuliko maji.

Kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Tanzanua Bara, kati ya timu 20 zinazoshiriki, ni Simba pekee iliyofungwa mabao machache (7) ikilinganishwa na Yanga iliyo kileleni ambayo imecheza michezo 31, kufungwa mabao 22 na kufunga mabao 51. Wakati Yanga ikipoteza michezo mitatu na kwenda sare mara tano, Simba imecheza mechi 22, kushinda michezo 18, kupata sare tatu, imefunga mabao 45 na kupoteza mchezo mmoja tu. Ina mechi tisa za viporo.

Hii yaweza kuwapa nguvu wachezaji wa Simba na kuwashitua TP Mazembe kuwafanya wacheze kwa wasiwasi. Hata hivyo Simba wanatakiwa kuwa makini sana kwani wachezaji wa TP Mazembe watacheza mchezo wa kushambulia zaidi. Watumie nafasi hiyo kujilinda kwa makini na kushambulia kwa kushitukiza bila kujali ngebe (maneno mengi yenye jeuri) za wenyeji watakaokuwa wakiishangilia timu yao ya nyumbani.

Aombaye atapewa: "Nami nawaambia: Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. (Luka 11:9-10). Inshallah (apendapo Mwenyezi Mungu).

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Bil. 30/- zatumika ujenzi madarasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema katika mwaka wa fedha 2018/19 imetoa Sh. bilioni 29.9 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma 2, 392 ya madarasa nchini.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tamisemi, Mwita Waitara, alisema hayo jana bungeni mjini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Lushoto(CCM), Shabani Shekilindi.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema serikali imekuwa na utaratibu wa kukarabati shule zake za msingi na sekondari nchini na kwamba ni lini itazifanyia ukarabati shule za msingi Kwemashai, Bandi, Milungui, Kilole na shule za sekondari za Ntambwe, Ngulwi, Mazashai na Mdando.

Akijibu swali hilo, Waitara alisema kati ya fedha hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imepewa Sh. milioni 512.5 kwa ajili ya kukamilisha maboma 46 ya madarasa shule za sekondari.

Waitara alisema serikali itaendelea kukarabati na kujenga miundombinu ya elimu kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Awali, alisema katika kipindi cha mwaka 2018/19 serikali kupitia program ya Lipa Kulingana na Matokeo(EP4R) imepeleka Sh. milioni 467 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali.

"Mabweni mawili, matundu sita ya vyoo na madarasa mawili katika Shule ya Msingi Shukilai na ujenzi wa mabweni mawili katika Shule ya Sekondari Magamba, ujenzi wa bweni moja na madarasa mawili Shule ya Sekondari

# Shahidi adai mshtakiwa alikiri kumuua mwanafunzi

**INATOKA UK. 3**

Kituo Kikuu cha Polisi Moshi mjini.

Shahidi huyo alidai alimchukua mtuhumiwa huyo na kwenda kuchukua maelezo yake katika ofisi yake ya chumba cha upelelezi na kwamba mshtakiwa huyo alikuwa na afya nzuri.

Aliendelea kudai kuwa baada ya kumfikisha Chacha katika chumba hicho alimpatia maelezo ya onyo na kumtaka kuwa na shahidi au wakili wake wakati anatoa maelezo yake majira ya saa 5:25 hadi saa 8:40 za usiku.

Alidai baada ya kumpatia maelezo hayo mshtakiwa huyo alieleza kuwa yupo tayari kuandika maelezo yake mwenyewe na alipoanza kuyatoa alikiri kufanya kosa la kuumuua mwanafunzi huyo.

Shahidi huyo amedai baada ya mtuhumiwa kukiri kosa alimsomea mshtakiwa maelezo na kuyakubali na kisha alitia saini kwa hiari yake mwenyewe na pia alimweleza maelezo yake hapo si mwisho wake na anaweza kuyatoa kwa mlinzi wa amani.

Hashim aliieleza mahakama hiyo kuwa baada ya kumaliza kumhoji mshtakiwa, alimrudisha rumande katika Kituo Kikuu cha Polisi Moshi Mjini na kwamba hakuna wakati alimpiga wala kutoa vitisho kwa mshtakiwa huyo.

Shahidi huyo alimfanyia mshtakiwa huyo mahojiano mengi, lakini mengine hatukuyaandika huku mshtakiwa huyo alimweleza yeye ni Polisi mstaarabu kuliko polisi wenzake waliomkamata kule Himo kwani wakati tu wa kumkamata na kupanda gari la Polisi walimchapa viboko.

Aidha, shahidi mwingine katika kesi hiyo ndani ya kesi, Mkaguzi wa Polisi, Fredrick Kisanga alidai mahakamani hapo kuwa Novemba 17 mwaka 2017 alimtandika viboko viwili mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo baada ya kukataa kutii bila shuruti amri yake wakati akimkamata na kumpandisha katika gari la polisi.

Naye Irene Mushi, shahidi, ambaye ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Moshi Mjini na mlinzi wa amani alidai mahakamani hapo mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo Hamisi Chacha alitoa maelezo yake mbele yake na pamoja na mambo mengine mshitakiwa huyo pia alidai kupigwa viboko viwili na mapolisi.

Juzi, upande wa utetezi katika kesi hiyo, uliibua hoja mbili kuu wakipinga kupokelewa kwa maelezo ya 'ungamo' yaliyotolewa na shahidi wa 14 wa upande wa mashtaka, Irene Mushi.

Baada ya pingamizi hilo kutolewa, Jamhuri iliomba Mahakama Kuu, Kanda ya Moshi kusikiliza sababu hizo kwa kuwa na kesi ndani ya kesi.

Mawakili wa utetezi, walitoa sababu za kupinga kupokelewa kwa kinachoitwa Extra Judicial Statement (maelezo ya ungamo), wakidai kuwa kielelezo hicho kina mapungufu makubwa ya kisheria na hakina masharti ya uhiari.

Ungamo hilo lilitolewa mahakamani hapo na mlinzi wa amani, Irene Mushi (35) ambaye ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Moshi Mjini.

Wakili Elikunda Kipoko ndiye aliyeanza kupinga kupokewa kwa ungamo hilo akidai kuwa jopo la mawakili wa utetezi, linapinga kupokelewa kwa kielelezo hicho kwa sababu kwanza kina mapungufu makubwa ya kisheria na sababu ya pili ni kwamba hakukuwa na masharti ya uhiari.

Baada ya kauli hiyo, Wakili Mkuu wa Serikali, Joseph Pande alisimama na kuieleza mahakama hiyo, kwa kuwa upande wa utetezi wanapinga kisipokewe kielelezo hicho, na kwa kuwa mapingamizi yao yameegemea kwenye sababu kuu mbili, wanaomba kwenye sababu hiyo ya kutokidhi kwa matakwa ya kisheria wangesikiliza sababu hizo walizonazo za kisheria, halafu mahakama ipate nafasi ya kupima huo uhiari, kwa kuwa na kesi ndani ya kesi kwa kadri jinsi Jaji atakavyoona inafaa.

Upande wa utetezi ulisimama tena na kupinga hoja hiyo kwa Wakili wa utetezi, David Shilatu kuieleza mahakama hiyo kwamba wanakubaliana na muongozo wa Jaji Matogolo lakini hoja yao ya kisheria ni kuhusu admissibility (usahihi) wa hiyo Extra Judicial Statement (maelezo ya ungamo) na katika eneo hilo wanakataa eneo la admissibility of document (usahihi wa nyaraka) na voluntarlyness (uhiari).

"Suala la uchukuaji wa Extra Judicial Statement ni suala la kisheria na suala hili linao muongozo wa namna ya kuliendea, na muongozo huo mtukufu Jaji ulitolewa na Chief Justice (Jaji Mkuu) for the guide of justice (kama muongozo) wa jinsi gani ungamo linavyopaswa kuchukuliwa. Julai mosi mwaka 1964 muongozo huo ndio ulitolewa na tangu ulipotangazwa katika kijitabu hicho ulikuwa ni muongozo rasmi wa mahakama zetu kama ambavyo imeelekezwa katika kifungu cha 72 (3) cha Sheria ya Mahakimu na Mahakama (MCA).

Zaidi alidai kuwa: "Kifungu hicho kimeelekeza mambo sita ambayo Magistrate Court inatakiwa kufuata wakati wa kuchukua Extra Judicial Statement. Sasa kwenye hii Extra Judicial Statement wenzetu (upande wa mashtaka) walioileta mahakamani, hakuna sehemu ambayo imeandikwa muda ambao mshtakiwa alichukuliwa maelezo yake na accused (mshtakiwa) hakuulizwa na mlinzi wa amani alilala wapi. Maelezo haya ya ungamo yanakosa sifa ya kuwa admitted (kupokelewa) na mahakama yako tukufu."

Dakika mbili baadae, Wakili wa utetezi Gwakisa Sambo alisimama naye pia akipinga kupokewa kwa ungamo hilo akidai kuwa kwa niaba ya mshtakiwa namba mbili anapinga kwa sababu zifuatazo; kwamba kielelezo hicho kimechukuliwa nje ya muda ambao unatakiwa kisheria chini ya kifungu cha 50 na 51 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA).

Pia wakili wa utetezi Patrick Paul aliongeza uzito katika mapingamizi hayo, akidai kuwa anaunga mkono mapingamizi yaliyotolewa na upande wa utetezi na anaomba mahakama ihaulishe (adapting) kile ambacho kimeshasemwa na wenzake kwamba hiyo ni mahakama ya kisheria na inapaswa kufuata sheria. Wakili Paul alieleza mahakama hiyo kuwa: "Ungamo ambalo halikuzingatia maelekezo ya kutaja muda wa kukamatwa na mahali mshtakiwa alipolala, Mahakama ya Rufani imeelekeza ungamo hilo litupiliwe mbali na wewe (Jaji) umefungwa na maelekezo hayo, tunaomba uyatupilie mbali."

Kutokana na mabishano hayo ya kisheria, Wakili Mkuu wa Serikali Joseph Pande alisimama tena kujibu hoja hizo akidai kuwa hoja zilizotolewa hazina msingi wowote wa kisheria na wanaomba mahakama hiyo izitupilie mbali kwa ujumla wake.

Lakini pia ni rai yao kwamba Extra Judicial Statement inayobishaniwa ina sifa zote za kupokelewa na wanaomba Jaji aipokee kwa sababu ikishasomwa kama ilivyo eneo linalobishaniwa muda na tarehe ya kukamatwa mtuhumiwa na alipelekwa wapi baada ya kukamatwa na alitokea wapi kwenda kwa mlinzi wa amani na alienda lini, vitu hivyo vyote vipo.

Wakili Pande alidai kuwa: "Mheshimiwa Jaji, tunachopaswa kujua hicho kinacholalamikiwa kama kina kwenda kwenye mzizi wa suala la msingi na sio tu kwamba kitu fulani hakipo, document (nyaraka) isipokelewe. Mahakama hii haiwezi kui-dismiss hiyo nyaraka bila kielelekeza kwenye misingi ya kisheria inayojengwa kwenye kifungu cha 169 cha Sheria ya CPA kuanzia kifungu cha 1 hadi 6."

Hoja hiyo ikaongezewa nguvu na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula aliyesimama na kuieleza mahakama hiyo kwamba kifungu cha 50 na 51 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) hakina mahusiano ya uchukuaji wa maelezo ya ungamo na kwamba kifungu hicho kinaangukia kwenye sehemu ya 2 (b) ya CPA na vifungu hivyo vinazungumzia majukumu ya maofisa wa Polisi wanapokuwa wanafanya uchunguzi wa makosa ya jinai.

"Tunajiuliza MCA (Magistrate Court Act) ni Ofisa wa Polisi au? Si sahihi kusema kifungu hicho kinamhusu mlinzi wa amani na hoja ya muda haina mantiki na inakosa miguu ya kusimamia katika macho ya sheria.

Ni maoni yetu hoja zilizotolewa na upande wa utetezi hazina mantiki, zipuuzwe na kama kungalikuwa na gharama tungezidai kwa sababu wamesumbua akili zetu,"alieleza zaidi Wakili Chavulah Wanaokabiliwa na kesi hiyo, namba 48 ya mwaka 2018 ni mshtakiwa wa kwanza Hamisi Chacha ambaye ni mlinzi wa shule hiyo, mmiliki wa shule hiyo Edward Shayo 'king size' na mwalimu wa nidhamu Laban Nabiswa.

Juzi, shahidi 12 katika kesi hiyo ambaye ni Meneja wa Kitengo cha Sayansi ya Huduma na Vipimo vya Kibaiolojia kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Hadija Saidi Mwema alieleza mahakama hiyo kwamba alipima vipimo zaidi ya 15 vya DNA (sampuli za vinasaba), lakini kipimo kimoja ndio kiliweza kuuwiana sawa na mwili unaodaiwa wa marehemu Humphrey Makundi.

## Mahiga asema Sokoine ndiye nguzo ushindi vita vya Kagera

**Na Mwandishi Wetu,** MONDULI

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga, ametoa siri ya ushindi wa Tanzania katika vita vyake na Uganda, akisema ilichangiwa na uzalendo wa aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Moringe Sokoine.

Tofauti na wengi wanavyojua, Dk Mahiga alitoboa kwa mara ya kwanza kwamba hayati Sokoine ndiye aliyekuwa nguzo kuu ya ushindi katika vita hivyo wakati huo akiwa Waziri wa Ulinzi.

Alisema wakati huo yeye (Dk Mahiga) akiwa Mkurugenzi Idara ya Usalama wa Taifa na huku chokochoko za Nduli Idi Amin zikiendelea, alimweleza Sokoine juu ya uwezo mdogo wa Tanzania kijeshi ikilinganishwa na Uganda, lakini Sokoine alitoa mikakati ya kumkabili hadi ushindi ukapatikana.

"Iddi Amin alikuwa na ndege za kivita, sisi hatukuwa nazo, Iddi Amin alikuwa na magari ya deraya sisi hatukuwa nayo, wanajeshi wa Idd Amin walikuwa wanatembea kwenye magari ya doria, sisi hatukuwa nayo," alisema.

Akaongeza: "Kutokana na uzalendo wake, Sokoine alisema tutafute makombora ya kutunguliwa ndege, mizinga ya masafa marefu kutoka nchi marafiki na askari wetu watembee kwa miguu."

Mapema Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa CCM, alisema amefanya kazi na Sokoine wakati (Pinda) alipokuwa msaidizi wa Baba wa Taifa. Alisema mara nyingi Nyerere alitangaza kutaka kung'atuka lakini alitaka atakayemrithi awe mwadilifu na asiyependa rushwa.

Kwa mujibu wa Balozi Mahiga, kifo cha Sokoine kilisononesha taifa na wengi walikuja kujua kuwa aliyeandaliwa kurithi nafasi hiyo alikuwa Sokoine. Alisema hata sasa wanapoona juhudi zinazofanywa na Rais John Magufuli zinaonyesha kuwa anafuata nyazo za Sokoine.

Alisema Magufuli ni kiongozi anayependa wanyonge, mwadilifu, anayechukia rushwa na anafanya kazi kwa nguvu zake zote kama alivyokuwa akifanya Sokoine.

Akiongoza misa ya kumbukumbu ya Sokoine nyumbani kwake Monduli Juu jana, Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar as Salaam, Polycarp Kardinali Pengo, aliwataka viongozi na wananchi kuiga maisha ya hayati Sokoine ya kutojilimbikizia mali.

Alisema katika uhai wake, licha ya kuwa na wadhifa mkubwa serikalini, Sokoine hakuwa na tabia ya ubinafsi ya kujilimbikizia mali.

"Kifo cha Edward kiwe fundisho kwetu, tumuombe Mungu tuwe chombo cha amani kwa ajili yetu na taifa zima," alisema. Alisema hakuna watu wanaoweza kuvumilia wafe njaa, wanaweza kuwa na uvumilivu kwa siku chache tu na baada ya hapo vurugu lazima zitazuka.

Kardinali Pengo alisema hayo jana katika mahubiri yake wakati wa maadhimisho ya Misa Takatifu ya kumbukumbu ya miaka 35 ya kifo cha Sokoine, kilichotokea Dumila mkoani Morogoro Aprili 12, 1984 akiwa njiani kuelekea Da es Salaam, akitokea Dodoma kwenye vikao vya bunge.

Alisema wakati wa uhai wake, Sokoine alipenda kuishi maisha ya ufukara ya Mtakatifu Fransisko, huku akimuomba Mungu kila siku amfanye chombo cha amani.

# RC anusa ufisadi ujenzi wa kituo cha afya Chato

**Na Consolata Evarist** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kuuchunguza mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Mganza katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato.

Alitoa agizo hilo juzi kutokana na kuchelewa kukamilika kwa mradi huo ambao ulianza kujengwa mwaka 2009 kwa nguvu za wananchi na baadaye serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ilitoa Sh. milioni 400 lakini hadi sasa utekelezaji wake unasuasua.

Hatua ya mkuu huyo wa mkoa imetokana na kutokurishishwa na taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chato, Eliud Mwaiteleka, kuelezea utekelezaji wa mradi huo.

Alisema hajaona kazi ambayo inafikia thamani ya fedha zilizotolewa kwa sababu ujenzi haujakamilika na fedha zimekwisha, hivyo kuna umuhimu wa kufanya uchunguzi ili kubaini tatizo linalosababisha kutokukamilika kwa mradi huo.

"Tutachunguza taarifa ya mradi huu. Watu wengi wameweka fedha, mimi sikuleta Sh. milioni 100 hapa hivi hivi na sioni hiyo fedha na kila nikija sioni kazi iliyofanyika," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mganza, James Kongwa, kwa upande wake alizungumzia nguvu za wananchi na mchango wa Rais John Magufuli ulivyotumika kwenye ujenzi.

Alisema serikali ilipeleka Sh. milioni 400 na wananchi walijitolea kuchimba msingi na kuchota maji wakati Rais Magufuli alitoa Sh. Million 10 zilizotumika kununua mabati na mbao za kuezekea.

Mradi huo ni kwa ajili ya Kata ya Mganza yenye vijiji tisa na vitongoji 41 ambayo haina kituo cha afya wala zahanati ya serikali.



Waendesha guta wakiwa wamesheheni mzigo katika Barabara ya Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

## Ripoti ya CAG bado gumzo

INATOKA UK 2

kuuanzisha.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka 2017/18, iliyowasilishwa bungeni juzi, CAG Assad anabainisha kuwa mifuko ya hifadhi ya jamii ya LAPF, GEPF, PSPF na PPF iliyounganishwa kutengeneza mfuko mmoja wa PSSSF ilikuwa na madeni makubwa.

"Mifuko ya hifadhi ya jamii inasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko Hifadhi ya Jamii (SSRA). Nimeangalia utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na mifuko ya pensheni ya LAPF, PSPF, GEPF, PPF na NSSF pamoja na utendaji wa SSRA.

"Serikali ina deni la jumla ya Sh. trilioni 2.39 kwenye mifuko sita ya hifadhi ya jamii. Kati yake, kiasi cha Sh. trilioni 1.625 (asilimia 68) kilipaswa kiwe kimelipwa katika mwaka wa fedha 2017/18. Mikopo mingine iliiva tangu mwaka 2014.

Katika deni hilo kwa mifuko ya hifadhi ya jamii, serikali inadaiwa na NSSF Sh. trilioni 1.253, PSPF Sh. bilioni 448.9, PPF Sh. bilioni 292.11, LAPF Sh. bilioni 169.64, GEPF bilioni 10.4 na NHIF Sh. bilioni 216.2.

"Kuchelewa kulipwa kwa mikopo hiyo kumeathiri uendeshwaji wa mifuko husika. Mfuko mpya wa PSSSF umebeba madeni ya mifuko iliyoungana ambayo yanaweza kuhatarisha ukwasi wa mfuko huu," Prof. Assad anabainisha katika ripoti yake hiyo.

## Ataka magari yataifishwe

INATOKA UK 2

da alilipongeza jeshi hilo kuwa limekuwa halilali usiku na mchana likihakikisha nchi inakuwa salama.

"Ukisikia Krismasi, Mwaka Mpya, Pasaka maana yake jeshi halilali wakati watu wengine wakifikiria kwenda kwenye hoteli au baa kutumia fedha zao, Jeshi la Polisi linawaza kulinda nyumba zao ili amani iendelee kuwapo," alisema.

Pia aliwapongeza makamanda wa mikoa ya kipolisi Ilala, Kinondoni na Temeke wa sasa na walioondoka kwa kile alichosema wamesaidia katika mikoa yao kuiweka vizuri.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alimshukuru Makonda kwa misaada mbalimbali aliyotoa ndani ya jeshi hilo, zikiwamo pikipiki 10, komputa, baiskeli 200 na magari ambayo yanaendelea na matengenezo.

"Leo (jana) umetusaidia askari wetu waliofanya vizuri mwaka jana wapate zawadi hizi ambazo zimetokana na wadau mbalimbali,tunakushuruku sana kwa kuhakikisha jeshi wakati wote linakuwa imara na tayari kukabiliana na vitendo vya uhalifu," alisema.

## Polisi yatumia Tehama

INATOKA UK 5

namba maalumu na kulipa Sh. 500 kwa njia ya mtandao, atakwenda kituo chochote cha polisi kwa ajili ya uthibitisho na atatoa nakala ya fomu hiyo kwa manufaa yake," alisema.

Msangi alisema kwa kuanzia mfumo huo umeanza kufanyakazi mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, na kwamba majaribio yakifanikiwa ifikapo Juni mwaka huu mfumo huo utatumika nchi nzima.

## Maiti yafukuliwa Dar, yavuliwa nguo

INATOKA UK 2

chochote kilichoibwa," alisema.

Maramo alisema mashada waliyokuwa wameweka juu ya kaburi hayakuguswa na watu hao, hali inayoonyesha hakuwakuwa na lengo la kufanya wizi wa aina yoyote.

Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na mtaalam wa afya, waliufanyia uchunguzi mwili huo na kukubaliana kuuhifadhi tena.

Aidha, fundi aliyejenga kaburi hilo, Josephat Mkelemi, alikuwa wa kwanza kubaini tukio hilo wakati akienda kulimwagilia maji.

"Saa 1:00 asubuhi wakati nakuja kwa ajili ya kumwagilia kaburi, nilishtuka baada ya kukuta likiwa wazi ikabidi kwenda kutoa taarifa kwanza," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema alikwenda kutoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Pugu Bombani, Gido Benard, ambaye alifika na kushuhudia tukio hilo.

Baada ya uchunguzi, mwili huo ulivalishwa nguo upya na na kurudishwa kwenye jeneza na kurudishwa kaburini kisha kujengewa upya mahali palipokuwa pamevunjwa.

Tukio hilo lilizua taharuki kwa majirani na watu waliokuwa wakipita karibu na makaburi hayo huku mashuhuda wakilihusisha na ushirikina.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Ilala, Zuberi Chembera, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kulihusisha na ushirikina.

"Hatutaki kuthibitisha moja kwa moja kuwa ni ushirikina isipokuwa tunalihusisha tukio hili na ushirikina," alisema Kamanda Chembera.

Alisema juzi mwili wa Mary ulizikwa katika makaburi hayo lakini jana wakati fundi alipoenda kumwagilia alikuta sehemu ya kaburi imevunjwa.

Alisema Jeshi la Polisi walipata taarifa na kwenda kufanya uchunguzi wake na bado wanaendelea kabla ya kutoa taarifa ya kilichofanywa na wahalifu hao.

Kamanda alisema eneo lilipochimbwa kaburi lilikuwa na mteremko, hivyo sehemu ya juu ya kaburi matofali hayakufunikwa na udogo, hivyo wahalifu hao walipavunja na kuingia ndani.

Alisema pia matofali na udongo wa saruji iliyotumika kujenga kaburi hilo haikuwa imara hali ambayo ilikuwa rahisi kwa mhalifu kuvunja.

# Madaktari bingwa watoa huduma za matibabu bure

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAMIA ya wakazi wa Mji mdogo wa Mto wa Mbu kutoka familia zisizo na uwezo wamepata huduma ya matibabu ya magonjwa bure kutoka kwa madaktari bingwa.

Idadi kubwa ya wagonjwa hao waligundulika wakisumbuliwa na matatizo ya macho na shinikizo la damu hali inayotajwa kusababishwa na mazingira wanayoishi.

Huduma hiyo ya matibabu iliratibiwa na Klabu ya Lions tawi la Arusha wakishirikiana na Hoteli ya Serena.

Matibabu hayo yaliyolenga maeneo ya pembezoni yamekuwa na manufaa makubwa baada ya idadi kubwa ya watu waliojitokeza kupata vipimo mbalimbali kwa ajili ya kutambua afya zao, Mratibu wa matibabu hayo Klabu ya Lions, Chief Masanya Yusuf, alisema wamefikia maamuzi hayo baada ya kuguswa na hali za wakazi hao na kwamba wagonjwa watakaogundulika kuathirika zaidi watapatiwa rufaa na huduma ya bure ya upasuaji.

Alisema katika utoaji wa matibabu ya bure wanalenga maeneo ambayo wanaamini yana mahitaji hasa maeneo ya vijijini kwani asilimia kubwa ya watu hawana utamaduni wa kucheki afya zao kutokana na hali duni ya maisha.

Akizungumzia utoaji wa huduma ya matibabu kwa jamii za pembezoni, mwanachama wa Klabu ya Lions, Satish Sharma, alisema ni mwaka wa tatu mfululizo wamekuwa wakitoa matibabu bure ambayo yamewaponyesha wengi waliokuwa wanasumbuliwa na magonjwa mbalimbali.

Sharma aliwataja wadau wengine wanaoshirikiana nao katika utoaji wa huduma hiyo kama Anant Knetia na marafiki wengine kutoka Uingereza.

Kwa upande wake, Meneja wa Hoteli ya Serena, Nickson Kanyika, alisema awamu ijayo ya utoaji wa matibabu watalenga maeneo ya Ngorongoro kwani utafiti walioufanya wamegundua kuwa wananchi wa maeneo hayo wanahitaji msaada wa matibabu.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Kirurumo, kinachohudumia eneo hilo Dk Elisha Raphael, alisema idadi kubwa ya wagonjwa waliopatiwa matibabu wamegundulika kuwa na magonjwa.

Baadhi ya wananchi waliopatiwa matibabu hayo bure walisema yamekuja wakati mwafaka kwa kuwa wengi wao hawana uwezo wa kifedha kuygharamia.



Meneja Uhusiano na Mawasiliano ya Nje wa kampuni ya Saruji ya Tanga (TCPLC), Mtanga Noor (kushoto), akikabidhi msaada wa mifuko 200 ya saruji yenye thamani ya 2,139,000/- kwa Kamishna Msaidizi wa Polisi Mkoa wa Tanga, Leonce Rwengazira (kulia), iliyotolewa na kampuni hiyo kusaidia ujenzi wa nyumba za polisi wilayani Kilindi, mkoani humo, katika hafla iliyofanyika kiwandani hapo, Pongwe jijini Tanga jana. Wengine ni maofisa wa kampuni hiyo pamoja na maofisa kutoka katika jeshi hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bidhaa za viwandani zinazouzwa Kenya zaongezeka

**Na Novatus Makunga,** NAMANGA

BIDHAA za viwandani zinazouzwa nje ya nchi kupitia mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Namanga, mkoani Arusha, zimeongezeka katika kupindi cha mwaka mmoja na nusu uliopita kutoka tani 21,478 hadi 26,690.

Meneja Msaidizi wa Mamlaka ya Mapato Nchini, (TRA), mkoani Arusha, anayeshughulikia forodha, Godfrey Kitundu, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na tathmini ya mwaka mmoja na nusu baada ya kuanzishwa kwa Kituo cha Huduma kwa Pamoja Mpakani, (OSBP), cha Namanga.

Alisema baada ya kituo hicho kuanza kutoa huduma mnamo Oktoba 2017, kumepunguza kero hasa ya mizigo na wasafiri kuchukua muda mrefu mpakani na pia kurahisishiwa kutumia fursa za Jumuia ya Afrika ya Mashariki, (EAC), katika biashara na hivyo kuongeza hamasa kwa wafanyabiashara na wazalishaji wa nchini.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, malori yaliyosafirisha bidhaa kwenda Kenya kupitia mpaka huo yalikuwa 1,268 huku magari hayo makubwa ya mizigo yakiongezeka kufikia malori 1,585 katika mwezi Machi wa mwaka huu wa fedha wa 2018/2019.

Alifafanua idadi ya bidhaa zilizoongezwa thamani kwa kusindikwa na viwanda vya ndani zinazouzwa nje kupitia mpaka wa Namanga zimeongezeka kutoka bidhaa 429 kwa mwaka 2016 na kufikia bidhaa 640 kwa mwaka jana.

Kitundu alizitaja baadhi ya bidhaa za viwandani zinazoongozwa kwa mauzo ya nje kupitia mpaka wa Namanga kuwa ni pamoja na marumaru za sakafuni na ukutani za kiwanda cha kampuni ya Goodwill Tanzania Ceramic Ltd, kilichopo wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani.

Alizitaja bidhaa nyingine kuwa ni pamoja na vinywaji vya matunda na vya kuongeza nguvu, unga wa ngano na sembe, konyagi, playwood, marine boards na kraft liner.

Aidha, Kitundu alisema pia bado kuna uuzaji mkubwa nje ya nchi wa mbogamboga, matunda, mashudu ya pamba, tangawizi pamoja na madini ya viwandani yakiwamo makaa ya mawe na chokaa.

Alisema mauzo ya bidhaa hizo ambazo zinapitia Namanga zina thamani ya wastani wa Sh. bilioni 25.1 kwa mwezi.

Kwa upande wa bidhaa zinazoingia nchini kutoka nchi jirani ya Kenya alizitaja kuwa na ujazo wa tani 4,190 kwa mwezi zikiwa na thamani ya Sh. bilioni 25. Aidha, Kitundu alisema kuanzishwa kwa kituo hicho kumewezesha kuwabana wafanyabiashara waliokuwa wanakwepa kulipa kodi na tozo za serikali na hivyo kuongeza mapato.

"Thamani ya bidhaa zilizokamatwa zikiingizwa nchini pasipo kufuata taratibu zimepungua kutoka za zaidi ya Sh. milioni 630.3 kwa mwaka 2015/16 hadi kufikia bidhaa za zaidi ya Sh. milioni 24.7 kwa mwaka 2017/18," alifafanua.

# Ufugaji nyuki waleta neema

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

ZAIDI ya wakazi 300 katika Halmashari ya Hanan'g na Mbulu, wameanza kunufaika na mradi wa ufugaji nyuki na utunzaji wa mazingira baada ya kuwezeshwa na mtandao wa vikundi vya wakulima Tanzania, (Mviwata).

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana, Afisa Miradi wa Mviwata, Donald Laizer, alisema kupitia mradi wa STRONG, (Sustainable Transfomation opportunity Networking and Growth) ambao unafadhiliwa na Shirika la Trias kutoka nchini Ubelgiji wameanzisha vikundi vitano ambavyo vinashiriki mradi huo katika Halmashauri za Hanan'g na Mbulu.

Afisa huyo alisema mradi huo unawalenga wanawake na vijana kwa kuwa makundi haya mawili yamekuwa yakisahaulika huku akitolea mfano wa wanawake kuwa wameshiriki katika kilimo lakini wanajikuta wakiambulia patupu kutokana na waume zao kutokuwapa chochote kilichotokana na mavuno. Kuhusu vijana alisema wamewashirikisha kwenye mradi maana walikuwa wanaachwa kwa kisingizio hawajaanza kumiliki ardhi. Alivitaja vikundi wanavyofanya navyo kazi kuwa vipo maeneo ya Endasaki na Endagaw kwa upande wa Halmashauri ya Hanan'g na Halmashauri ya Mbulu ni Dongobesh, Dirmu na Bashay ambapo kila kikundi alisema kina wanakikundi 60.

Katika mradi huo alisema wanalenga ufugaji nyuki lakini kutunza mazingira ambapo kabla hawajaanza walipewa mafunzo ya ufugaji nyuki kwa njia za kisasa na akadai wamewaoteshea miche ya miti ambayo wanavikundi wanapewa ili wapande kwenye maeneo ambayo watafugia nyuki hao.

"Mradi huu wa ufugaji nyuki unatunza mazingira kwa asilimia 100 ndio maana tunawapa miche ya miti ambayo inavutia nyuki na nyuki siyo mharibifu wa mazingira na hawezi kukaa kwenye jangwa au sehemu yenye upepo," alisema.

Alifafanua kuwa tokea mradi huo uanze mwaka 2016, wanavikundi wamepanda miti zaidi ya 8000 ambayo inasaidia kutunza uoto wa asili na kuwapatia chakula nyuki ambapo anadai miti hiyo pia wanaweza kuuza na kujipatia fedha hivyo watakuwa wamepata faida kwa kuuza asali lakini watapata mbao. Alisema Mviwata wameweza kuwapatia mizinga 208 vikundi vyote ambapo mizinga hiyo ni aina ya Top bar na Long trof ambayo inawapa fursa hata wanawake kuipandisha juu ya mti siyo mpaka uwe na uwezo wa kuitundika kwenye miti juu.

Alisema vijana wanafurahia ufugaji wa nyuki kwa kuwa wanapenda kupata fedha za haraka huku akitolea mfano kuwa mfugaji wa nyuki anaweza kuvuna asali kuanzia miezi sita mpaka nane toka nyuki waingie kwenye mizinga.

Alisema mizinga yao ni ya kisasa ambayo wanaweza kuvuna mara mbili hadi mara tatu kwa mwaka.





# DC atinga mnadani kugawa vitambulisho vya Magufuli

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya 'ametinga' mnadani na kugawa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, zaidi ya 500 ambao ni wafugaji.

Ole Sabaya jana alifika katika mnada wa mifugo uliopo karibu na Uwanja wa Ndege Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na kugawa vitambulisho hivyo kwa wafugaji wa jamii ya Kimasai.

"Sasa sikilizeni nyie wafugaji, mheshimiwa Rais Magufuli amechapisha vitambulisho hivi kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara wadogo kutobugudhiwa. Zaidi alisema: "Leo nimekuja hapa nataka kila mtu awe nacho na kinatolewa kwa bei ya Sh. 20,000 tu." Kabla ya kuwafuata wafugaji hao, Mkuu huyo wa Wilaya alianza kwa kupita ofisi zote za Halmashauri ya Wilaya ya Hai na kugawa vitambulisho vitano kwa kila Mkuu wa idara na kutakiwa kuwafuata wafanyabiashara na kuwasilisha makusanyo Jumatatu ya Aprili 15 mwaka huu.

Vitambulisho hivyo ambavyo vimechapishwa na Rais John Magufuli, vina lengo la kuwatambua wafanyabiashara wadogo na kuhakikisha wanafanya shughuli zao bila kusumbuliwa.

Uamuzi wa kutoa vitambulisho hivyo kwa kila mkoa na kila mfanyabiashara mdogo nchini, ulifanywa Desemba 10 mwaka jana na Rais Dk. John Magufuli, wakati wa mkutano wake na watendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wakuu wa mikoa yote nchini. Mara kadhaa, Rais Magufuli amekuwa akinukuliwa akisema kuwa mfanyabiashara yeyote ambaye mapato yake kwa mwaka hayazidi Sh. milioni 4 atakayekuwa na kitambulisho hicho asibughudhiwe.




Mkuu wa Jeshi la Polisi - Inspector General of Police (IGP), Simon Sirro, akipokea mfano wa funguo kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani, Meja Jenerali Jacob Kingu, baada kupokea majengo saba yaliojengwa kwa ufadhili wa serikali ya China, katika Chuo cha Taaluma ya Polisi mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Mwalimu adakwa Takukuru kwa kujifanya ofisa wa NIDA

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoani Kilimanjaro (Takukuru), inamshikilia Hemed Shaban anayedaiwa kujifanya Ofisa wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) katika Wilaya ya Moshi kwa ajili ya uchunguzi.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kilimanjaro, Holle Makungu amesema Shaban anadaiwa kujitambulisha kama Ofisa wa NIDA.

Alisema mtu huyo ambaye si mtumishi wa NIDA amekuwa akijipatia fedha isivyo halali kupitia vitambulisho hivyo.

Makungu alisema Aprili 9 mwaka huu walipokea taarifa kutoka kwa mwananchi mmoja, akieleza kuwa anadaiwa rushwa ya Sh. 100,000 na Ofisa wa NIDA ili apewe kitambulisho.

Kwa mujibu wa Makungu, Afisa huyo feki, alifanya kosa hilo huku akijua ni kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Makungu alisema mtego ulioandaliwa ulisaidia kukamatwa kwa Shabani ambaye amekuwa akijitambulisha kuwa ni Ofisa wa NIDA.

"Uchunguzi unaonyesha Hemed ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiusa iliyopo Manispaa ya Moshi ambapo uchunguzi zaidi unaendelea ili kubaini watumishi wa NIDA wanaohusika kumpa vitambulisho hivyo kitendo ambacho ni kinyume na kifungu cha 31 cha sheria ya kuzuia na kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007," alisema Makungu.

Alidai kuwa uchunguzi utakapokamilika hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wale wote watakaobainika kujihusisha na uvunjaji huo wa sheria, huku pia akitoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema vitambulisho vya uraia wa Tanzania vinavyotolewa na NIDA ni bure na yeyote atakayedaiwa fedha atoe taarifa ofisi za Takukuru au wapige simu ya bure ya Takukuru ambayo ni 113.

# Wazalishaji mifuko mbadala wahamasishwa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk.Anna Mghwira amewataka wazalishaji wa mifuko mbadala ambayo ni rafiki wa mazingira kuchangamkia fursa ya kuzalisha kwa wingi ili kukidhi mahitaji.

Mkoa wa Kilimanjaro tayari umezuia matumizi ya mifuko hiyo ya plastiki.

Dk. Mghwira alisema hayo jana, wakati alipotembelea maonyesho ya wiki ya elimu katika Uwanja wa Mashujaa katika Manispaa ya Moshi.

Akiwa katika eneo hilo alisema kuwa wajasiriamali wanaotumia vifungashio vya mifuko ya plastiki wanapaswa kujiandaa mpaka muda uliopangwa na serikali mwezi Juni mwaka huu waweze kuondokana na matumizi ya plastiki.

"Kwa sasa mkoa wa Kilimajaro ni marufuku kutumia mifuko ya plastiki, tumeanza mapema ili watu wajiandae ikifika mwezi Juni mwaka huu watu wawe kwenye mstari na kuzoea kutumia mifuko mbadala. Tunashukuru wenzetu wa Harsho Group wameanza kuzalisha mifuko ya kutosha, " Alisema Dk. Mghwira

Mratibu wa Masoko Kampuni ya Harsho Group inayozalisha vifungashio mbadala, Caroline Satsif alisema kwa mkoa wa Kilimanjaro wamejiandaa vyema kuzalisha mifuko ambayo ni rafiki kwa mazingira na kuisambaza kwa bei nafuu.

Caroline alisema kuwa wanazalisha mifuko 500,000 kwa siku ambayo inatosheleza mahitaji ya mkoa wa Kilimanjaro na mikoa jirani na ndani ya nchi.

Anaeleza kuwa mifuko hiyo inaweza kufuliwa zaidi ya mara tano na iwapo ikitupwa inaweza kuoza na kuwa mbolea katika ardhi.

Mkazi wa Manispaa ya Moshi, Roman Mnzava alisema kuwa hatua ya Mkoa wa Kilimanjaro kupiga marufuku matumizi ya plastiki utasaidia kuokoa mazingira na hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ambao ni kitovu cha utalii mkoani hapa.





Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe (kushoto), akizungumza wakati wa kufungua mafunzo kwa maafisa elimu Kata wa mikoa ya Singida na Dodoma yanayoendelea katika kituo cha Chuo cha Ualimu Bustani Wilaya ya Kondoa, Mkoani Dodoma juzi. Kulia ni Kaimu Mkurungenzi wa Elimu Msingi, Paulina Mkonongo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge aomba ongezeko bajeti uchaguzi wa mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ameiomba serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa ili changamoto zilizojitokeza kipindi cha nyuma zisijitokeze tena.

Akichangia Hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI) kwa mwaka 2019/2020, Chikota alisema ni vyema Tamisemi ikatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia uchaguzi huo.

"Tuna uzoefu kwenye chaguzi zilizopita zilitengwa fedha ndogo na halmashauri kuambiwa waongezee kiasi kilichobaki,"alisema.

Alisena kuwa Halmashauri nchini uwezo wake unafahamika hivyo wasipewe mzigo hivyo fedha zitengwe za kutosha ili uchaguzi ufanyike kama ulivyopangwa na kukamilika bila kuwepo dosari yoyote.

Akizungumzia kuhusu Wakala wa Barabara mijini na Vijijini(Tarura), Mbunge huyo alisema Tarura inafanya kazi kubwa na imeonyesha mafanikio lakini ina changamoto ya uhaba wa fedha na watumishi.

"Walipewa watumishi wachache kutoka mamlaka za serikali za mitaa na kutengeneza pengo kwenye uhaba wa wahandisi nashauri ifisi ya Rais Tamisemi kwa kushirikiana na utumishi wa umma watoe kibali ili Tarura wapate watumishi,"alisisitiza Chikota.

Pia, aliishauri ofisi ya Rais Tamisemi kutatua changamoto ya wakuu wa idara ambao wamekuwa na makaimu wengi kutokana na uwepo wa malalamiko mengi ambayo yanatolewa na wakurugenzi kwamba suala la upekuzi linachukua muda mrefu.

"Kwa hiyo hili suala la upekuzi kama walivyosema wajumbe wengine tuliwekee mkakati ili ufanyike kwa muda mfupi na wenye sifa waweze kuteuliwa,"alisema Chikota.

Naye, Mbunge wa Kilindi(CCM), Omary Kigua, alishauri kuwa Tarura ibaki ilipo isipelekwe kwa madiwani kama ilivyodaiwa na baadhi ya wabunge kwa kudai kuwa kutakuwa na vurugu nyingi.

Alisema changamoto iliyopo ni kuwa Tarura haina usimamizi wa kutosha na kwamba hakuna chombo cha kusimamia kazi zake.

"Wapo waliosimama hapa na kusema kuwa Tarura ibaki kwa madiwani, mimi nasema ibaki palepale ilipo sio kurudishwa kwa madiwani maana ikirudi kule kutakuwa na vurugu nyingi tatizo lililopo sasa wamekosa usimamizi mzuri kwakuwa hakuna chombo cha kuisimamia,"alisema.

Alisema meneja wa tarura anasimamia barabara za halmashauri lakini ni nani anasimamia kiwango cha ubora wa Tarura.

Alisema kuna upungufu wa bajeti huku akitolea mfano jimbo lake la kuwa kiasi cha fedha cha ujenzi wa barabara walichotengewa wakala huo katika jimbo lake la Kilindi ni kidogo huku ikiiomba serikali itazame suala hilo ili kuongeza fedha.

"Kiuhalisia fedha zilizotolewa kwa jimbo langu ni kidogo sana na kula ni mabonde na milima na wenye kusema wamesema kwamba nendeni muone mara moja kuliko kusikia mara nyingi ,"alisema.

Aliongeza kuwa nyakati za mvua magari hayapiti kutokana na miundombinu ya barabara kuwa mibovu na kuomba serikali kutazama suala hilo badala ya kukaa ofisini ili kuona hali halisi.

# Naibu Waziri awapa kazi makamishina TCDC

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, amewataka Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC) na Viongozi wa Bodi za Mazao kuweka Mkakati wa pamoja wa kumsaidia Mkulima ili kuongeza tija katika uzalishaji na uuzaji wa mazao.

Bashungwa aliyasema hayo jijini Dodoma wakati akifungua kikao kazi cha Makamishna wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na viongozi wa bodi za mazao ambapo alisema kuwa wanatakiwa kumsaidia mkulima kupata pembejeo ambayo itamwezesha katika kuzalisha mazao bora.

"Hakikisheni mnakuwa na mkakati wa pamoja wa upatikanaji wa pembejeo, uhakika wa masoko na namna bora ya kuhifadhi mazao ya wakulima ikiwemo ujenzi wa maghala," alisema Bashungwa.

Aidha, alisema kuwa mfumo wa ushirika ukitumika vizuri utawasaidia wananchi kupata masoko ya mazao yao ndani na nje ya nchi na ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi za Mazao kutafuta masoko ya bidhaa za wakulima na kuacha kuwategemea viongozi wa juu wa serikali kuingilia katikati kutatua changamoto za wakulima. Kwa upande wake mwenyekiti wa tume hiyo, Dk. Titus Kamani alisema kuwa lengo la kikao hicho ni kutafsiri kwa pamoja ujenzi na uchumi wa kilimo kupitia dhana ya ushirika na kuondoa mazingira ya migogoro inayojitokeza ili kuepuka kujitokeza tena.

"Tumeona juhudi zinazofanywa na serikali katika kumsaidia mkulima kunufaika na shughuli zake za kilimo kupitia sekta ya ushirika na mabadiliko kwa baadhi ya maeneo japo kuwa bado kuna changamoto," alisema Dk. Kamani.

Aidha, Dk Kamani amehimiza upatikanaji wa masoko bora kuhakikisha mazao yote ya kimkakati na yale yasiyo ya kimkakati yanaingizwa pamoja na mfumo wa stakabadhi za ghala, mfumo wa soko la bidhaa na mingine kulingana na aina zao na mfumo wa biashara ulivyo

## Serikali yaonya maofisa elimu kata nchini

**Na Ibrahim Joseph,** KONDOA

SERIKALI imewaonywa Maofisa elimu Kata nchini kuwa watapimwa utendaji kazi wao kutokana na matokeo ya mitihani ya wanafunzi wa darasa la nne itakayofanyika mwaka huu.

Onyo hilo limetolewa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe wakati alipokuwa akifungua mafunzo kuhusu elimu endelevu kwa Maafisa elimu Kata wa Mkoa wa Singia yanayoendelea katika Chuo cha Ualimu Bustani Kondoa mkoani hapa.

" Serikali imetoa fedha nyingi kugharamikia mafunzo haya hivyo kila afisa elimu kata nchini tutampima utendaji wake wa kazi kutokana na matokeo ya mitihani ya wanafunzi wa darasa la nne mwaka huu asipofikia malengo ataonekana hatoshelezi kwenye nafasi hiyo, " alisema. Alisema kuwa baada ya mafunzo hayo kila afisa elimu kata anatakiwa kuandaa mpango kazi wake wa kutoa mafunzo kwa walimu wa shule zilizopo katika eneo lake na mwisho kufanya tathimini ya matokeo ya mafunzo hayo.

Aidha, alisema watendaji wote wa ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), wamekubaliana kurudisha heshima ya shule za serikali kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Alisema miaka hiyo wazazi wengi hawakupeleka watoto wao shule za binafsi waliziamini shule za serikali lakini kwa miaka ya karibuni hata mtoto akichaguliwa shule za serikali anachagua kwenda shule binafsi. Alisema ili kufikia mafanikio hayo serikali imeanza kwa kutoa mafunzo kwa maafisa elimu kata ili baada ya mafunzo wakawafundishe waalimu wengine katika maeneo yao.


Katika kuhakikisha wanafikia malengo ya kuboresha elimu wizara hizo mbili zimekubaliana kutekeleza malengo mbalimbali kwa upande wa elimu ya awali na msingi. Malengo hayo ni kuhakikisha wanafunzi wote wa darasa la kwanza na pili wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) katika kiwango stahiki.

Lengo lingine ni kuhakikisha wanafunzi wa darasa la nne wanafaulu mitihani yao kitaifa kwa asilimia 100 na kwa wanafunzi wa darasa la saba kufikia asilimia 80.

Aliongeza kuwa lengo lingine kwa shule za msingi ni kuhakikisha uwepo wa walimu wenye sifa na weledi wa kufundisha elimu ya awali na mtaala wake ufuatwe kama uliv yoandaliwa na Taasisi ya elimu Tanzania.

Kwa elimu ya sekondari wamekubaliana kuwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya kidato cha pili ufikie asilimia 90 na kidato cha nne asilimia 80 na ifikapo mwaka 2025 shule zote za sekondari za serikali pasiwapo na daraja la nne na sifuri. Kwa upande wake msimamizi mkuu wa mafunzo kutoka Chuo cha Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), Lucas Mzelela, alisema jumla ya maofisa elimu kata 3,915 wamewezeshwa mafunzo hayo katika maeneo mbalimbali nchini na mikoa ya Dodoma na Singida watawezeshwa 339.

Aliyataja maeneo mengine kuwa ni Adem Bagamoyo na Mbeya, chuo cha ualimu Patandi, Tabora, Shinyanga, Butimba, Sumbawanga, Mtwara na shule ya sekondari Njombe,





# Rais Shein ataka kuendelezwa misingi muungano Tanzania

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa wakati Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatimiza miaka 55 ni vyema misingi ya Muungano ikaendelezwa ikiwa ni pamoja na kuiimarisha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Dk. Shein aliyasema hayo Ikulu mjini Zanzibar, wakati alipofanya mazungumzo na Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki aliyefika Ikulu ikiwa ni pamoja na kupokea maelekezo na miongozo kutoka kwa Rais kufuatia kuteuliwa kushika wadhifa huo hivi karibuni.

Alieleza kuwa waasisi wa muungano huo waliweka misingi madhubuti, hivyo ni vyema kuimarishwa na kuendelezwa misingi hiyo ambayo imeupelekea Muungano wa nchi mbili hizo kuwa imara, madhubuti sambamba na kuleta maendeleo endelevu kwa pande zote mbili. Alieleza kuwa miongoni mwa misingi hiyo ni pamoja na ushirikiano katika masuala ya diplomasia ikiwa ni pamoja na mashirikiano na mataifa ya nje chini ya taasisi inayohusiana na mambo ya nje ambayo kwa hivi sasa ni Wizara hiyo ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Rais Dk. Shein alieleza kuwa wizara hiyo ina umuhimu mkubwa katika kuendeleza masuala ya kidiplomasia hivyo ushirikiano wa pamoja unahitajika kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili liweze kufikiwa lengo lililokusudiwa. Alieleza kuwa azma ya wizara hiyo kuanzisha utaratibu wa kubadilishana uzoefu kati ya watendaji wa wizara hiyo wa upande wa Zanzibar na wale wa Tanzania Bara kuja Zanzibar kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupanua wigo wa kiutendaji na mashirikiano.

Naye Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi alimueleza Dk. Shein kuwa wizara yake mbali ya kujikita na masuala ya mahusiano na mataifa ya nje pia ni sikio na jicho la mambo yote yanayohusu Muungano na yale yasiyohusu Muungano kutokana na umuhimu wake.

Profesa Kabudi alisema kuna kila sababu ya kuiendeleza misingi ya Muungano ambao unatimiza miaka 55 mnamo Aprili 26 mwaka huu ambapo misingi hiyo imeleta mafanikio na maendeleo makubwa kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakati huo huo, Rais Dk. Shein alimuonesha Profesa Kabudi chumba maalum kilichotumika kwa hatua za awali na viongozi waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa ajili ya kutia saini makubaliano ya Muungano.




Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Benjamin Sita (kushoto), akizungumza kabla ya kuzindua Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), kilichopo Kijitonyama, jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Omar Nundu na Afisa Mkuu wa Masoko na Mauzo, Ally Mbega. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwenyekiti ataka viongozi CCM kuwa wakweli

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa Matawi, Kata na Majimbo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)wametakiwa kutoa ripoti zinazoonyesha uhalisia na usahihi ili kama kuna mapungufu yaweze kufanyiwa kazi na siyo kuyaficha kwa kuhofia aibu.

Akizungumza na wajumbe wa kamati ya siasa ya halmashauri kuu ya chama hicho, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini, Talib Ali Talib, alisema ripoti ambazo zinahitajika ni zile zinazoweza kufanyiwa kazi na sio ripoti za kufurahisha watu

Alisema ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya viongozi wanaanda ripoti zinazoonyesha mambo mazuri pekee na kuuficha ukweli kwa kuhofia aibu kitu ambacho hakiwezi kujenga chama. Aidha, alieleza kuwa ripoti ni kitu muhimu inayoonyesha uhalisia hivyo ni vyema kama kuna mapungufu kuyafichuwa ili yaweze kufanyiwa kazi kwa faida ya CCM na wananchi kwa ujumla. "Tumechoka kupokea maripoti yanayoonyesha mazuri tunataka ripoti zenye mapungufu ili tuweze kuyafanyia kazi matatizo ya Wananchi",Alisema Mwenyekiti huyo.

Alisema kuwa chama hicho kipo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wake hivyo kutoa ripoti kwa ajili ya kusifia viongozi na kuuficha ukweli ni kwenda kinyume na katiba na maadili ya CCM.

Hata hivyo aliwataka wananchama na viongozi wa Jimbo la Mpendae kuwakataa Viongozi wanaopita wakiwanadi wagombea wakati muda haujafika na baadae wapeleke taarifa sehemu husika ili chama kiweze kuwafanyia kazi.

Kwa upande wake Katibu wa CCM Jimbo la Mpendae Abdallah Ahmad , alisema tayari viongozi wa jimbo hilo wameshatekeleza ilani ya CCM kwa zaidi ya asilimia 96 katika sekta ya Maji, Umeme na kuwapatia posho Mabalozi wa Mashina.

Wakitoa maelezo katika ziara hiyo baadhi ya Viongozi wa Matawi,Wadi na Jimbo la Mpendae walisema licha ya utekelezaji huo wa ilani uliotajwa lakini bado wanakabiliwa na matatizo ikiwemo ubovu wa barabara za ndani na baadhi ya watendaji kushindwa kuwajibika ipasavyo jambo ambalo linapelekea kushidwa kufanya kazi kwa ufanisi.

# Wanufaika TASAF watakiwa kuendeleza miradi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WANANCHI wanaonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF) wametakiwa kutunza na kuiendeleza miradi waliobuni na kutekelezwa na serikali ili iendelee kuwahudumia na kuwanufaisha mara baada ya kumalizika kwa kipindi cha miradi hiyo. Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Shaaban Seif Mohamed alieleza hayo wakati alipokuwa katika ziara maalum iliojumuisha Wilaya ya Magharibi "A"na Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa lengo la kukagua miradi hiyo ya TASAF awamu ya tatu na kusikiliza changamoto zinazowakabili wananchi hao ili kuzipatia ufumbuzi.

Katibu Mkuu huyo alisema, serikali imekuwa mstari wa mbele katika kuwaanzishia wananchi wake miradi mbali mbali lakini hujitokeza changamoto ya kuilinda na kuendeleza miradi hiyo pale serikali inapoiwacha mikononi mwa wananchi pindi miradi inapofikia ukingoni.

Akikagua kituo cha afya kilichopo Kianga na nyumba ya Madaktari iliopo Matamwe Kijini ambavyo vyote vimesaidiwa kupitia mradi wa TASAF, alisema wananchi wanapaswa kuiendeleza miradi hiyo kwa niaba ya serikali na wasisite kuwachukulia hatua endapo watawaona watu wasiokuwa waaminifu wakiharibu miradi yao.

"Baadhi ya watu hawathamini jitihada za serikali ambazo zinalenga kuwaletea maendeleo wananchi wake, hivyo hufanya hujuma za makusudi nawaombeni msisite kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria za nchi" Alieleza Katibu Shaaban.

Katika ziara hiyo pia alitembelea mradi wa Kilimo katika bonde la kizimbani, bonde ambalo mpango wa kunusuru kaya maskini umeliendeleza kwa kuligawa kwa kujenga matuta maalum na kuweka miundombinu ya kupitishia maji. Kwa upande wao walengwa wa mradi huo wameishukuru serikali kutokana na miradi walioanzisha imewaletea matunda kwa kupata kipato kinachowasaidia katika kutatua matatizo yanayowakabili.

Waliiomba serikali kuwapatia vifaa vitakavyowasaidia kuendeleza shughuli zao za kilimo ili waweze kuzalisha za kupata kipato cha ziada. Akiwa katika kijiji cha Kijini Katibu mkuu Shaaban alipokea changamoto inayolalamikiwa na wananchi hao juu ya kukosekana kwa daktari wa kudumu katika hospitali yao licha ya kuchukuwa jitihada ya kujenga nyumba maalum ya kulala daktari pamoja na kuweka miundombinu yote ikiwemo umeme, maji safi na salama.

Walisema kukosekana kwa daktari wa kulala kijijini hapo kumepelekea wananchi kupatwa na maradhi na nyakati za usiku kupata usumbufu wa kutafuta huduma masafa marefu.

Nae Mkurugenzi uratibu wa shughuli za serikali SMT na SMZ Khalid Bakar Amrani aliwaeleza wananchi hao kuwa hivi sasa serikali ipo katika mchakato wa kuwapelekea awamu nyingine ya TASAF.

Hata hivyo aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi kupitia kwa masheha katika shehia zao na kutoa taarifa sahihi zitakazoisaidia serikali kupanga mipango yake.

Ziara hiyo ya Katibu Mkuu imejumuisha Shehia za Kianga, Kizimbani, Donge Mbiji, na Matemwe Kijini ambapo amepata fursa ya kutembelea miradi ya ujenzi wa Vituo vya Afya na Kilimo iliyobuniwa na wanakaya husika.



**LAVALAVA MSIKIE DOGO HUYU**
Soma UK.15

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI APRILI 13, 2019



# JAY DEE KOMANDOO

## BASI SAWA



## Bad Girl unamtesa Baraka Da Prince!

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Baraka Da Prince, ameshindwa kufyatua video ya wimbo wa 'Bad Girl', kutokana na sababu zilizo juu ya uwezo wake.

"Nilipanga kuuweka katika audio tangu Februari mwaka huu nikitarajia kwamba isingechukua muda mrefu kushuti video, lakini kutokana na sababu zilizo juu ya uwezo wangu imebidi nisubiri kwanza," amesema.

Amesema kwa sasa ameamua kutulia kwanza nyumbani kwao Mwanza na kisha akijipange upya ili kuhakikisha anakamilisha mipango ya kushuti video hiyo mwaka huu wa 2019.



## Eti Chemical umetosa hizi!

RAPA wa kike, Chemical, ameachana na kutunga nyimbo za mapenzi na badala yake na kujikita zaidi katika zile zinazohusu mambo ya kijamii.

Amesema kila kitu kina mwanzo na mwisho, ambapo amefikia mwisho wa kuimba nyimbo zenye ujumbe wa mapenzi na kujikita kwingine ili kupata heshima zaidi katika sanaa.

"Kwa mfano nina wimbo uitwao 'Kilwa', unahamasisha kutembelea eneo hilo la kitalii, umenipa heshima kubwa, ndio maana nikaamua kuachana na nyimbo za mapenzi," amesema Chemical.



# Jay Dee ni komandoo bwana

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya, Lady Jay Dee, hataki mbwembwe za kuwa na mabaunsa katika kazi zake kama wafanyavyo baadhi ya wasanii.

"Mimi mwenyewe ni komandoo, hivyo sioni sababu ya kuwa na mabaunsa, katika shughuli zangu za muziki...ninajitosheleza," anasema Jay Dee.

Amesema katika shughuli zake za muziki amekuwa akizunguka na wasaidizi wake wachache na siyo mabaunsa wa kumlinda.


Msanii huyo kwa sasa ana kibao kipya alichokipa jina la 'I don't Care' ambacho anatarajia kukitambulisha wiki ijao.

## INSTA-TWITTER





**Natafakari** sana, maana muda ni mchache na mambo ni mengi-**Johari.**



**Mungu** atabaki kuwa Mungu tu. Ahsante kwa kila changamoto nilizozipitia kwenye maisha yangu. Kila njia niliyoipita ilikuwa na mafunzo ndani yake-**Shamsa Ford.**



## Lavalava tafadhali msikie dogo huyu

MSANII chipukizi, Tobi One, kutoka jijini Mwanza, amesema anatamani siku moja afanye kazi na Lavalava.

"Ninapenda sana uimbaji wake ila sijui itawezekana kumpata na kumshirikisha katika nyimbo zangu? Kwa kweli nina imani sana kufanya naye kazi," amesema Tobi One.

Anaamini wasanii wenye uwezo mkubwa wako wengi lakini anavutiwa zaidi na Lavalava na kwamba hana jinsi ya kukutana naye ili amuombe ampige tafu katika nyimbo zake.

"Nina nyimbo nyingi tu ambazo sijazirekodi, hivyo ninawatafuta wasanii kama Lavalava niwashirikishe ili niweze kuwa juu," amesema.


UNASEMAAA...

## Jimmy Master amekuwa kiona mbali

MKONGWE wa filamu za kivita, Jimmy Master, ameamua kupumzika kwa muda kuandaa vitu vipya baada ya soko la filamu nchini linayumba.

Jimmy Master, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Mzimuni Theatre Arts, amesema filamu ya mwisho kuingizwa sokoni na kundi hilo ni 'Foundation' iliyotolewa mwaka 2016.

"Kaka maisha haya ni lazima kujiongeza unapoona mambo yanakwenda ndivyo sivyo, na mimi nimeona ni bora nipumzike kwanza baada ya kuona soko la filamu haliendi vizuri," amesema Jammy Master.



## Tour Arts kutembeza bakuli

KUNDI la sanaa la Tour Arts Group, la mjini Mpanda mkoani Katavi, litafanya harambee ya kusaka Sh. milioni 10 liweze kushuti video ya filamu yake iliyopewa jina la 'Vita ya Ukoo'.

Mwenyekiti wa kundi hilo, Chen Lee, amesema harambee hiyo itafanyika wiki ijayo mjini Mpanda na likifanikiwa kupata kiasi hicho, mchakato wa kushuti video utaanza mara moja sehemu mbalimbali huko Mpanda na Sumbawanga.

"Katika filamu hii tutawashirikisha baadhi ya wasanii maarufu kama Riyama Ally, Magali, Seba na Bad Boy waongeze ujuzi wao," amesema Chen Lee.



BODA 2 BODA

## Maisha haya kujiongeza lazima

GIGY Money amedai kwamba anafanya kazi ngumu hivyo ni lazima awe makini katika matumizi ya pesa zake kwa ajili ya kujiletea maendeleo.

"Siyo siri kupata pesa katika kazi ya muziki kuna changamoto zake, hivyo ni lazima niwe makini kwenye matumizi," amesema Gigy Money.

Anakumbuka kuwa zamani alikuwa akitumia pesa zake vibaya kwa kununua vitu vya gharama kubwa, lakini sasa yuko makini katika matumizi.

Msanii huyo asiyeishiwa vituko, amesema katika kutafuta mafanikio ni muhimu kujiongeza ili kufikia mafanikio badala ya kubweteka tu.







@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Uzee** kudadadeki kha gym inanihusu mapaja yamekua... ntakomaa tu na watoto jamani-**Faiza Ally.**




**Asante** mungu wangu, nazidi kuuona ukubwa wa jina lako. Umekua mtetezi wangu na kunipa furaha bila kujali mitihani ninayopitia. Basi usinipite, endelea kunisimamia bila wewe hakuna kitu-**Sabrina Rupia.**



**Ungetaka** awe wa kwako peke ako ungemzaa wewe kwani sisi hatuna macho silembii-**Amber Lulu.**

# Kuumbe!

## SIMARO
### awaliza JB Mpiana, Koffi, Werrason



**Na Adam Fungamwango**

'MAYA najing'ata ulimi, damu inachanganyikana na mate kinywani, zingine natema zingine nameza, kizunguzungu kinapita, mara ya kwanza ulifanyiaga matata, nikavumilia, kama nisingekata tiketi kukufuata, hukutaka kurudia.'

Ni baadhi ya mashairi mazito yaliyo kwenye wimbo wa 'Maya' uliotungwa na gwiji la muziki kutoka Kongo, Lutumba Simaro Masiya aliyefariki dunia nchini Ufaransa Machi 30 mwaka huu.

Watanzania wengi wanaujua wimbo huu kwa sababu ulitafasiriwa na kuimbwa kwa Kiswahili na mwanamuziki Mafumu Bilal, lakini ukweli ni kwamba ngoma hiyo ilichukuliwa kutoka kwenye wimbo wa 'Maya' halisi uliopigwawa na TP OK Jazz chini ya hayati Luambo Luanzo Makiadi aka Franco, ikiwa ni utunzi wa brother Simaro.

Mafumu Bilali alichukua kila kitu. Aliutafasiri kama ulivyo kutoka Kilingala na kuweka kwenye Kiswahili, huku mirindimo na mapigo yakiwa ni yale yale ya TP OK Jazz.

'Mtu aliyekuwa akinipikia samaki, leo ananipikia nyoka, majivuno yote niliyokuwa najivuna yamekwenda na maji. Mungu aliumba neno mapendo, aliumba mateso, siendi kulia kwenye mvua ili machozi yabaki alama usoni. Hii yote ni kosa la mama alinizaa na wema, wema wa kupenda watu duniani, acha nidhulumiwe.'

Ni mwendelezo wa maneno mazito, yenye hisia za uchungu kutoka kwenye wimbo huo wa 'Maya'. Si wimbo huo tu, Afrika hususan Wakongomani wanamlilia Simaro kutokana na aina yake ya utunzi, kwani alikuwa akitunga nyimbo zenye mashairi mazito, hisia kali, maono na tafakari ya hali ya juu kiasi cha kuheshimika mno nchini Kongo.

Labda ni kwa vile kabla ya kuwa mwanamuziki alitaka kuwa Padri, akichunga kondoo wa Mungu kanisani.

Mwanamuziki huo mmoja wa waasisi na viongozi wa TP OK Jazz, akishirikiana na hayati Franco, alifariki dunia akiwa na miaka 81.

Mwaka jana alistaafu rasmi muziki na kulikabidhi gitaa lake la rhythm rais wa zamani wa Kongo Joseph Kabila kabla hajaondoka madarakani ili aliweke makumbusho na akafanywa kama alivyotaka.

Wanamuziki wengi nchini Kongo wamelia na kuguswa na msiba huo mkubwa wakiwemo Koffi Olomode, JB Mpiana na Ngiama Makanda Werrason.

"Sina la kusema, nina majonzi mengi, naona kama dunia imesimama," anasema Koffi.

"Muziki wa Kongo uko kwenye msiba mkubwa. Afrika imeondokewa na mmoja wa wasanii wake vinara kabisa. Dunia ya muziki imepoteza nembo. Wanamuziki tunakulilia mzee wetu." alisema JB Mpiana.

"Ningependa maneno yangu yaendane na hisia niliyonayo kutokana na msiba huu. Kumbukumbu niliyonayo kwa marehemu sina uwezo wa kufidia ukubwa na kipaji chake na ubora wa kazi yake ambayo kamwe haitoweza kusahaulika." Haya ni maneno ya Werrason.

Serikali ya Kongo imemteua mwanamuziki mkongwe nchini humo Kiamangwana Mateta Verckys akiambatana na wengine, Felix Wazekwa, Tshala Muana na Mbilia Bel, familia ya marehemu na ya hayati Hayati Franco, kwenda nchini Ufaransa kuuchukua mwili na kuurejesha nchini humo kwa mazishi.

Ujumbe huo ulitarajia kuondoka jana Ijumaa na kurejea Kongo kesho Jumapili. "Siwezi kujua mazishi yatakuwa lini, nadhani inaweza kuwa Aprili 16 au 17," wiki ijayo alisema Verkys. Ina maana mazishi ya nguli huyo mahiri wa kucharaza gitaa huenda yakawa Jumanne au Jumatano ijayo.


Kwa maisha yake yote ya muziki, Simaro alikuwa mpiga gitaa la kati au rhythm, mtunzi na mpangaji wa muziki.

Mbali na 'Maya', nyimbo nyingine maarufu ni 'Bisalela', 'Ofela,', 'Mabele','Cedou', 'Ebale ya Zaire' na nyinginezo.

'Siku nikifa hata kama binadamu watanikimbia, lakini inzi watanikimbilia.' Ni mmoja kati ya maneno yaliyo kwenye nyimbo aliyotunga iitwayo 'Mabele.'



## NGOMA MPYA 5 ZINAZOTIKISA BONGO


Baba Mondi

**Na Mwandishi Wetu**

KILA kukicha wasanii wanatoka studio na wengine wanaingia kurekodi ngoma mpya.

Kuanzia mwezi Machi kuna baadhi ya ngoma zimeipuliwa kutoja jikoni na kuanza kukonga mioyo ya mashabiki wa muziki, hasa wa kizazi kipya, maarufu kama bongo fleva.

Ngoma hizo kwa sasa zinatamba kwenye vituo mbalimbali za redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

Hizi baadhi ya ngoma mpya kabisa zinazobamba ambazo zimeachiwa kuanzia mwezi uliopita.

**Mwewe-Sungura ft Baba Mondi**

Hii ndiyo ngoma inayobamba sana na kusikilizwa na wengi hasa kwenye mitandao ya kijamii. 'Mwewe' ni wimbo uliotungwa na kuimbwa na msanii Sungura Madini na kutoka mwanzoni mwa mwezi Aprili, au mwezi huu.

Lakini umaarufu au umeonekana kwani unafuatiliwa na wengi kutokana na kumshirikisha Baba Diamond.

**Hallelujah-Willy Paul ft Nandy**

Msanii huyu hakuwa nyuma kwani mwishoni mwa mwezi Machi, ametoa ngoma yake mpya ambayo imeanza kubamba kwa mashabiki.

Ngoma inaitwa 'Hallelujah', akimshirikisha msanii Nandy.

**Your the Best-Ommy Dimpoz**

Baada ya kutoka na singo ya 'Ni Wewe', Ommy Dimpoz amerejea tena kwenye ulingo aliozoea wa muziki kwa kutoa ngoma nyingine anayoiwta 'Your The Best'. Ikumbukwe kwa muda mrefu msanii huyo alikuwa nje ya gemu akipigania afya yake, baada ya kile kinachosadikiwa kula au kunywa sumu bila yeye kujua. Ngoma hii kaitoa Machi 25.

**Yente-Dogo Janja**

Dogo Janja naye hajabaki nyuma. Mwezi Machi naye ameutambulisha mzigo mpya ambao ameubatiza jina la 'Yente'.

Kama kawaida yake amechana mistari kisawasawa na hajawahi kukosea.

**Niteke-Harmonize**

Huyu ndiye Harmonize. Mwezi mmoja ametoa ngoma mbili. Ya sasa inaitwa 'Niteke'. Ni ya mapenzi ambayo anazungumzia jinsi alivyomzimikia mwanadada na kumwambia afanye anavyotaka.

Ni maneno ambayo huzungumzwa na wapenzi, kila mmoja anapotaka kutoa hisia zake kwa mwenzake.


Willy Paul na Nandy


Ommy Dimpoz


Dogo Janja


Harmonize

# Vijimambo

## PICHA ILIYOPITA



1. Siku hizi nakamata swala kidigitali, sitimui mavumbi - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Kwa mwendo huu, safari hii nitakoma - Majuto Magazeti, Iringa.
3. Ukakamavu uliotukuka - Shirima, Morogoro.
4. Ushazoea kunionea, leo acha nikupindue pindue mpaka ujute - Mama Nah, Manzese DSM.
5. Daaah, kama wanacheza ku-fu! Kweli kutolewa na kutoa roho si mchezo - Judith Kigosi, Sinza.
6. Hapa situi chini, nikitua tu nimeliwa, nabaki hapa hapa hewani - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
7. Haya sasa, mi nangojea nione tu nani atashinda hapo - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Duuuh, hatari na si salama kwa swala wa watu - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
9. Hivyo hivyo swala, mpindue huyo chui mpaka achoke. Usikubali kuliwa - Dotto Gumbo, Muheza Tanga.
10. Hii ni kama msomo usemao; "ukiona mambo hayaendi, basi nenda wewe" - Bajom, Kiwalani DSM.
11. Kila mmoja amekua mjanja. Huwezi kunifanya mboga kirahisi rahisi - Agatha Mbale, Moro Town.
12. Windo la kibabe - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
13. Huo ni uzoefu wake na juhudi yake ya kujishibia - Frank S.J. Kimati, Mbauda Arusha.
14. Asiyefanyakazi na asile - Mfaume Mbugi, Mshindo Iringa.
15. Wewe ndio kitoweo changu, tena hapa hutoki - Dokta Student Muhas, DSM.
16. Hapa namsumbua, akichoka natoka mbio si za mbuga hii - Doe Mashoto, Mikindani Mtwara.
17. Maisha porini si kutafuta ni kutafutana. Ukizubaa hausemwi, unaliwa - Beneali Moussa, Zenji.
18. Hapa siondoki mpaka nione mwisho wa mchezo - Exaud Mbando, Arusha.
19. Namwaminia sana swala kwa michezo hii, chui lazima ale vumbi leo - Exaud Mbando, Arusha.
20. Walimwengu niamlieni jamani, mbona mnaniangalia tu, nitaliwa na chui hivyo! - D Ndole, Rozana Buguruni.
21. Nishamla nyani anayeruka sana mitini, utakua wewe swala! - Beatrice Mbando, Sakina Arusha.
22. Daaah, hii ione tu pichani usiombe yakukute na wewe - Hamisi Ndole, Rozana Buguruni.
23. Hapo Wachina wanaangalia staili, sisi Waswahili tunaleta huruma! - Mama Nadia, Manzese DSM.
24. Asiyejipenda akatishe katikati yao aone kilichowafanya wanyama wengine wasiingilie - Jutto Jittu, DSM.

**SMS Bomba ya Leo:**

**Asiyejipenda akatishe katikati yao aone kilichowafanya wanyama wengine wasiingilie - Jutto Jittu, DSM.**

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Penzi kamwe haligawanyiki

**Na Adam Fungamwango**

KITU kinachoitwa penzi siku zote huwa hakigawanyiki. Vijana Jazz Band, Wanasaga rumba waliwahi kutunga nyimbo iitwayo 'Penzi Haligawanyiki' na baadhi ya mashairi yake ni haya:

'Dunia hii yote inagawanyika, mali na shamba pia vinagawanyika, lakini siyo penzi, litafanya kila njia upande mmoja litazidi.'

Hapa ina maana yeyote anayekuwa na mpenzi zaidi ya mmoja , iwe mwanaume au mwanamke, hawezi kuwapenda wote kwa usawa.

Kuna mmoja atapendwa zaidi kiasi kwamba wengine watahisi kabisa kuwa kuna namna. Na hapo ndipo utakuta yule ambaye anaona hatendewi usawa kwenye penzi, anaanza kutafuta njia mbalimbali za heri na shari ili kuhakikisha penzi linaelemea upande wake, hata kama kwa kulazimisha.

Mtunzi wa filamu ya 'Diana', ameliangalia hili na kutengeneza kitu ili kutoa elimu kwa jamii.

Picha hiyo imechezwa na wasanii mbalimbali mastaa kama Single Mtambalike "Richie', Sabrina Rupia 'Cathy', Halina Yahaya 'Davina' na wengineo.

Inaanza kuonyesha Richie akiishi kwa amani na upendo na familia yake, akiwa na mke na watoto wake wawili.

Hata hivyo, anaanza kuingiwa na shetani na kuanza kumpenda sekretari wake Davina.

Richie ambaye ni bosi kwenye kampuni, anatumia cheo chake kumnasa mrembo huyo.

Davina anakuwa 'nyumba ndogo' na siku zote penzi halina siri na siri si ya watu wawili, baadhi ya wafanyakazi wanaanza kuelewa mchezo mzima.

Siri inavuja na mke wa Richie anaipata, anavamia ofisini na kupelekwa kinyemela sehemu ambayo wapenzi hao wanapata chakula cha mchana.

Mke anatembeza mkong'oto kwa mwizi wake na kumchania nguo, huku akimchimba mkwara mzito wa kutishiwa maisha.

Kitendo hicho kinamuumiza mno Davina ambaye anaamua kutishia nyau, kuua uhusiano.

Richie alitumia msemo wa palipo udhia penyeza rupia, anambembeleza kwa maneno, mavazi na pesa, penzi likarejea upya.

Mapenzi yao kila yalivyozidi kushamiri, ndivyo walivyozidi kuiumiza familia. Mke wa watoto wa Richie hali ikawa mbaya kwani walikosa chakula na ada ya shule.

Siku zote muonja asali huchonga mzinga, Davina alichoshwa na tabia ya kutukanwa mara kwa mara na mke wa bosi wake, hivyo akataka aue ndege wawili kwa jiwe moja. Amkomoe Cathy, lakini pia ammiliki moja kwa moja Richie.

Akaenda kwa mganga kumroga mke wa bosi wake na kweli, Cathy akapata ugonjwa wa kupooza.

Kunatokea upotevu wa pesa za kampuni na kusababisha Richie afukuzwe kazi. Ugonjwa wa mkewe na kuyumba kiuchumi vikamchanganya na kusababisha atake kujiua.

Hata hivyo rafiki yake anamshauri asifanye hivyo, badala yake akampeleka kwa mganga ili kuangalia kama kuna mikosi iondolewe.

Huko anakutana na mpenzi wake Davina ambaye anakimbia alipomuoa.

Mganga anamwambia msichana aliyekimbia alikuwa akija kuchukua dawa ya kuroga kwani anatembea na mume wa mtu.


Richie anamwambia kuwa mtu anayerogwa ni yeye na familia yake, kitu ambacho kinamshangaza mganga.

Hata hivyo, baada ya mazungumzo ya muda mfupi wanagundua kuwa wanafahamiana na walishawahi kusoma shule moja miaka ya nyuma.

Baada ya kuona hivyo, mganga anampa Richie dawa ya kumponyesha mkewe na kumuodolea mikosi ili arejeshwe kazini.

Anarejea nyumbani kwake na alipofika hapo, ghafla mkewe alirejea na nguvu, akasimama. Furaha ikarejea ndani ya familia kwani mke amepona. Richie akarejesha upendo kwenye familia na kuachana na Davina.

**Simu 0716 350534.**
**afungamwango@gmail.com**



# BURIANI PAU PEPE KALLE

MIAKA 20 baada ya kifo cha gwiji la muziki wa dansi na mmiliki wa bendi ya Empire Bakuba Kabasele Yampanya, al maarufu Pepe Kallé, mkewe, Pauline Lundokisi naye ameaga dunia.

Kwa mujibu wa vyanzo vilivyo karibu na malkia wa Pepee, alifariki baada ya kushambuliwa na maradhi kwa mwezi mzima bila kutibiwa kikamilifu.

Vyanzo vinaeleza kuwa alifariki akiwa nyumbani kwake mjini Bandalungwa.

"Licha ya kuomba msaada wa matibabu kupitia runinga ya Chaka Kongo, ombi lililofanywa na the Asbl -"Artiste en danger"; au wasanii wanaotishiwa kuangamia' hakukuwa na msaada." Anasema mmoja wa wadau wa bendi ya Empire Bakuba Pepe Kallé orchestra.

Pepe Kalle alifariki dunia Novemba 28, 1998 akimuacha mkewe Pauline Lundokisi, aliyezaliwa Machi 30, 1957, ambaye matanga yake yalifanyika Adoula mjini Bandalungwa.

Mama licha ya kufiwa mwaka 1999 hakutaka kuolewa akimuomboleza mumewe hadi dakika ya mwisho. Kifo cha Pépé Kallé, kilitokea ghafla na kuwaachia maswali kibao wapenzi wake.

"Siwezi kuolewa tena. Huu ni ujinga, nitamkasirisha mwanaume aliyenitangaza na kuniwezesha nifahamike kote duniani. Ninamheshimu ndani ya nje ya Congo niseme tena asante kwake, "anasema Pauline Lundokisi, wakati wa uhai wake.

Anatangaza msimamo kwenye kipindi cha runinga kuadhimisha miaka 20 ya kifo cha mumewe.

Mama Pauline, alikuwa na uhusiano mzuri na vigogo wa Empire Bakuba orchestra, pamoja na wanamuziki wengine wa Congo.

# Ramsey amfagilia mkewe



MCHEZA sinema nguli wa Nollywood pamoja na mtengeneza sinema Ramsey Nuoah, aibuka na kutamba kuwa hana kashfa tena , ndoa yake imesimama.

Akiwa na miaka 17 ya ndoa iliyofungwa tangu mwaka 2002, anajulikana kuwa kivutio cha wanawake , hivyo wengi kushangaa amedumuje kwenye ndoa.

Anasema katika mahoajiano ya runinga kuwa hana shida yuko vyema ndani ya ndoa licha ya kuwa na jina kubwa ndani ya Nollywood.

Anamfagilia sana mkewe akisema ni 'mtu spesho. Si wa kawaida, anaelewa mambo tofauti na wanawake wengine. Ndiyo maana nasema mcheza sinema mwanamke au mwanaume ni lazima apate mwenza anayeelewa kama wa kwake"

"Si penzi linalowaunganisha. Sahau kuhusu penzi linakufa. Kinachodumisha ndoa ni ushirika 'companionship."anasema.



## Beckham ndani ya Kiswahili

NYOTA wa Soka wa Uingereza David Beckham, anatisha kwani ni miongoni mwa watu wachache wanaozungumzia lugha zaidi ya tano kwa ufasaha.

Akizindua kampeni ya kupambana na malaria duniani, anahamasisha kwa kutumia lugha lukuki lakini pia anatamba na Kiswahili.

"Malaria isn't just any disease. It's the deadliest disease there's ever been,"Beckham anasema kwa Kiingereza , kwa Kiswahili ' Malaria si kwamba tu ni ugonjwa. Ni maradhi hatari kuliko yote ambayo yamewahi kutokea.."

Baada ya kutangaza ubaya kwa malaria kwa Kiinglish anazama kwenye lugha nyingine kadhaa akianza kushika kwa Kispanyola, Kiarabu, Kifaransa, Kihindi, Kichina au Mandarin, Kiswahili, Kinyarwanda na Kiyoruba kinachozungumzwa Nigeria.

Kwa Kiswahili Beckham anatangaza vita dhidi ya malaria akisema maneno haya: 'hivyo tunazindua kampeni ya sauti'.

## Waacheni Harry na Meghan

FAMILIA ya Kifalme ya Uingereza imewaomba watu wawaachie wenyewe mwanamfalme Prince Harry na mkewe, Meghan Markle, masuala yanayohusu ujio wa mtoto wao, ambaye Meghan anatarajia kujifungua wakati wowote.

"Wanachukulia suala hili kama jambo lao binafsi na wameamua kuwa ni suala linalowahusu kuamua na kupanga mipango ya mtoto wao wanayemtarajia."

"Familia ya Malikia na Wana wa Ufalme wa Uingereza wanatazamia kwa hamu kubwa na kwa furaha kushirikiana na Harry na Meghan kufurahia taarifa za kufurahisha za ujio wa mtoto wao."





## Nipsey azikwa

KITUO cha ruinga cha BET cha Marekani ndicho kilichorusha mubashara matangazo ya mazishi ya Rapa na mwanaharakati Nipsey Hussle. Kilianza na ibada ya mazishi na hatua za kumuaga mwanamuziki huyo mwenye asilia ya Eritrea barani Afrika.

Aliuawa mwishoni mwa mwezi uliopita akiwa anatoka kwenye stoo yake ya nguo iliyoko Los Angeles huko Marekani.

Kabla ya mazishi familia yake na marafiki wa rapa wa Marekani Nipsey Hussle, walimuaga kimya kimya na kutoa heshima zao za mwisho kabla ya mazishi yaliyofanyika Alhamisi..

Familia ya Nipsey na marafiki zake walimuomboleza katika shughuli ya kumuaga iliyofanywa na familia yake kabla ya kufikishwa kwenye kituo cha Staples Center, sehemu ambayo mwili wa gwiji wa muziki wa Pop duniani, Michael Jackson, uliagwa.

Jamaa wa karibu na marafiki wa damu wa Nipsey walijazana kwenye ukumbi wa kampuni ya Angelus Funeral Home, inayotoa huduma za mazishi , Jumatano mchana .

## Baby nitabaki na nani: Lauren

ALIYEKUWA mchumba wa Nipsey Hussle, Lauren London, alikuwa wa kwanza kutizamwa baada ya mshikaji wake kuuawa mwishoni mwa mwezi uliopita jijini Los Angeles huko Marekani.

Licha ya muuaji wake kufikishwa mahakamani na kukataa kuhusika na mauaji hayo, mrembo London muda wote alijitahidi kusimama imara na hakuwa tayari kutetereka.

Akiandika kwenye akaunti yake ya insta ameeleza haya:"Ni kama nimepotea jamani nimempoteza mpenzi wangu na mtu wa muhimu kwenye maisha yangu ...alikuwa rafiki wa kipekee, kimbilio, mlinzi, ooh roho yangu... nimekwisha na kupotea bila wewe .... Sina neno la kusema."





## Mionzi ya Sheria

Na John Juma
0716217615

# Watanzania wanahitaji kazi za Bunge na CAG

HIVI karibuni kumekuwa na suala linalojielekeza kwenye mamlaka na mipaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Hivyo Mionzi ya Sheria imeona ichangie kuhusu ofisi ya CAG ambayo ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ofisi ya CAG inaundwa kikatiba kupitia ibara za 143 na 144 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa mara kwa mara.

Ibara hizo kwa ufupi zinaeleza mambo yafuatayo kwa kuanza na ibara ya 143 inasema mosi kutakuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano. Aidha, CAG atakuwa na jukumu juu ya mambo yafuatayo:

Katiba inasema kuwa atahakikisha kwamba fedha zozote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali matumizi yake yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 136 ya katiba na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

Kadhalika katiba inasema mdhibiti atahakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria zilizotungwa na Bunge na ambazo zimetumika, ziwe zimetumiwa kwa ajili ya shughuli zilizolengwa au kutajwa wakati wa kuidhinishwa. Katiba inatamka kuwa CAG angalau mara moja kila mwaka afanye ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa serikali, za mahakama, bunge.

Pia, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu, kumbukumbu, hati nyinginezo zote zinazohusika na hesabu za aina yoyote iliyotajwa katika ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 143.

Aidha, atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) ya ibara 143 ya katiba. Baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza watu wanaohusika waiwasilishe kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kuipokea na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakuwa na jukumu la kutekeleza kazi na shughuli nyingine, madaraka mengine ya namna mbalimbali, kama itakavyoelezwa na sheria ya hesabu za serikali au za vyombo vya umma yakiwamo mashirika.

Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2), (3) na (4) ya ibara hii, mdhibiti huyo hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwingine yeyote au idara yoyote ya serikali, lakini maelezo hayo ya ibara hii ndogo hayataizuia mahakama kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya katiba.

UWAJIBIKAJI/KUWAJIBISHWA

Mdhibiti anawajibika kwa Rais kwa mujibu wa ibara ya 143. Bungeni huwasilisha taarifa ambayo imetoka kwa Rais. Aidha, mdhibiti halazimiki kufuata maagizo ya mtu yeyote kwa mujibu wa ibara ya 143 (6). Mahakama ina uwezo wa kuchunguza kama ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa katiba. Kuhusu kuondoka kazini katiba inasema mdhibiti ataondoka kazini kwa kustaafu, kuugua, kwa sababu ya tabia mbaya, au kwa kuvunja masharti ya sheria ya maadili ya viongozi wa umma kwa mujibu wa ibara ya 144

Kuondolewa kazini kwa mdhibiti ni mchakato mrefu unaoanza na Rais kuteua tume maalum ambayo itakuwa na mwenyekiti na wajumbe wengine wasiopungua wawili. Ibara ya 144 (3) inaelekeza.

Kimsingi ripoti ya CAG ni muhimu sana katika kufanikisha uhalifu, wizi, matumizi mabaya ya fedha za serikali, taifa hili limejipambanua kupigana vita ya uchumi na kuleta maendeleo kwa mujibu wa ibara ya 9 (c), (h), (i), (j) na (k); pia 11 (1)].

Kwa njia moja au nyingine inatoa picha kamili, ni jinsi gani fedha za umma au za walipakodi zinatumika, na jinsi gani Bunge linatekeleza wajibu wake katika kuisimamia serikali kwenye kuijadili na kuipitisha bajeti.

Ni muhimu kutilia mkazo zaidi suala la kusimamia na kufuatilia matumizi ya fedha za umma, hivyo ofisi ya CAG yenyewe haitaweza kuyabana mashirika, wakala, mamlaka za udhibiti, serikali kuu na zile za mitaa hivyo linahitajika bunge na wadau wengi kutekeleza jukumu hilo.

Kisha basi, mtakubaliana na mwandishi wa makala hii kutoa shukrani za kipekee kwa Rais mstaafu Jakaya Kikwete, kwa kuanzisha utaratibu huu unaotoa fursa ya ripoti husika kusomwa na kujadiliwa bungeni ili kuongeza ushirikishwaji na ukomavu wa demokrasia na kujiletea maendeleo.



## Kalamu ya Mwalimu

Reubeni Lumbagala

# Mabaraza mitihani EAC yaanze kutibu mitaala

KATIKA jitihada za kudumisha mtangamano baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwenye sekta ya elimu, mabaraza na bodi za mitihani za nchi wanachama zimeunganisha nguvu.

Zimekuja pamoja na kuazimia kwa sauti moja kuviunganisha vyombo hivyo ili kupeana ujuzi, maarifa na uzoefu wa masuala ya elimu na hatimaye kuchagiza mafanikio yanayopatikana kupitia elimu ili kufikia maendeleo endelevu.

Wakati wa mchakato huo wa muungano wa mabaraza na bodi za mitihani ya Afrika Mashariki, Dk. Charles Msonde ambaye ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (Necta) anateuliwa kuwa Rais wa umoja huo.

Tangu mwanzo nia ya kuinua elimu ni moja ya malengo yaliyokuwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu mwaka 1967 ilipoanzishwa kwa mara ya kwanza.

Hivyo, muungano wa mabaraza na bodi za mitihani za jumuiya hiyo ni kielelezo cha kusimamia na kutekeleza lengo la kuinua sekta ya elimu miongoni mwa nchi wanachama.

Moja ya njia ya kuinua sekta hiyo ili kuleta tija kwa wanufaika ni kuandaa mitaala inayoendana na wakati ili kumuwezesha mwanafunzi kujimudu ili kujitegemea baada ya kuhitimu.

Kwa lugha nyepesi mitaala ni yale yote mwanafunzi anayopewa kujifunza shuleni au vyuoni, ambayo yameandaliwa na wataalam wabobezi wa elimu waliopewa jukumu la kutayarisha mada zinazotolewa kwenye ujifunzaji na ufundishaji darasani.

Umoja huu wa mabaraza ya mitihani una wajibu wa kutoa mapendekezo bora yenye kuleta mapinduzi katika sekta ya elimu kwa kuhakikisha kuwa mitaala inayotumika katika nchi wanachama inakuwa bora yenye kuwasaidia wahitimu kukabiliana na kumudu maisha ya kumaliza masomo.

Kila nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inaweza kuwa na mitaala yake katika ngazi za shule za msingi, sekondari hadi vyuo vikuu lakini kukawa na makubaliano ya pamoja ambayo kila mwanachama itayajumuisha katika mitaala yake ili kuleta tija kwa wahitimu.

Maofisa waliopo katika umoja huu wahakikishe wanatumia kikamilifu utaalamu wao kuboresha elimu yetu ili vijana wa jumuiya hiyo wawe na uwezo wa kushindana na wenzao wengine kutoka nchi za kanda nyingine za Afrika na mabara mengine duniani.

Machi 24, 2018, katika mkutano wa nne wa mwaka wa Chama cha Waajiri Afrika Mashariki (EAEO) ilielezwa kuwa nusu ya wahitimu wa vyuo vikuu katika nchi za Afrika Mashariki wanakosa sifa na ujuzi wa kuajirika.

Katibu Mkuu wa EAEO, Dk Aggrey Mlimuka, anawaambia washiriki kuwa utafiti unaonyesha kuwa vyuo vikuu na vyuo vya kati katika nchi za Afrika Mashariki vinatoa elimu ambayo inawafanya vijana washindwe kuajirika.

Anaendelea kusisitiza kuwa ni lazima kuwapo na mahusiano baina ya mitaala ya masomo na mahitaji katika soko la ajira iwe ndani ya nchi, jumuiya na duniani pia.

Ni dhahiri upo umuhimu wa kuhuisha mitaala ili iendane na mahitaji ya soko la ajira. Lakini pia, mitaala isisitize zaidi elimu ya vitendo kuliko nadharia madarasani.

Hii inatokana na ukweli kuwa si wahitimu wote watakaopata nafasi ya kuajiriwa katika taasisi mbalimbali za serikali na za watu binafsi, wengine ambao ndiyo wengi zaidi watapaswa kujiajiri wenyewe.

Kama mitaala ya elimu katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki itakazia elimu ya vitendo zaidi kuliko nadharia, wahitimu wake watakuwa katika nafasi kubwa ya kunufaika na matunda ya elimu waliyoipata kwani wataweza kujitegemea kwa kuajiriwa au kujiajiri wenyewe.

Eneo jingine ambalo mabaraza na bodi za mitihani ya Afrika Mashariki yamekubaliana kushirikiana kwa karibu ni kuzuia udanganyifu wa kipindi cha mtihani ya taifa.

Mkazo huu unawekwa na Dao Odongo ambaye ni katibu wa umoja huo kutoka nchini Uganda. Wizi wa mitihani ni tatizo kubwa linalokabili sekta ya elimu katika nchi nyingi za Afrika, hivyo, mikakati ya kutokomeza kadhia ya uvujaji wa mitihani inapaswa kuwekwa ili elimu yetu izidi kusonga mbele.

Umoja huu usaidie kupeana mbinu za kukabiliana na wizi wa mitihani kutokana na kubadilishana uzoefu na ujuzi kutoka kwa maofisa hao wa nchi mwanachama.

Kwa kumaliza tatizo la uvujaji wa mitihani, wahitimu watakaopatikana watakuwa bora wenye uwezo wa kuleta tija katika jamii na taifa kupitia maarifa, ujuzi na stadi walizozipata shuleni na vyuoni.

Jukwaa hili lililoanzishwa linategemewa kuleta chachu ya maendeleo ya elimu katika ukanda wa Afrika Mashariki kwa kuhakikisha wananchi wanapata elimu bora kupitia mawazo yanayotolewa na maofisa wa mabaraza na bodi za mitihani ya Afrika Mashariki.

Ni jambo jema kwa EAC kuviunganisha vyombo hivi vya elimu ambavyo vitaleta tija kwa wanajumuiya katika nyanja zote kutokana na elimu kuwa suala mtambuka.


Reubeni Lumbagala ni Mwalimu kwa taaluma kutoka Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

**Maoni: (+255) 764 666349.**










# Matapeli mitandaoni wanavyowachuna wazazi

**Na Gaudensia Mngumi**

MATAPELI wa mitandaoni wameendelea kutunga mbinu za kufanikisha udanganyifu ili kujipatia fedha kutoka kwa watu mbalimbali, sasa wakiwalenga wazazi na walezi wa wanafunzi walioko shuleni.

Hivi karibuni wamebainika kutuma taarifa kwa baadhi ya wazazi au walezi huku wakijitambulisha kwa majina ya walimu wa shule , wakiwajulisha kuwa watoto wao wameumwa ghafla, hivyo watume fedha za matibabu ili kuokoa maisha yao.

"Ukipata ujumbe huo unachanganyikiwa unaweza hata kupata presha na kuanguka chini kutokana na hofu na mstuko mkubwa unaokupata" anasema mama wa binti wa kidato cha kwanza anayesoma katika shule moja jijini Dar es Salaam.

Akieleza kisa chake mama huyo (jina tunalo) mwenye namba ya simu 0655-602002 anasema alipokea ujumbe kutoka kwa mwanae wa kiume, aliyemaliza kidato cha nne mwaka jana kwenye shule moja (jina tunalo), ukimfahamisha kuwa mwanaye mwingine anayesoma katika shule hiyo , amekimbizwa hospitalini tena yuko hoi.

"Kijana alirusha meseji akisema mama dada anaumwa mpigie mwalimu simu ufuatilie . Nilipoiona nikampigia mwalimu Simon Mphubusa aliyetuma meseji kuwa mtoto anaumwa," anasema.

Mama huyo anaeleza kuwa shuleni anakosoma mwanaye kuna mwalimu anayeitwa Simon, hivyo akaamini na kumpigia simu mara moja.

### UJUMBE

Anaeleza kuwa simu iliyopokelewa na tapeli aliyekiri kutuma ujumbe huo na kumweleza kwamba binti yake alianguka ghafla ndani ya chumba mitihani na sasa amekimbizwa hospitalini.

Anasema mwalimu huyo feki alidai alikimbizwa hospitalini kwa sababu alizimia na kabla ya vipimo ametundikiwa drip kwani ana upungufu mkubwa wa maji.

Baada ya kupimwa amekutwa na malaria, homa ya matumbo (taifodi) na ukosefu wa maji mwilini na amelazwa kwenye zahanati ya Upendo Mikocheni hivyo atume Sh 58,500 mara moja kulipia vipimo vya awali, anaongeza mama huyo.

Hata hivyo, alimwambia anaweza kufika shuleni akaelekezwe zaidi, anasema mama huyo. Aliamua kwenda shuleni na kuwasiliana na uongozi uliomjulisha kuwa binti yake yuko salama na kwamba hawahusiki na taarifa hizo.

"Nilimpigia tapeli simu kumwarifu kuwa nimeshafika shuleni kwa mtoto anayeumwa. Akabadili kauli kutoka shule aliyoitaja mwanzo akasingizia nyingine. Mwanangu yuko shule iliyoko Mikocheni, lakini ananibadilishia kibao akisema aliniambia niende Tegeta,.." anasema yote hayo aligundua kuwa ni mbinu zao.

### MZAZI MWINGINE

Mzazi mwingine ambaye mtoto wake anasoma shule ya bweni, alipigiwa simu kuwa mwanaye ameanguka ghafla na sasa wako hospitalini, taarifa zikitumwa na mwalimu Idd mwenye namba 0712-718736.

Alipopiga simu kuuliza zaidi alimuuliza kuwa mtoto anaumwa nini, tapeli huyo alimwambia kuwa hana maji, ana taifodi, malaria naye pia ameongezewa maji hivyo atume Sh. 59,000 mara moja.

"Nilimwambia hapana mwanangu asitibiwe kwenye hospitali ambazo sizijui apelekwe hospitali (jina tunalo) kwani wana bima na wanatibiwa huko. Siwatumii pesa ili mkifika kwenye hospitali ninayowaelekeza mtanikuta niwarudishie gharama za teksi." Anasema.

Mama huyo ambaye binti yake anasoma darasa la saba kwenye shule ya bweni, alijibiwa kuwa hawezi kuondolewa hospitalini bila kupata drip za maji kwanza kwani ana hali mbaya mno.

Anasema baada ya kuwasiliana na jamaa zake wengine kuhusu tatizo hilo, walimfahamisha kuwa huo ni utapeli ulioibuka siku hizi hivyo aachane nao.

### KUITWA SHULENI

Baba mzazi wa mwanafunzi anayesoma mkoani Tabora ni miongoni mwa watu waliotapeliwa na kuzungumza na gazeti hili.

Anasema alitumiwa ujumbe wa kuitwa shuleni kwa kuwa mwanawe ni mgonjwa na amekimbizwa hospitalini kwani hajitambui.

Mzazi huyo aliyetumiwa meseji kutoka kwa mwalimu Boniface Minja mwenye namba 0657-753672, aliujibu ujumbe wa mtoa taarifa akihoji ni mtoto yupi na anasoma shule gani kwani anao watoto wengi. Mbinu hiyo ilimkwamisha tapeli kwani alishindwa kutoa majibu, kwa mujibu wa maelezo ya mzazi huyo.

Anasema, hata hivyo alijaribu kuwasiliana na jamaa zake waliko karibu na watoto huko Tabora lakini nao simu zikawa hazipatikani hali iliyompa hofu zaidi.

"Nilichanganyikiwa. Lakini baada ya muda ndugu hao walinipigia simu wakiniambia kuwa walikuwa kanisani na kuniarifu kuwa hakukuwa na tatizo." Anasema baba huyo, anapozungumza na Nipashe.

### MAONI YA JUMLA

Wazazi hao wanaona kuwa taarifa hizo zinastua na kusababisha kuchanganyikiwa, kupata presha na wakati mwingine mzazi anaweza kupata tatizo kubwa la kiafya linalotokana na wasiwasi.

Wazazi hao wanaona kuwa hiyo ni njia mojawapo ya kutapeli fedha ambayo kama haitadhibitiwa itaumiza wazazi na walezi au jamaa wasio jua kuhusu wizi huo na wanaoamini kila kitu wanachoambiwa kupitia simu.

### MAMLAKA YA MAWASILIANO

Mwongozo kwa Watumiaji wa Huduma na Bidhaa za Mawasiliano, uliotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), unaodhibiti ubora na ufanisi wa mawasiliano ya kilektroniki, uliotolewa mwaka 2017, unawaelekeza wateja wa simu kuachana na kutapeliwa.

Kwanza unawakumbusha kutoweka viwango vikubwa vya fedha katika simu zao na kuwataka kuhifadhi fedha nyingi benki ili kuepusha kuibiwa na matapeli hao. Mwongozo huo ambao pengine watu wengi hawaufahamu unaelekeza wateja wa simu kuwa wanapopigiwa simu au kupokea ujumbe mfupi unaotaka watume pesa , hata kama anayetaka muamala wanamfahamu wahakikishe kwanza kama ndiye kwani matapeli wanaweza kutumia simu yake.

Kitabu hicho kinatahadharisha watu wasikubali kushinikizwa na maelekezo ya meseji hizo kwa kuwa matapeli wana njia nyingi za kulaghai na mbinu mojawapo ya kujihakikishia ni kumpigia simu aliyetaka hizo fedha ili atoe maelekezo ya kujiridhisha.

Akizungumza katika mkutano mkuu wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), wiki iliyopita, Ofisa wa TCRA Mabel Masasi, anasema unapotumiwa ujumbe au kupigiwa simu kuarifiwa kuingia kwenye 'madili' makubwa yenye majina maarufu , au taarifa za kushinda bahati nasibu usizoshiriki kuwa makini usianze kutanguliza malipo.

Anakumbusha kuwa kupata fedha hakufanikiwi kwa njia za kupiga madili au kushinda bahati nasibu usizocheza.

"Kumbukeni mafanikio yanapatikana kwa kufanyakazi halali kwa bidii na maarifa na si kwa njia za mkato kama hizo za kutumiwa meseji," anasema Masasi akinukuu mwongozo huo.

Akizungumzia kutumiwa pesa na mtumiaji mwingine anayekutaka umrudishie kwani amekosea namba ya aliyekuwa apokee, Masasi anawashauri watumiaji kuwaambia waliokosea kutuma mwamala huo, kuwasiliana na watoa huduma ili warejeshe fedha kwa utaratibu wa kimtandao.

### KUTUMIA POLISI

Masasi anawaambia wana Tamwa kuwa ni vyema kutoa taarifa polisi unapotumiwa ujumbe wa kutaka fedha au taarifa unazozitilia mashaka.

Anasema kazi za TCRA ni kutoa elimu kwa watumiaji wa simu za mikononi na kuwataka wateja kutafuta taarifa na kujielimisha zaidi ili kujiepusha na matapeli wa mitandao ya simu.

MAKALA



# Bajaji zinapogeuka kumbi za disko zinazotembea mitaani

Na Beatrice Moses

MIAKA ya nyuma kusikia muziki wenye sauti ya juu na mdundo mzito, yalikuwa mambo ya baa au kumbi za starehe. Lakini sasa mambo yamebadilika. Karibu kila mahali kelele za 'muziki mnene' unaoumiza ngoma za masikio unaotikisa anga.

Muziki huo mbali na kutoka kwenye magari, unasikika zaidi kwenye bajaji na hata bodaboda ambao ni usafiri wa haraka unaotegemewa na wakazi wengi wa mijini mathalani, Dar es Salaam hasa kule ambako daladala hazifiki.

Madereva wa vyombo hivyo wengi ni vijana, hivyo wana mambo mengi kuanzia mavazi, kupenda starehe na burudani hasa muziki unaofunguliwa kwa sauti ya juu na wenye mdundo mkubwa.

Tofauti na magari madogo na bodaboda bajaji zimetia fora kuwa usafiri wenye kelele za muziki wa kishindo kikubwa kupindukia.

Madereva wake wamefunga spika za kisasa zinazotoa sauti za kubwa na za kishindo na mitetemo maarufu kama 'subwoofer' ambazo zikifunguliwa husababisha bajaji kutikisika kwa kishindo cha muziki .Ninachoweza kusema ni kwamba pengine madereva wengi hawajui kwamba pamoja na kuwa vyombo hivyo ni ofisi zao binafsi, wanapaswa kuwahudumia wateja vyema badala ya kuwasababishia kero.

Miongoni mwa madereva hao wengine ni wamiliki wa vyombo hivyo, walivyonunua kwa mkopo au kwa fedha taslim, au ni mali ya familia zao na huenda hali hiyo inawapa kiburi baadhi yao, kwani hata wakionywa na abiria hawawasikilizi. Msemo wa mteja ni mfalme wameshindwa kutafakari wanapowahudumia abiria wao.

**SHERIA ZINASEMAJE?**

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2014 pamoja na mambo mengine inakataza upigaji muziki unaosababisha kelele, au kuwa na ibada au ngoma za kukesha za pamoja na kufanya sherehe mtaani, vinginevyo inapaswa kulipia Sh.milioni 10.

Kanuni za sheria hizo zilizoanza kutumika rasmi mwaka 2015, zilileta mtikisiko ulioripotiwa kwenye vyombo vya habari kwa watu binafsi na taasisi kadhaa kukamatwa kutokana na kelele.

Hata hivyo, hali ilivyo leo ni kama vile watu wengi wamejisahau kwa kuwa kelele kwenye mitaa ni nyingi. Si watu pekee hata magari ya matangazo na 'promotion' za bidhaa mbalimbali ambayo huzunguka mitaani na vipaza sauti na muziki wenye kelele ni jambo ambalo sasa linaelekea kukubalika bila kujali kuwa ni uvunjaji sheria.

Licha ya sheria kuwataka watu kuheshimu kanuni za viwango vya kelele na mitetemo katika maeneo mbalimbali bado baadhi ya watu wameendelea kufanya ukaidi hivyo kusababisha kero kwa jamii.

Ikumbukwe sheria hiyo inaelekeza kuwa hata unaposikiliza redio nyumbani unaelekezwa kuwa sauti iwe inasikika ndani ya chumba isitoke nje kukera majirani.



Utafiti uliofanywa na Nipashe kwenye baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam, umebaini kuwa madereva wa bajaji na pikipiki ndiyo wanaoongoza kwa kero hiyo ya kelele.

Wanaongeza kelele wakikatiza kwenye maeneo wanapopeleka abiria au kurejea kwenye vijiwe vya maegesho wanawasha radio zinazotoa sauti kubwa na mitetemo.

Hayo yote yanaweza kukomeshwa iwapo Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) litatekeleza wajibu wake kwa kusimamia ipasavyo sheria zinazohusika.

**KUSHTAKIWA**

Kwa upande mwingine Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (Sumatra Consumer Consultative Council) ndilo lenye jukumu la kuunganisha watumiaji (wateja) wa huduma zinazothibitiwa na Sumatra, watoa huduma na serikali.

Pia jukumu jingine la baraza hilo ni kuhakikisha kuwa maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri wa nchi kavu na majini yanawasilishwa katika uundaji wa sera inayohusu usafiri huo.

Baraza hilo lililoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2001, wadau wake ni pamoja na abiria wa daladala wa mabasi ya mikoani na treni.

Wengine ni abiria wa meli, vivuko, boti, mashua, mitumbwi, pikipiki, bajaji pamoja na watembea kwa miguu barabarani.

Pamoja na mambo mengine yanayoahinishwa na baraza hilo ni kuwa mtumiaji ana haki ya kusafiri na kutumia huduma au bidhaa za usafiri katika mazingira yaliyo salama.

Linaeleza kuwa pia mtumiaji wa usafiri ana haki ya kutosumbuliwa awapo safarini. "Ni wajibu wa mmiliki wa chombo cha usafiri na mtoa huduma ya usafiri na mamlaka zinazosimamia sekta ya usafirishaji kuhakikisha mabasi, treni, boti na meli vinaendeshwa vikiwa katika hali salama," inaelezwa na baraza hilo katika kitabu chake cha mwongozo.

Kanuni ya 18 (1) (a) (g) (h) inatoa haki kwa abiria kutonyanyaswa kwa matusi au vitendo vyovyote kinyume na taratibu au kwa mujibu wa haki za binadamu iwe kwa abiria mtu mzima au mdogo.

"Ikitokea abiria akanyanyaswa na mfanya kazi ndani ya chombo alichosafiria, anao wajibu wa kulalamika kwa kuandika barua kwa mmiliki au menejimenti ya kampuni husika kudai fidia kwa hasara aliyoipata na/au kuomba watumishi wachukuliwe hatua stahiki,"inaelezwa.

Baraza hilo linataja pia wajibu wa mtumiaji ikiwa ni pamoja na kuwasilisha maoni na kero, kwamba anao wajibu wa kutoa maoni yake kwenye chombo hicho kingine chochote kinachodhibiti huduma za usafiri.

Kutokana na maelezo hayo ni wazi abiria wanapaswa kuwashtaki madereva wanaofungulia radio au muziki kwa sauti kubwa, hatua ambayo kwa namna nyingine inaweza kuhatarisha maisha, hasa kwa abiria wenye magonjwa.

Lakini inaweza kuwa hatari kwa maisha kwa sababu dereva hawezi kusikia honi iwapo kuna hatari nyuma au pembeni yake. Hivyo, Baraza la Sumatra nalo litimize wajibu wake kwa kuhakikisha inaendelea kutoa elimu au kuwashughulikia wale wote wanaoonyesha ukaidi wa kufungulia miziki kwa sauti kubwa.

# 'KISU CHA NGARIBA KILINIPA ARI, USHUJAA NA USHINDI'

**Na Mary Geofrey**

MACHOZI na uchungu wa kukeketwa, kupoteza damu nyingi na hatimaye kuzimia kwa zaidi ya saa tano, kulichochea ari na kuamsha nguvu mpya ya kuwapigania mabinti wanaokataa kukeketwa lakini hawana wa kusaidia."

Ni ushuhuda wa Robi Samwel, aliyepitia machungu ya kukeketwa na kuonja madhara yake, lakini leo amegeuka kuwa shujaa wa kuwalinda wasichana wanaopinga na kuzuia kuendeleza mila hiyo inayoelezea na wadau wa afya kuwa ni potofu.

Robi anasema alikeketwa kwa sababu hakuwa na mahali pa kukimbilia wala mtu wa kumsaidia wakati huo ili kuepuka kisu cha ngariba, baada ya kuondoka nyumbani ili kukwepa mila hiyo inayoumiza.

"Damu yangu iliyomwagika baada ya kukeketwa ilikuwa silaha ya kuinuka na kuanzisha mapambano ya kuwaokoa na kuwachomoa wasichana kwenye mikono ya mangariba kabla ya kukeketwa," anasema Robi.

Hakika kazi yake ni ya kutukuka, ndiyo maana anatambulika na kuheshimika tena, anachukua Tuzo ya Heshima inayoandaliwa Clouds Media Group, kwenye tukio la utoaji wa Tuzo ya Malkia wa Nguvu, jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

Anaibuka malkia wa nguvu, baada ya kuwasaidia wasichana zaidi ya 100 waliokuwa waumie mikononi mwa mangariba.

Robi ni mama ambaye amejitolea kulea watoto hao ambao wanazikimbia familia zao kuepuka kufanyiwa ukeketaji hukoMusoma mkoani Mara.

Shujaa huyo anasema anawalea wasichana wanaosoma Shule ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Ufundi katika kituo chake cha Hope kilichopo wilayani humo.

**KILICHOMFIKA**

"Nikiwa binti mdogo wazazi wangu walitaka kunikeketa. Nilikataa kwa sababu nilikuwa sipendi kitendo hicho walichofanyiwa wasichana wenzangu walionitangulia," anasimulia Robi.

Hivyo, anasema, alifanya jitihada za kukimbia kutoka mikononi mwa wazazi wake na kwenda kwa shangazi yake kuomba msaada, lakini hata hivyo hakumsaidia.

"Shangazi badala ya kunisaidia alianza kufanya sherehe kufurahia ujio wangu. Kwake ujio wangu ni kama mnyama amejinasa mtegoni. Nililia sana kwa sababu sikujua nitapata wapi msaada," anasema Robi.



Vick Mtetema (kushoto) na wadau wengine katika harakati zake za kila siku. **PICHA :MTANDAO.**

Akizungumza zaidi kilichomfika anasema baada ya muda alipelekwa kukeketwa aliumia baada ya kupoteza damu nyingi na kusababisha kuzimia kwa zaidi ya saa tano.

"Nilipozinduka nilidhamiria moyoni kuwa nitasimama kidete kuwatetea na kuwasaidia watoto wa kike wanaokabiliwa na kukeketwa lakini hawana mahali pa kukimbilia,"anajiambia.

**ANACHOKIFANYA**

Baada ya Robi kuwa mtu mzima alianzisha kituo cha kulea watoto wa kike ambao familia zao zilitaka kuwakeketa. Anawapata mabinti hawa kupitia ofisi za serikali za mtaa na wengine wanafika nyumbani au ofisini kwake.

Robi anasema tuzo aliyopewa itakuwa na manufaa kwa mabinti na wasichana wanaopinga na kukataa matukio hayo ya ukatili wa kijinsia.

Kuhusu utekelezaji wa majukumu yake anasema, anapita kwa jamii kutoa elimu kwa mangariba wanaokeketa watoto wa kike.

"Tumetoa elimu kwa jamii kuhusu matukio haya ya ukeketaji na tayari tumewasaidia mangariba kuacha kazi ya ukeketaji," anasema.

Katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Robi, Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, anaahidi kumpatia gari kwa ajili ya kubeba wanafunzi wakati wa kwenda na kurudi nyumbani.

Makonda anasema watoto hao wa kike ambao wametokea kwenye changamoto ya kutaka kukeketwa atawapatia gari hilo ili kuwaondolea usumbufu.

"Mchango wangu kwako utakuwa ni gari la kubeba watoto hawa wa kike kwenda shule, nitalikabidhi katika Siku Kuu ya Wafanyakazi Mei Mosi mwaka huu," anaahidi Makonda.

**TUZO YA AFYA**

Kazi ya kuwaokoa watu wenye ulemavu ni jukumu ambalo halitasahaulika. Vick Ntetema ni malkia wa nguvu anayechukua Tuzo ya Afya.

Vick Ntetema ambaye alisimama kidete kuhakikisha anatumia kalamu yake kuripoti watu waliokuwa wakihusika na mauaji ya watu wenye ualbino nchini.

Ntetema ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Under the Same Sun nchini, mwaka 2015 alipewa tuzo ya Mwanamke Jasiri wa Kimataifa na serikali ya Marekani kwa kazi hiyo kubwa ya kufichukua ukatili uliokuwa ukifanywa na waganga wa kienyeji.

Mwanahabari huyo nguli, anapewa tuzo ya afya kwa sababu ni mwanamke wa kwanza kuthubutu kuwaripoti wauaji wa watu wenye ualbino na kufikia hatua ya kuhatarisha maisha yake.

Akizungumzia tuzo hiyo, Ntetema anasema aliweza kuthubutu kuanza kuripoti habari za kuwafichua wahusika wa mauaji ya watu wenye ualbino baada ya kupata msaada na ushauri kutoka kwa mama yake mzazi.

"Namshukuru mama yangu mzazi ambaye alikuwa mstari wa mbele kunitia moyo na kunieleza kama waganga ndiyo wanaohusika kuua watu wenye ualbino hata kama watakuua na wewe utakuwa umekamilisha jukumu lako la kusaidia jamii," anaeleza Ntetema.

Anaeleza kuwa, kwa sababu mama yake alikuwa nyuma yake alipata nguvu ya kufanya kazi hiyo kwa moyo na kufanikiwa kuripoti watuhumiwa wa mauaji hayo.

Anasema kutokana na changamoto ya usumbufu aliopata alilazimika kwenda kujificha nchi nyingi kulinda usalama wake.

"Tuzo hii ni kwa ajili ya wanahabari wote ambao wapo mstari wa mbele kuripoti matukio ya kikatili wanayofanyiwa Watanzania wenzetu, inaenda kwa watu wenye ualbino, taasisi ya Under the Same Sun na Shirika la Utangazaji la Uengereza (BBC) ambalo lilinisimamia kufanya kazi hii kikamilifu," anasema

**'MSIKATE TAMAA'**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya kutengeneza samani za ndani na maofisini ya Amorette, Jacqueline Mengi, anawataka wanawake kuiga mfano wa waliochukua tuzo hizo tena wasikubali kukata tamaa.

Jacqueline ambaye alikabidhi tuzo ya Sayansi na Teknolojia kwa Mahinda Waziri na Sophia Abeil, aliwataka wanawake kuendelea kujituma na kujiamini.

Kwa upande wa tuzo ya malkia anayetoa hamasa, ilichukuliwa na Faraja Kota, kupitia mradi wake wa Shule Direct unaosambaza vitabu shuleni.

Tuzo ya kilimo na biashara ilikwenda kwa mfanyabiashara na mfugaji wa vifaranga, Elizabeth Swai, anayetotolesha vifaranga vya kuku 8,000 kwa siku.

**WANAWAKE WATHAMINIWE**

Mgeni rasmi katika utoaji wa tuzo hizo zinazotolewa na Clouds kwa mwaka wa nne sasa, Rais Mstaafu wa Bunge la Afrika, Balozi Getrude Mongela, anasema wanawake waliopewa tuzo ni sehemu ya kuongeza chachu kwa wengine wanaofanya mambo makubwa ndani ya jamii.

Kadhalika anasema katika kuendeleza juhudi za wanawake nchini, Watanzania wanapaswa kuwachagua viongozi watakaotoa ajenda zinazowatambua na kuwathamini wanawake ifikapo mwaka 2020.

Mongela anasema mataifa mengi duniani yamesonga mbele bila nguvu ya wanawake lakini kwa Tanzania haiwezekani kwa sababu wanawake ndiyo washika uchumi na nguvu ya uzalishaji.

"Uchaguzi unakuja, ajenda zinazotolewa na wagombea lazima zitambue thamani na nafasi ya mwanamke ndani ya jamii. Kama mgombea ataona wanawake kama vitendea kazi huyu hatufai na hana sababu ya kuchaguliwa kwa sababu asilimia kubwa wanawake ndio wazalishaji wa uchumi wa taifa hili hivyo wanapaswa kutambuliwa," anasema Mongela.

Adha, anawasihi wanawake waliopewa tuzo za Malkia wa Nguvu, kuwa chachu ya kuwainua na kuwandaa wengine wengi 10 kila mmoja katika kipengele cha tuzo yake.

Mongela pia anawapongeza Clouds Media Group kwa kuandaa tuzo hizo zinazoenda sambamba na kumbukizi miaka 20 ya kuanzishwa kwake na kuifananisha na umri wa mtu wa miaka 20 wa kufanya mambo makubwa katika nchi.

"Umri wa Clouds ni sawa na umri wa mtu ambaye ameishi duniani lakini hakuna alichofanya kinachoweza kuacha alama lakini nyie mmefanya mambo makubwa yanayopaswa kuungwa mkono na kila mmoja," alisema Mongela.

Kwa upande wake, meneja wa Vipindi na Maudhui wa Clouds Media, Sebastian Maganga, anasema tuzo za malkia wa nguvu zimetolewa kwa wanawake 20 kuashiria miaka 20 ya kuazishwa kwa kituo hicho cha Luninga na redio.

Anasema wanatoa tuzo hizo kutambua mchango wa wanawake ambao wanafanya mambo yenye matokeo chanya ndani ya jamii

# Baraza la kijeshi Sudan kujadili makundi kisiasa

**KHARTOUM, Sudan**

MAELFU ya waandamanaji nchini Sudan wameweka kambi nje ya Wizara ya Ulinzi mjini Khartoum kushinikiza iundwe serikali ya kiraia.

Aidha, wamekaidi amri iliyotolewa na baraza la mpito la kijeshi ya kutotoka nje usiku.

Waandamanaji hao ambao wamekuwa wakiandamana karibu kila siku kuipinga serikali ya rais aliyeondolewa Omar al-Bashir, ambaye ameitawala Sudan kwa miaka 30.

Wameukataa uamuzi wa kuanzishwa kwa baraza la mpito la kijeshi ambalo limetangaza kuitawala nchi hiyo kwa miaka miwili na kuahidi kuendelea na maandamano hadi serikali ya kiraia itakapowekwa.

Wanaharakati wamewasihi wananchi kujitokeza kwa wingi katika sala ya Ijumaa nje ya wizara hiyo, eneo kuu ambako maandamano yamekuwa yakifanyika.

Mahema makubwa yamewekwa katika eneo hilo na watu wameleta vyakula na kugawa maji kwa umati mkubwa wa watu. Ahmed al-Sedek, mwenye umri wa miaka 39 alisema hajalala nyumbani kwake tangu walipoanza kuweka kambi nje ya makao makuu ya jeshi Jumamosi iliyopita.

Chama cha upinzani cha Congress kinataka kuanzishwa kwa baraza la pamoja la kijeshi na kiraia ili kutawala katika kipindi cha mpito cha miaka minne.

Pia kimelitaka jeshi kukabidhi mamlaka kwa raia. Na habari za hivi punde zinasema kuwa baraza la mpito la kijeshi lilisema linapanga kuanza mazungumzo na makundi ya kisiasa baadaye leo.

Akizungumza na waandishi habari, mkuu wa kamati ya kijeshi na kisiasa, Omar Zein al Abidin, ambaye ameteuliwa na rais wa baraza la mpito la kijeshi, Mohammed Ahmed Awad Ibn Auf, alisema wanataka kujenga mazingira ya kufanyika mazungumzo na kwamba lenyewe halina suluhisho katika mzozo wa Sudan, bali suluhisho linatoka kwa waandamanaji.

"Baraza letu linawajumuisha mkuu wa polisi, mkuu wa usalama na kamanda wa vikosi vya jeshi, na hatutalazimisha kitu chochote kwa wananchi. Tunatarajia kuwa kipindi cha mpito kitakuwa cha miaka miwili, ingawa kinaweza kuwa kifupi hata kwa mwezi mmoja, iwapo mambo yatatatuliwa bila ghasia," alisema Zein al Abidin.

Mataifa yenye nguvu duniani ikiwamo Marekani na Uingereza, yamelitaka jeshi kuwaachia raia kuamua kiongozi wanayemtaka kuwaongoza na kwamba miaka miwili ni mingi kwa jeshi hilo kutawala. Mataifa hayo yamesema yanaunga mkono kipindi cha mpito cha amani na demokrasia mapema zaidi ya miaka miwili.

Umoja wa Ulaya kwa upande wake umelisihi jeshi kukabidhi haraka madaraka kwa utawala wa kiraia na kuwepo hali ya utulivu.

Hata hivyo, Umoja wa Afrika umelaani njia iliyotumika kumuondoa Bashir madarakani ukisema haikuwa sahihi katika kuzitatua changamoto zinazowakabili watu wa Sudan pamoja na matakwa yao.

*DW*




Waandamanaji nchini Sudan wakiwa nje ya Wizara ya Ulinzi mjini Khartoum. **PICHA: DW.**

# Waandamana kudai muasisi WikiLeaks aachiliwe

**SYDNEY, Australia**

KATIKA wakati ambapo Australia inasema itapinga adhabu ya kifo kwa Julian Assange pindi akipelekwa Marekani , maelfu wanaingia mitaani Sydney na Melbourne kudai muasisi huyo wa WikiLeaks aachiwe huru.

Julian Assange, raia wa Australia aliyeanzisha mtandao wa WikiLeaks alikamatwa akiwa katika ubalozi wa Equador mjini London na jaji kumkuta na hatia ya kuvunja masharti ya dhamana. Anakabiliwa na mashitaka nchini Marekani ya kufichua siri za serikali.

Waziri Mkuu wa Australia, Scott Morrison, alisema nchi yake haihusiki hata kidogo na mipango ya kumpeleka Marekani na kwamba Assange atapatiwa huduma za kawaida na maofisa wa ubalozi mdogo wa Australia.

Kwa upande wake, Waziri waMambo ya Nje, Marise Payne, akijibu hofu za mashabiki wa Assange kuhusu uwezekano wa adhabu atakayopewa nchini Marekani, alisema Australia inapinga moja kwa moja adhabu ya kifo". Aliongeza kusema Uingereza imetaka ihakikishiwe na Marekani kwamba Assange hatohukumiwa adhabu ya kifo pindi akipelekwa nchini humo.

Harakati za kumuunga mkono Assange zimeanza katika nchi alikozaliwa Australia. Watu wasiopungua 30 waliandamana katika eneo la kati ya Sydney baada ya kukusanyika nje ya ubalozi mdogo wa Uingereza na kutoa wito aachiliwe huru yule wanaemtaja kuwa "mshika bendera wa wanaopigania ukweli na uhuru wa mtu kuzungumza.

Wakibeba maandishi yanayosema "Aachiwe huru Assange. Asipelekwe Marekani,"waandamanaji hao walipaza pia sauti wakidai Assange "Msema kweli aachiwe huru na mjumbe asipigwe risasi". Kundi jengine dogo la watu wameandamana katika mji wa Melbourne pia.

Shirika la waandishi habari wa Australia, muungano wa mashirika ya vyombo vya habari na sanaa nayo pia yanaliunga mkono Assange aachiliwe huru. Mwenyekiti wa shirika hilo, Marcus Strom alisema Assange anaandamwa kwa sababu ya shughuli zake kama mwandishi habari.

Akikumbusha kwamba mwaka 2011 WikiLeaks walitunukiwa tuzo muhimu kabisa ya uandishi ya Australia, Strom alisema kadhia ya Assange inahusiana na uhuru wa vyombo vya habari.

"Julian Assange anaandamwa kwasababu ya shughuli za uandishi zilizoendeshwa na WikiLeaks na shughuli hizo zinahusiana na kufichua habari ambazo ni za maslahi bayana kwa jamii kuhusu visa vya kikatili, na pengine uhalifu wa kivita uliofanyika Iraq na Afghanistan" alisema mwenyekiti wa shirika la waandishi habari nchini Australia, Marcus Strom.

*DW*

# Madaktari Wacuba watekwa, polisi auawa

**NAIROBI, Kenya**

WATU wenye silaha ambao hawajafahamika wamewateka madaktari wawili wa Cuba wanaofanyakazi nchini Kenya na kufyatua risasi na kumuua polisi mmoja.

Kituo cha televisheni cha KTN na gazeti la Daily Nation nchini Kenya vimeripoti jana kuhusu shambulio hilo katika eneo la kaskazini mashariki mwa kaunti ya Mandera.

Daily Nation ilisema washambuliaji waliondoka na madaktari hao baada ya kumpiga risasi ofisa wa polisi.

Kwa upande wa televisheni ya KTN iliesema polisi wanashuku kwamba madaktari hao na watekaji nyara wao, wanaofikiriwa kuwa ni kutoka kundi lenye mahusiano na Al-Qaeda la Al-Shabaab, na kwamba wamekwenda Somalia.

Katika siku za nyuma, Mandera ilikuwa sehemu ya mashambulizi ya mara kwa mara, ambayo raia kadhaa pamoja na wanajeshi waliuawa. Kundi la Al-Shabaab limedai kuhusika na mengi ya mashambulio hayo.

*DW.*

# Maandamano Algeria yaongeza shinikizo

**ALGERIA, Algeria**

WAANDAMANAJI nchini Algeria wamejikusanya kwa ajili ya Ijumaa ya kwanza ya maandamano tangu tangazo la uchaguzi wa rais ili kuchukua nafasi ya rais aliyeondolewa madarakani Abdelaziz Bouteflika wakihofia njama ya kundi la watawala kuendelea kubaki madarakani.

Mitandao ya kijamii, chanzo cha maandamano ya umma ambayo yamesababisha kuondolewa kwa utawala wa miongo miwili wa Bouteflika, imeendelea kuwa na miito ya maandamano ya wiki ya nane, mara hii chini ya kauli mbiu ya Wataondoka wote.

Uchaguzi wa rais unatarajiwa kufanyika Julai 4, ofisi ya kiongozi wa mpito Abdelkader Bensalah, ilitangaza Jumatano iliyopita, saa chache baada ya kuahidi uchaguzi wa uwazi. Uteuzi wa spika wa baraza la Seneti Bensalah kuwa rais wa kwanza mpya wa Algeria katika miaka 20 umeshindwa kufikia madai ya waandamanaji.


*DW*

# HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro, baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na watu wengine kadhaa kujeruhiwa.
Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia, ni ajali iliyopangwa na muuaji , mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua kitendawili hiki. Fuatilia kisa hiki....

# Kisanduku Cheusi-43

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Alifikiria pia jinsi wananchi watakavyomlaani na kumuombea kila aina ya baya na kuitaka mahakama ifanye kazi yake haraka ili ahukumiwe.

Alimfikiria vile vile mke wake mtarajiwa Getrude atakavyoangua kilio atakapoona tukio hilo kwenye TV, lakini baadaye akitulia pia atamlaani na kuona ni mwanaume katili ambaye pia hata yeye akijichanganya anaweza kupata adhabu kama hiyo ya mwenzake au zaidi ya hiyo.

Baada ya kufikiri vyote hivyo, Mapunda alionekana ni kama amepagawa. Aliona ni bora afe kuliko kuchukuliwa kama kuku na kuwekwa hadharani mbele ya Watanzania akiwa hai, huku akiwa na tuhuma hizo. Ni bora tu tuhuma hizo zifike kwa Watanzania akiwa ameshakufa na yeye hatopata aibu ambayo ataipata akiwa hai.

"Bora nife kuliko aibu hii." Aliwaza. "Lakini siwezi kufa peke yangu. Ni lazima nifanye kitu humu ndani ili kama kufa tufe wote." Aliwaza.

Wakati akiwaza hilo, kengele ya hatari ilianza kulia kwenye ubongo wa Eddy.

Aliruka ghafla na kuokota moja ya gololi ambazo zilikuwa zimerushwa na Eddy ambazo aliwaambia kuwa ni mabomu.

Kitendo bila kuchelewa Eddy naye aliingiza mkono mfukoni na kutoa bastola ndogo iliyompiga Mapunda mkononi bila kutoa mlio.

Badala ya bastola kutoa mlio, Mapunda ndiye aliyetoa mlio wa kugugumia maumivu.

"Huwezi kufanya kitu chochote kwa sasa Mapunda. Umeshachelewa." Eddy alisema wakati Mapunda akiwa anajinyonganyonga kwa maumivu ya mkono uliokuwa umetapakaa damu.

"Hizo gololi haziwezi kulipuka kamwe, hata uzibonde na chuma. Hizo ni mpaka mimi nikamue hiki kitufe kilicho mkononi mwangu." Eddy alimpasha Mapunda huku akitabasamu.

Bado Mapunda alionekana hajakubali na kilichotokea, licha ya kwamba alikuwa ameumia mkono.

Alionekana kuna kitu anamnong'oneza baunsa wake mmoja.

Ni yule ambaye alijitaja kuwa alimuua Hellen. Eddy alihisi hatari. Hakujiuliza zaidi ya kupiga risasi mbili zilizompata sawia baunsa huyo kichwani na kutawanya ubongo.

Kitendo hicho kilichotokea kwa muda mfupi sana kiliwatisha wote waliobaki humo ndani.

Mapunda, pamoja na kuonyesha ubishi katika dakika za mwisho aliduwaa kana kwamba anaangalia filamu ya kutisha.

Hakuamini kile kinachotokea mle ndani. Akili yake ilitulia sasa na kuamua chochote kitakachotokea kitokee.

Saa tatu zilikuwa zimepita tangu vurumai zote zitokee ndani mle na hakuna mfanyakazi wake yoyote nje aliyekuja kumuokoa.

Akili yake ilidhani kuwa baada ya saa kadhaa, walinzi wake wa nje zaidi ya 50 wangekuwa na kazi ya kutafuta mle ndani kwani wana uhakika kuwa yumo, lakini kimya kilizidi kumfanya kuogopa na kuhisi hakuna uwezekano wowote wa kujiokoa.

"Wamepatwa na nini? Au wamenisaliti?" Alijiuliza.

Eddy kwa upande wake alifurahi kimoyo moyo kwani kwa mkono wake mwenyewe amefanikiwa kulipiza kisasi cha mpenzi wake Hellen.

"Nitakapomtia mikononi yoyote aliyekuua na kumuua kwa mkono wangu huu, nitakuwa nimemaliza msiba wako mpenzi wangu. Kwa sasa nitaomboleza kila siku mpaka nimtie mtu aliyokuua mbaroni. Na nakuahidi nitamkamata kwa mkono wangu huu." Alikumbuka maneno hayo aliyoyasema mbele ya maiti ya Hellen, nyumbani kwake Tabata Kimanga.

"Tayari nimetimiza ahadi niliyokuahidi, lala salama mpenzi wangu Hellen. Licha ya kuwa tulionana, kupendana na kukaa kwa kipindi kifupi tu, lakini nilipata vitu vingi kutoka kwako na nilitegemea kuwa ungekuwa mke wangu, lakini haikuwezekana. Sasa unaweza kupumzika kwa amani." Eddy alisali kimoyomoyo.

"Bwana Mapunda usidhani wewe ni mjanja sana. Na wala usidhani kuwa muda utakuokoa. Hapa hakuna yoyote atakayekuja kukuokoa, zaidi ya polisi kuja kukuchukua.

"Kumbuka nilipotoroka hapa kwa kuruka ukuta na kwenda nyumbani niliandika kila kitu nilichokiona, tangu nilipotekwa kwa kutaka mwenyewe, nilipelekwa wapi na nilikuwa jengo gani, lipo vipi, ulinzi wake ukoje na akina nani wapo ndani na pia mmiliki.

**"Kumbuka nilipotoroka hapa kwa kuruka ukuta na kwenda nyumbani niliandika kila kitu nilichokiona, tangu nilipotekwa kwa kutaka mwenyewe, nilipelekwa wapi na nilikuwa jengo gani, lipo vipi, ulinzi wake ukoje na akina nani wapo ndani na pia mmiliki.**

Karatasi hiyo nilimpa sekretari wangu Lilly na akaipeleka kwa bosi wangu. Na kati ya vitu nilivyochukua na redio ndogo ya mawasiliano na kuwaambia kuwa siku ambayo waje kwenye jengo hili kwa ajili ya kazi maalum ya kuliweka chini ya ulinzi na kuchukua watu wote muhimu kwetu walio kwenye jengo hili." Eddy aliongea ili kuzidi kuwapasha kuwa hawakuwa na njia yoyote ile zaidi ya kusalimu amri.

"Kwa hiyo hivi ninavyozungumza ni kwamba jengo hili lipo chini ya ulinzi kwa sababu tayari nimeshawapigia simu jeshi la polisi kitengo maalum na walinzi wenu wote wameshakamatwa."

Mapunda alionekana kuamini hilo, kwani haingewezekana muda wote ule walinzi wake washindwe kumsaka na kuingia kwenye chumba hiki kumuokoa, licha ya kwamba tayari ameshapiga king'ora kinachoashiria hatari.

"Bwana askari na mimi naomba niue tu kama mlinzi wangu." Yalikuwa na maneno yaliyotoka kinywani mwa Mapunda.

Mapunda aliona hatari iliyopo mbele yake. Kama atatiwa chini ya ulinzi, pamoja na dunia nzima kufahamu nini amekifanya, lakini pia hatokiepuka kitanzi. Hivyo aliona ni bora afe. Lakini kwa wakati huo hakuwa na silaha yoyote ile, tena akiwa chini ya ulinzi.

"Huwezi kufa kirahisi hivyo. Wewe ni mtu mkubwa sana." Eddy alitania.

"Wewe unatakiwa uwe mzima ili watu wamshuhudie bwana mkubwa, ambaye upande mmoja wa Shilingi anaheshimika kwenye jamii, mwekezaji na tajiri mkubwa Tanzania, lakini upande wa pili ni shetani halisi, aliyeua watu wasio na hatia, wakiwemo akinamama kwa sababu tu ya tamaa ya mapenzi." Alizidi kushindilia.

Ghafla mlango ukagongwa. Kulikuwa na aina fulani ya ugongaji ambao haukumtia wasiwasi Eddy, akafungua.

Aliyetangulia mbele ni Samson Mwakabana, Bosi Mkuu wa Usalama wa Taifa.

Nyuma yake aliongozana na maofisa wa vyeo vya juu wa polisi, pamoja na watu wengine watatu waliovalia kiraia.

"Bosi, nadhani kazi nitakuwa nimeshaimaliza. Yule pale mwenye shati ya bluu anaitwa Benson Mapunda. Huyu ndiye mhusika mkuu wa ajali ya basi la abiria iliyotokea miezi sita iliyopita huko Mikese na kuua watu zaidi ya 10, huku ikiaminiwa kuwa limeungua moto. Lakini pia ndiye mhusika mkuu wa mauaji wa watu wengine kama yile msichana aitwate Hellen mkazi wa Tabata Kimanga, Said, yule kijana mpaka kucha.

Na sababu zote za mauaji ni moja tu. Alitaka kumuua mpenzi wake Careen aliyepanda basi hilo la Bomoa Trans kwenda kufunga ndoa na mwanaume mwingine. Lakini hawa wengine ilikuwa ni kuficha siri hiyo iliyokuwa ikikaribia kutoka."

"Vizuri Eddy, hongera kwa kazi yako nyingine nzuri, lakini kama kawaida yako huwa ukimaliza kazi kama hizi hukosi ushahidi kwa sababu tunaweza kupeleka kesi mahakamani tukakwama." Mzee Mwakabana aliongea huku akikuna upara wake.

Eddy aliingiza mfukoni na kutoa redio ya kunasa sauti, akamkabidhi bosi wake.

"Humu mna kila kitu, na ni yeye wenyewe ndiye aliyekiri kwa kinywa chake na alifanya hivyo akidhani kuwa ataniua, hivyo kabla ya kunimaliza alitaka anayemuua ajue ukweli wote kabla ya kunimaliza.

Lakini Bosi ushahidi mwingine nitakuja kuuwasilisha kesho ofisini kwako. Kuna mahojiano ya watu kadhaa niliofanya nao huko Ifakara kama vile shangazi ya marehemu Bi. Mkali, Nassy, na wazazi wa mume mtarajiwa wa Carren, Mayambua, lakini pia kuna santuri CD aliyojirekodi bwana huyo kabla ya kujinyonga.

*Itaendelea Jumamosi*

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**OMBI LA URAIA**



**VIVIAN LEON NTIRANDEKURA**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa mambo ya ndani ya nchi, utaifa wake wa sasa ni BURUNDI nchi atokayo ni BURUNDI shughuli zake ameajiriwa, na anwani ya mwajiri wake ni S.L.P. 10915 mwanza Yupo hapa nchini tangu 1999.

Kwa yeyote mwenye taarifa/ sababu za kwanini mwombaji asipewe uraia wa Tanzania,atume taarifa ya maandishi kwa kamishna jenerali wa uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam..Kumb.Na.DN. 505469.

………………………..

**Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI**

215176402

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**ERICK KAFURIA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 412 DCQ TOYOTA.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **WMB/RB/5022/2019.**

115175102

---

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**YUSTA LIVISTINO LUBELEJE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 962 BAS (BOXER).

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: UR/RB/698/2019.**

115169702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 12 /04/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya ALHAMISI tarehe 13/04/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka MOROGORO kuelekea LONGIDO gari hilo lenye namba za usajili: **T 188 APK / T 741 CPB / T 985 ABJ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 17
   Upana – mita 3.0
   Kimo – mita 4.4
3. Njia itakayotumika MOROGORO hadi LONGIDO kupitia MSATA ROAD gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115175702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA / 63)**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA MBINGA MJINI**
**WILAYA YA MBINGA**
**MADAI NAMBARI 13 YA 2018**
**Mdai: THEOLINDIS NICOLAUS MBUNDA**
**AMDAI**
**Mdaiwa CRESENSIA CHIWALO**

Kwa **CRESENSIA CHIWALO MTAA WA MATARAWE MBINGA**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
Unatakiwa Mahakamani kwa ajili ya malipo ya fedha Tshs 2,046,550/= Milioni mbili arobaini na sita elfu mia tano hamsini tu. Mali ya mdai.

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe 15/04/2019 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 03/04/2019

115176802

---

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**MARGARETA FRANCIS LAUWO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki iliyosajiliwa kwa namba MC854 AVM. Engine No. 162FMJF5062116. Chassis No LFSGE2PK003910.

Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu nae.
AR/RB/16668/2017.

115174302

---

**KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI**

**VINCENT J. KIBWANA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 695 DJE TATA na T 959 DJD TATA.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1973/2019.**

115175002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 11 /04/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI** tarehe 13/04/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **ARUSHA** kuelekea BABATI gari hilo lenye namba za usajili: **T827 BCN / T741 CPB.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 17
   Upana – mita 3.0
   Kimo – mita 3.2
3. Njia itakayotumika **ARUSHA hadi BABATI kupitia BABATI ROAD** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115174201

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO YA MTIBWA**
**ILIYOPO WILAYA YA MVOMERO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:19..2019**

| | |
|---|---|
| **Mdai:** | **SUZANA GERVAS SWAI** |
| | **DHIDI YA** |
| **Mdaiwa:** | **PROSPAR TITUS MBUNJU** |
| **Kwa:** | **PROSPAR TITUS MBUNJU** |
| **Ombi la Mdai:** | **SUZANA GERVAS SWAI** |
| **Madai ya:** | **TARAKA NA MATUNZO YA MTOTO.** |

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 24 mwezi 04 mwaka 2019 saa 02:00 Asubuhi.Siku ya JUMATANO.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 11 mwezi 04 mwaka 2019.

215175502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI2)**

Katika mahakama ya mwanzo MJINI TANGA
Usimamizi wa mirathi………55………2019

Ombi la **FUAD ABDULRAHIM BARAHIYANI** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu **MOHAMED ABDULRAHIM SALIM**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 2/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 11-4-2019

215176902

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI**

**MAKUNDI BOX MOROGORO** anatangaza kupotelewa na kadi pikipiki yenye namba za usajili MC 595 BXK model SANLG. Yenye chasis namba :

LBRSPJB57J901206 na Injini namba : SL157FMI*18913578.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi,

Taarifa ya Polisi: **MOR/TR/RB/7300/2018**

215175302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:24..2019**

| | |
|---|---|
| **Mdai:** | **MATERINA MSING'A ALEX** |
| | **DHIDI YA** |
| **Mdaiwa:** | **VALERI ALBERT KWEMBE** |
| **Kwa:** | **VALERI A.KWEMBE WA MBOZI - MBEYA** |
| **Ombi la Mdai:** | **MATERINA MSING'A ALEX** |
| **Madai ya:** | **TARAKA,MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO.** |

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 18 mwezi APRIL mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 08 mwezi APRIL mwaka 2019.

215175402

---

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**NANDHRA ENGINEERING & CONSTRUCTION** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye namba za usajili T 967 ABJ.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **OB/RB/7580/2019.**

115175602

---


KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

0767 223311


---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:101..2018**

| | |
|---|---|
| **Mdai:** | **HELLEN MNDEME DHIDI YA** |
| **Mdaiwa:** | **SHANAM ABRAHAM** |
| **Kwa:** | **SHANAM ABRAHAM IRINGA** |
| **Ombi la Mdai:** | **HELLEN MNDEME** |
| **Madai ya:** | **PESA SHILINGI 1,200,000/= NA GHARAMA ZA KESI ADA 15,000 ERV.** |

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 23 mwezi 04 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 11 mwezi 04 mwaka 2019.

215176502


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# SMALLING: KUMUUMIZA MESSI ILIKUWA NI AJALI TU

**MANCHESTER, England**

BEKI wa Manchester United, Chris Smalling amefunguka mengi baada ya mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona ambapo lilitokea tukio la kumuumiza nyota, Lionel Messi.

Katika mchezo huo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya uliopigwa kwenye dimba la Old Trafford, Man United walifungwa bao 1-0.

Baada ya tukio hilo Smalling aliongelea na kusema kuwa:- "Tulizungumza baada ya mchezo na tulikuwa na majadiliano mafupi na tukapeana mikono.

"Anajua ilikuwa ni ajali tu."

Alifafanua zaidi juu ya changamoto ya angani ambayo imesalia mpinzani wa Argentina, Smalling alisema: "Sikujua wakati ambao niliruka kuwania mpira kama ningemgusa"

"Luis Suarez alikuja kwangu baada ya mchezo pia. Tulikuwa na mazungumzo mazuri na alinipa mkono baadaye na kusema 'Kila la kheri'.

"Kwa upande wangu ni nzuri sana wakati unaweza kuwa na vita hiyo kwenye soka na kisha baada ya mchezo kunakuwa na heshima, kwa sababu kila mtu anataka na anajitahidi kufanya vilivyo bora zaidi katika upande wake."

# COSTA
## AFUNGIWA MECHI NANE

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Diego Costa amefungiwa mechi nane baada ya kuthibitika kuwa alimtukana mwamuzi, Jesus Gil.

Costa amefungiwa kucheza mechi nane za Ligi Kuu Hispania maarufu kwa jina la La Liga kwa kumtusi mama mzazi wa mwamuzi huyo, kosa hilo alilitenda wakati wa mchezo dhidi ya Barcelona uliochezwa kwenye Uwanja wa Nou Camp.

Katika mchezo huo, Atletico ilifungwa mabao 2-0, shukrani kwa Luis Suares na Lionel Messi ambao walifunga magoli katika mchezo huo.

Katika mchezo huo, Costa alionekana kumlalamikia mwamuzi na baadae kumtolea lugha ya matusi na akaonyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja.

Kadi hiyo alionyeshwa katika dakika ya 28 na na sasa atazikosa mechi zote za ligi hiyo zilizobakia.

Kwani hadi sasa Atletico imebakiwa na mechi saba kumaliza ligi hiyo na hivyo, ataukosa na mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa msimu ujao.



# Hazard ameamua kuondoka Chelsea

**LONDON, England**

NYOTA wa Chelsea, Eden Hazard ameripotiwa ameshafanya uamuzi wake wa kwenda kujiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huu, hivyo hakuna kitu ambacho wababe hao wa Stamford Bridge watakifanya asiondoke.

The Blues wanahangaika kumshawishi Hazard asaini dili jipya baada ya hili la sasa kufika tamati mwakani, lakini mpango huo huonekani kukamilika kutokana na mchezaji mwenyewe tayari ameshahamishia mawazo yake ya kwenda kucheza Bernabeu.

Madrid inaendelea kuhusishwa na mchezaji huyo, ambaye Chelsea hawatakuwa na ujanja zaidi ya kukubali tu kumpiga bei jambo ambalo itabidi wakubali yaishe kwa sababu Los Blancos hawapo tayari kutoa pauni milioni 100 ili kupata huduma ya mchezaji huyo, ambaye mwakani tu mkataba wake utafika mwisho.




Ripoti zimekuwa zikidai kwamba Hazard anajipangaa kulazimisha uhamisho wa kwenda Real Madrid mwishoni mwa msimu huu ili kutimiza ndoto zake huku Chelsea wakiwa kwenye wakati mgumu wa kumzuia mchezaji huyo kama watashindwa tena kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Hazard amekuwa kwenye kiwango bora kabisa msimu huu, akifunga mabao 19 na kutengeneza nafasi 12 za kufunga katika mechi 42 alizoitumikia klabu hiyo ya London kabla ya mchezo wao wa usiku wa jana Alhamisi kwenye Ligi ya Europa.

Paul Pogba amekuwa miongoni mwa wachezaji watatu wakiwemo Hazard wa Chelsea na Mbappe wa PSG kuhitajika na kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane mwisho wa msimu kitu ambacho kinadaiwa kumvutia sana Pogba.

Pogba amekuwa na msimu mzuri chini ya Solskjaer ukilinganisha na Jose Mourinho, katika mechi 12 za mwanzo za Solskjaer, ndani ya Man United Pogba alifunga magoli tisa.

## HABARI MICHEZO



# UNITED
## KUWAKATA WACHEZAJI MISHAHARA

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imesema kuwa itawakata nyota wake mishahara yao kwa asilimia 25 kama watashindwa kufuzu katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Watalazimika kukatwa robo ya mishahara yao kama wakishindwa kuipeleka timu yao katika michuano hiyo ya Ulaya.

Jambo hilo limewatia nguvu Real Madrid katika mbio zao za kumchukua staa wa United, Paul Pogba ambaye wameanza kumnyatia kwa kasi kwa ajili ya kumchukua katika dirisha kubwa la usajili la majira ya joto ambapo wapo tayari kuvunja benki kwa ajili ya staa huyo.

Mchezaji mwingine ambaye United inapambana kumbakisha ni kipa, David de Gea ambaye anataka mshahara mkubwa zaidi ili abaki Old Trafford lakini endapo United itakosa nafasi nne za juu itakuwa na kazi kubwa ya kumuongezea mshahara zaidi staa huyo wakati wao wakiangalia zaidi namna ya kushusha mishahara.

Staa mwingine ambaye anaweza kuathirika na suala hili ni nyota Marcus Rashford ambaye bado hajasaini mkataba mpya lakini anaweza kujikuta akikatwa mshahara wake kama klabu itaangukia katika michuano ya Europa.

Nyota wa kimataifa wa Chile, Alexis Sanchez, tayari anatakiwa kuondoka klabuni hapo bila ya kujali kama United itafuzu katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya au vinginevyo. United inataka kuondokana na mshahara wake mkubwa wa pauni 500,000 kwa wiki ambao unawaumiza.

Mpaka sasa United wako katika nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu England na ipo katika upinzani mkali kutoka kwa Chelsea, Tottenham na Arsenal katika kuwania nafasi mbili za kucheza Ulaya baada ya Manchester City na Liverpool kuonekana kuzitwaa nafasi mbili za awali.

United pia inaonekana kupitia kamba nyembamba katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuchapwa 1-0 katika pambano la awali na Barcelona nyumbani kwao Old Trafford juzi Jumatano usiku. Wana kazi ngumu wiki ijayo watakaporudiana na Barcelona ugenini.

Ubingwa wa Ulaya ni moja kati ya njia ambayo inaweza kuwarudisha United katika michuano hiyo msimu ujao lakini kwa jinsi hali ilivyo mambo yatakuwa magumu kwao kutokana na kuruhusu kichapo cha nyumbani.

Kupunguzwa kwa mishahara kwa wachezaji ni kwa ajili ya kuilinda United mapato ya United yasishuke kutokana na klabu hiyo kupoteza pesa nyingi pindi inaposhindwa kushiriki katika michuano ya Ligi ya Mabingwa. Kama vile haitoshi, baadhi ya kampuni ambazo zinadhamini United itapunguza pesa wanazoingiza klabuni hapo kama United itashindwa kufuzu katika michuano hiyo msimu ujao. Hii ni kwa mujibu wa vipengele vya mikataba baina yao.

Kampuni ya Adidas itapunguza asilimia 30 ya dau ambalo wameweka Manchester United endapo timu hiyo itashindwa kufuzu katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa misimu miwili mfululizo.

United pia itashindwa kuwa na mvuto kwa baadhi ya mastaa ambao inawafukuzia kwa ajili ya kuongeza makali ya kikosi chao msimu ujao. Mastaa wengi ambao inawafukuzia ni wale ambao klabu zao zinashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kama vile, Kalidou Koulibaly wa Napoli, Toby Alderwierld wa Tottenham na kipa, Jan Oblak wa Atletico Madrid.

## Madrid haitamuuza Raphael Varane

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid itakataa kumuuza beki wake nyota, Raphael Varane wakati wa kipindi cha majira ya joto chini ya euro milioni 500.

Hii ni maana yake ni kwamba uwezekano wa mchezaji huyo kwenda Manchester United, Manchester City, Liverpool, Juventus, Bayern Munich au Paris Saint-Germain haupo.

Uvumi ulienea mwezi uliopita kwamba, Varane amefikia uamuzi wa kutaka kuondoka Madrid kwa ajili ya kutafua changamoto mpya.

Mfaransa huyo ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu Hispania, La Liga, mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Copa del Rey na Klabu Bingwa ya Dunia wakati akijiunga na timu hiyo mwaka 2011.

Alikuwa mchezaji pekee kwa timu hiyo wakati aliposhinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Dunia mwaka jana.

Mapema mwezi uliopita kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, alisema kwamba hatamuachia mchezaji huyo aaondoke.

"Hapana, siwezi kufikiri kuwa hapa Real Madrid bila yeye. Hakuna anayetaka yeye kuondoka," kocha huyo wa dimba la Bernabeu alisema.




## Ancelotti: Napoli itapindua matokeo kwa Arsenal

**ROME, Italia**

CARLO Ancelotti amesisitiza kwamba Napoli inaweza kupindua matokeo katika mchezo wa marudiano wa robo fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Arsenal.

Arsenal usiku wa kuamkia jana iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 katika mchezo uliopigwa kwenye uwanja wa Emirates.

Alisema: "Leo (juzi) tulifanya makosa makubwa, lakini tuna nafasi ya kubadilisha matokeo kwenye mchezo wa marudiani.

"Arsenal walitushangaza, lakini naamini kwamba tutaweza kucheza vizuri katika mchezo wa pili na kupata ushindi..

"Najua wazi kwamba mchezo utakuwa mgumu, lakini naamini tutaweza kubadilisha matokeo, na naiona Napoli ikifuzu nusu fainali ya Ligi ya Europa."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BALE AWEKWA SOKONI RASMI

●●● Ni baada ya Madrid kutaja thamani ya mshambuliaji huyo raia wa Wales…

**MADRID, Hispania**

HATIMAYE Real Madrid imefikia uamuzi wa kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale katika kipindi cha majira ya joto kwa dau la pauni milioni 113.

Baada ya kudumu klabuni hapo kwa misimu sita na kutwaa mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa hapo Bernabeu, Bale anajiandaa kuondoka Madrid na inaonekana kuwa na nafasi kubwa ya kurejea kwenye Ligi Kuu England.

Na kwa mujibu wa gazeti maarufu la Hispania liitwalo AS, Real inaamini kuwa klabu moja kubwa ya England ina uwezo wa kutoa kiasi hicho cha fedha na kumsajili mshambuliaji huyo.

Real inaamini pia kiasi hicho cha fedha kilichotajwa katika mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ni sahihi kutokana na thamani yake ilivyo sokoni na kiasi hicho cha pesa kitakachopatikana kitaingia kwenye fungu la usajili ambalo klabu hiyo iko katika mawindo ya kuwasajili nyota kadhaa wakiwamo Neymar, Kylian Mbappe na Philippe Coutinho.

Hata hivyo, vigogo hao wa Hispania wamekaririwa wakisema kuwa hawatakuwa tayari kupunguza ada hiyo ya usajili wa Bale mara tu dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa.

Kitu kingine ambacho kimekuwa kikikwamisha uhamisho wa Bale ni kiasi cha mshahara cha pauni milioni 26 anacholipwa kwa mwaka, ukiwa bado haujakatwa kodi, jambo ambalo limekuwa likikwamisha klabu mbalimbali zinazomhitaji mshambuliaji huyo.

Pia, gazeti hilo la AS limeandika kuwa Real iko wako tayari kufanya mazungumzo na Manchester United kwa ajili ya kubadilishana na kiungo wake Mfaransa, Paul Pogba, huku pia klabu hiyo ikiongeza kiasi kidogo cha fedha katika kukamilisha usajili huo.

Zinedine Zidane, ambaye amerejea katika klabu hiyo kwa mara ya pili, anatajwa kuhitaji kufanya kazi na kiungo huyo Mfaransa.

Mchakato mwingine ambao Madrid watakuwa radhi kuufanya ni kama Bale atakubali kurejea katika klabu yake ya zamani ya Tottenham, ambapo Madrid itabadilishana kwa kumsajili, Christian Eriksen.

Bale ameichezea Madrid mechi 227, amefunga mabao 102 tangu alipojiunga na timu hiyo Septemba 2013 akitokea Spurs kwa dau la pauni milioni 85.3 ambalo lilivunja rekodi wakati huo.

Mshambuliaji huyo ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, La Liga, Copa del Rey, Kombe la Hispania , matatu ya Kombe la Ulaya na Klabu Bingwa Dunia.

## KWA UFUPI

### ARSENAL YAMTAKA HERRERA

ARSENAL itawasilisha maombi ya kumsajili kiungo wa Manchester United, Ander Herrera (29) katika dakika za lala salama kwenye majira ya joto kabla ya Mhispania huyo kufikia uamuzi wa kujiunga na Paris St-Germain. ***(L'Equipe, via Express)***

### QATAR KUGEUKIA EPL

KAMPUNI ya Michezo ya Qatar, ambayo inamiliki mabingwa wa Ligue , PSG, sasa inafanya uchunguzi kuona kama inaweza kununua klabu mojawapo inayoshiriki Ligi Kuu England. ***(Telegraph)***

### ZOUMA, GOMES KIMEELEWEKA

KOCHA wa Everton, Marco Silva amesema kuwa anataka kumsajili beki Mfaransa, Kurt Zouma (24) na kiungo Mreno, Andre Gomes (25), wote kwa sasa wako katika mkopo wa muda mrefu katika klabu hiyo wakitokea Chelsea na Barcelona. ***(Liverpool Echo)***

### GUEYE ANUKIA UNITED

MARCO Silva, kocha wa Everton amesema kuwa "hafahamu lolote" kuhusiana na tetesi kwamba kiungo wake Msenegali, Idrissa Gueye (29), anatarajia kujiunga na Manchester United katika kipindi cha majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

### ARSENAL, EVERTON VITANI

ARSENAL na Everton zote kwa pamoja ziko katika mazungumzo ya kumsajili winga wa Ajax, David Neres (22), ambaye dau lake limetajwa kuwa ni pauni milioni 34.5 ili kujiunga na klabu hizo zinazoshiriki Ligi Kuu England. Mapema Januari mwaka huu Ajax ilikataa ofa ya kumuuza iliyowasilishwa na Borussia Dortmund. ***(Telegraph)***

### ERIKSEN "KUMBURUZA" POGBA

KIUNGO wa Tottenham, Christian Eriksen anatajwa kuwa ndiye nyota wa kwanza anayewindwa na Real Madrid, huku Rais, Florentino Perez akimpa nafasi zaidi nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 kuliko kiungo wa Manchester United, Paul Pogba. ***(El Confidential, via Mirror)***

### JOVIC AIKACHA BARCA

BABA wa straika wa Eintracht Frankfurt na Timu ya Taifa ya Serbia, Luka Jovic (21), amesema hataki mwanae ajiunge na Barcelona kwa sasa kwa sababu anahofia kupata nafasi finyu ya kucheza. ***(Bild - in German)***

### VARANE KUIKAMUA UNITED

REAL Madrid imesema kuwa haitakubali kumruhusu beki wake wa kati Mfaransa, Raphael Varane (25), kuondoka klabuni hapo kwa dau lisilopungua pauni milioni 431 ambalo limetajwa katika mkataba wake. ***(AS)***

### BURNLEY YAJIPANGA

BURNLEY inatarajia kumpa ofa golikipa Nick Pope (26), ambaye pia anawindwa na Bournemouth wakati mlinda mlango mwingine wa England Joe Hart (31), naye anatajwa yuko mbioni kuondoka klabuni hapo. ***(Mail)***

### LEWANDOWSKI, COMAN WAZICHAPA

STRAIKA wa Bayern Munich, Robert Lewandowski (30) na winga Mfaransa, Kingsley Coman (22), walipigana wakati wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo juzi. ***(Bild - in German)***

### NKUNKU AIKACHA PSG

ARSENAL inatarajia kumsajili kiungo Mfaransa, Christopher Nkunku (21), ambaye amekataa ofa ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia Paris St-Germain. (Le Parisien - in French)

### DIA MAMBO SAFI

MANCHESTER United imempa ofa ya mkataba wa miaka minne, golikipa wa Marseille Mfaransa, Ahmadou Dia ambaye ana umri wa miaka 20. ***(L'Equipe, via Metro)***

## HABARI MICHEZO

# SIMBU, FAILUNA KUSHIRIKI NGORONGORO MARATHONI

Na Woinde Shiza, ARUSHA

WANARIADHA nyota wa hapa nchini, Alphonce Simbu, Failuna Matanga na Joseph Panga wamethibitisha kushiriki katika mbio za Ngorongoro Marathon zinazotarajiwa kufanyika Aprili 20 mwaka huu, imeelezwa.

Nyota wengine waliothibitisha kushiriki mbio hizo ni pamoja na Angelina Tsere, Magdalena Shauri, Fabian Joseph, Faraja Damas na Natalia Elsante.

Akizungumza na gazeti hili jana, mratibu wa mbio hizo, Meta Petro, alisema kuwa mbio za mwaka huu zinatarajiwa kushirikisha wanaridha zaidi ya 1,000 kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.

Petro alisema kuwa anaamini mbio za mwaka huu zitakuwa na ushindani zaidi kutokana na washiriki kufanya maandalizi kwa muda mrefu.

Alisema kuwa mbio hizo zitakuwa za kilomita 21 (nusu marathoni), kilomita tano pamoja na za kilomita 2.5 ambazo zimeandaliwa maalum kwa ajili ya watoto.

Mratibu huyo alitaja zawadi kwa mshindi wa kwanza wa mbio za nusu marathoni atapata Sh. milioni moja wakati mshindi wa pili ataondoka na Sh. 500,000 huku Sh. 300,000 zikienda kwa mwanariadha atakayemaliza katika nafasi ya tatu kwenye mbio hizo.

Alitaja malengo ya mbio hizo ambazo zinafanyika kwa mwaka wa 12 sasa ni kupiga vita ujangili pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani.

"Unajua wananchi wengi, ninamaanisha Watanzania wengi wamekuwa na tabia ya kutotembelea hifadhi zetu za taifa, hivyo mbio hizi zitasaidia kuhamasisha wananchi kuwa na tabia ya kutembelea hifadhi zetu," alisema Petro.

Alitaja zawadi nyingine zitakazotolewa kwa wanariadha watakaofanya vizuri ni fursa ya kutembelea Hifadhi ya mbuga ya wanyama ya Ngorongoro kwa ajili ya kujionea vivutio vilivyopo katika hifadhi hiyo.



Wachezaji wa kimataifa wa Simba wakiwa katika Uwanja wa Ndege wa zamani wakisubiri kuanza safari ya kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kuwafuata wapinzani wao TP Mazembe. Kutoka kushoto ni Emmanuel Okwi, Meddie Kagere, Juuko Murshid na James Kotei. **PICHA: SSC**

# Waogeleaji kusaka bingwa wa Tanzania

Na Renatha Msungu

MASHINDANO ya kuogelea ya Klabu Bingwa Taifa yanatarajiwa kufanyika kuanzia leo kwenye bwawa la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST), lililopo Upanga, jijini Dar es Salaam.

Jumla ya klabu 10 zinatarajiwa kushiriki mashindano hayo. Shule ambazo zitashiriki ni pamoja na Bluefins, Champion Rise, Mis Piranhas, Mwanza (MSC), FK Blue, Wahoo (Zanzibar), ISM-Moshi, ISM-Arusha,FK Blue Marlins, Talis-IST na mabingwa watetezi, Dar es Salaam (DSC). Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya mashindano hayo, Hadija Shebe alisema kuwa waogeleaji wa Tanzania wanaoishi nje ya nchi wamewasili kwa ajili ya kushiriki katika mashindano hayo ambayo yatakuwa ni ya siku mbili.

**Shebe aliwataja wao geleaji wanaotarajiwa kuchuana kutokana jijini hapa kuwa ni Sonia Tu miotto, Maia Tumiotto, Collins Saliboko, Dennis Mhini, Chichi Zengeni, Natalia Sanford, Smriti Gorkarn na Delvin Bar ick wote kutoka Shule ya St Felix iliyoko Uin gereza.**

Wengine ni Christian Shirima anayetoka Ukraine, Isam Sepetu (Afrika Kusini), Hilal Hemed na Kangeta wanaotokea klabu ya Hamilton Aquatic ya Dubai.

Alisema kuwa mashindano hayo yamepangwa kuanza saa 2.00 asubuhi na waogeleaji watashindana katika staili tano ambazo ni Freestyle, Breaststroke, Butterfly, Backstroke na Individual Medley.

Kwa mujibu wa Hadija, waogeleaji hao pia watashindana katika mashindano ambayo yamepitishwa na Shirikisho la Mchezo wa Kuogelea Duniani (Fina) kuwa ya kutafuta alama za kufuzu mashindano ya Dunia yaliyopangwa kufanyika nchini Korea mwezi Julai.

Aliongeza kuwa kutakuwa na jumla ya vipengele 108 vya mashindano na kila klabu imetakiwa kuwakilishwa na waogeleaji wawili katika kila kipengele cha mashindano hayo ambayo pia vimepangwa kutokana na umri.

## Wagombea ZFA wang'atwa sikio

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KOCHA wa Kipanga FC, Rashid Omar amewashauri viongozi wapya watakaochaguliwa katika Chama za Soka Zanzibar (ZFA) wazingatie maslahi ya mchezo huo ili lisonge mbele ikilinganishwa na hali ilivyo hivi sasa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Omar, alisema ili soka la Zanzibar liweze kusonga mbele sawa na kasi ya maendeleo iliyopo duniani, ni vema viongozi wajao wahakikishe kiwango cha mpira kinapanda.

Omar alisema kuwa anataka kuona kiwango cha soka za visiwani hapa kinarejea kwenye ushindani kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma ambapo Zanzibar ilikuwa ikifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya ndani na nje ya nchi waliyokuwa wanashiriki.

Alisema kuwa viongozi hao wapya watakaoingia madarakani wanapaswa kuzingatia mambo matatu muhimu ambayo aliyataja kuwa ni kuhakikisha Timu ya Taifa ya Vijana inaandaliwa mapema kama ilivyo kwa Tanzania Bara na kuimarisha mahusiano na shirikisho la kimataifa kama CAF na FIFA.

Alitaja sababu nyingine ni kuhakikisha wanawakabidhi makocha wenye elimu ya juu dhamana ya kufundisha ili kuharakisha maendeleo katika ngazi za klabu na hatimaye kufikia malengo yaliyotarajiwa.

"Makocha ndio wanatengeneza timu ambazo zinaweza kufanya vizuri au kufanya vibaya katika mashindano tutakayoshiriki, hivyo ZFA ijayo inapaswa kuzingatia juu ya ushirikiano na makocha wa klabu zote wenye uzoefu na kazi hii ya kufundisha jambo ambalo litasaidia kupunguza lawama kutoka kwa waamuzi." aliongeza.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.YANGA | 31 | 23 | 5 | 3 | 51 | 22 | 74 |
| 2.AZAM | 30 | 18 | 9 | 3 | 48 | 18 | 63 |
| 3.SIMBA | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4.LIPULI | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 5.MTIBWA SUGAR | 31 | 13 | 6 | 12 | 32 | 24 | 45 |
| 6.KINONDONI MC | 32 | 9 | 15 | 8 | 32 | 23 | 42 |
| 7.TZ PRISONS | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 8. COASTAL UNION | 32 | 9 | 14 | 9 | 28 | 31 | 41 |
| 9.MBEYA CITY | 31 | 11 | 7 | 13 | 31 | 33 | 40 |
| 10.SINGIDA UNITED | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 11.NDANDA | 31 | 10 | 10 | 11 | 21 | 30 | 40 |
| 12.JKT TANZANIA | 32 | 9 | 12 | 11 | 20 | 27 | 39 |
| 13.STAND UTD | 33 | 10 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 14.MWADUI | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 15.ALLIANCE | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 16.MBAO | 33 | 9 | 11 | 13 | 19 | 33 | 37 |
| 17.RUVU SHOOTING | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 18.KAGERA SUGAR | 32 | 8 | 12 | 12 | 26 | 34 | 36 |
| 19.BIASHARA UTD | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20.AFRICAN LYON | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# Michezo

Jumamosi Aprili 13, 2019

Nipashe




**Bale awekwa sokoni rasmi** HABARI UK 30




Mlezi wa Serengeti Boys na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi (katikati) akiwa na mhamasishaji wa Timu za Taifa kutoka Manyara, Ikizu Kicheko (kushoto), wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti na zawadi mbalimbali askari waliofanya vizuri kwa mwaka 2018. Mwingine ni Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# DK. MENGI AWATANGAZIA NEEMA SERENGETI BOYS

## ●●● Kila mmoja kupata Sh. milioni 20 endapo watafuzu kushiriki Fainali za Dunia...

**Na Romana Mallya**

MLEZI wa Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), Dk. Reginald Mengi ambaye pia ni Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, ameahidi kutoa Sh. milioni 20 kwa kila mchezaji wa timu hiyo endapo watafanikiwa kukata tiketi ya kucheza fainali zijazo za Kombe la Dunia kwa Vijana.

Timu nne zitakazofanya vema katika Fainali za Vijana za Afrika zitakazoanza kuchezwa hapa nchini kuanzia kesho zitafuzu kushiriki Fainali za Dunia ambazo zitafanyika baadaye mwaka huu nchini Brazil.

Ahadi hiyo ilitangazwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi, Paul Makonda na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti na zawadi mbalimbali kwa askari waliofanya vema kazini kwa kipindi cha mwaka jana.

Makonda alisema kuwa Dk. Mengi ameahidi kiasi hicho cha fedha kwa kila mchezaji wa Serengeti Boys endapo watashinda mechi mbili za hatua ya makundi za Fainali za Vijana ambazo zitawapa tiketi ya kushiriki michuano hiyo ya Kombe la Dunia.

"Serengeti Boys tunatamani mshinde, na mkishinda mtakuwa mmetuwakilisha vema, mlezi wenu ameongeza nguvu kwa kuipa kamati heshima ya kutoa Sh. milioni 20 kwa kila mchezaji, mkishinda mechi ya kwanza maana yake mmetengeneza nusu ya hapo, mkimaliza ya pili maana yake kombe la dunia hilo," Makonda alitangaza ahadi ya Dk. Mengi.

Alisema kuwa hii ni zawadi nyingine ya juu kutolewa baada ya Rais, John Magufuli kuwapa wachezaji wa Taifa Stars zawadi ya viwanja jijini Dodoma kutokana na ushindi wa mabao 3-0 walioupata dhidi ya Uganda (The Cranes).

"Mkishinda mchezo huu hamuwezi kujua mtakuwa mmemuhamasisha Rais Magufuli kwa namna gani, Rais ataendelea kuungana nasi kama anavyofanya kwa upendo," Makonda alisema.

Makonda alitaja ahadi nyingine za kamati yao kuwa ni chombo cha habari ambacho kitahamaisha kwa kiwango cha juu michuano hiyo kitapata zawadi ya Sh. milioni 10 pamoja na cheti cha hamasa huku mwandishi mmoja mmoja atakayefanya vizuri katika kampeni ya kuhamasisha Serengeti Boys ishinde kwenye michuano hiyo atazawadiwa Sh. Milioni mbili.

Makonda katika kuhamasisha makundi mbalimbali kwenye jamii kufanya kampeni za hamasa, alisema amegundua chama chenye nguvu ni cha walevi na kuliomba kundi hilo liendelee kushiriki katika kampeni ya kuinga mkono Serengeti Boys kama lilivyofanya kwenye mechi ya Taifa Stars dhidi ya Uganda.

"Klabu ya Yanga ina mashabiki, Simba ina mashabiki, Chadema wanao, CUF wanayo sasa, kwa utafiti wangu nimebaini chama chenye nguvu na umoja ambao wakiamua jambo linakuwa ni chama cha walevi. Hiki chama ni hatari sana," aliongeza.

Pia alisema ametuma maombi Shirika la ndege la Taifa ATCL kuomba ndege ya Dreamliner ambayo itawabeba wachezaji wa Taifa Stars kuelekea katika Fainali za Afrika (AFCON 2019) ambazo zitachezwa kuanzia Juni 21 hadi Julai 13 mwaka huu huko Misri.

Kiongozi huyo aliwataka pia askari waliopata zawadi watengeneze picha za "video fupi" kwenye uwanja wa kituo cha polisi Oysterbay kuhamasisha ushindi wa timu hiyo.

Serengeti Boys ambayo iko katika Kundi A itafungua pazia la Fainali za Vijana za Afrika kwa kuwakaribisha yosso wenzao kutoka Nigeria, mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

# Simba: Ni jasho na damu Kongo

**Na Somoe Ng'itu**

TUTAPAMBANA! Hayo ndio maneno ya nahodha wa Simba, John Bocco, kuelekea mchezo wa marudiano wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji TP Mazembe utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Lubumbashi.

Kikosi cha Simba kilitua salama mjini Lubumbashi jana asubuhi tayari kwa mchezo huo ambao mshindi wa jumla atafanikiwa kuingia hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo ya kimataifa yanayofanyika kila mwaka hapa barani Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kuondoka nchini, Bocco, alisema kuwa wamekwenda Lubumbashi kwa kazi moja ya kupambana kusaka ushindi na kamwe "fitna" za nje ya uwanja hazitawatoa mchezoni.

Bocco alisema kuwa wachezaji wa timu hiyo wanafahamu mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani, lakini wanawaambia mashabiki wao wasiwe na hofu ya aina yoyote.

Alisema kuwa watacheza kwa utulivu na umakini kwa sababu TP Mazembe ni moja ya timu kubwa barani Afrika na inaundwa na wachezaji wenye uzoefu na mashindano mbalimbali ya kimataifa.

"Wachezaji tuko katika morali nzuri, katika ari nzuri, kikubwa tunaenda kupambana ili kufanikisha tunavuka katika hatua hii,...tunajua mchezo utakuwa mgumu, TP Mazembe ni timu kubwa, haitakuwa rahisi," alisema mshambuliaji huyo.

Aliongeza kuhusu kukosekana kwa beki wao wa kati, Paschal Wawa hakuwavunji moyo kwa sababu timu yao ina kikosi kipana na ni jukumu la benchi la ufundi kupanga mchezaji mwingine atakayeziba pengo hilo.

Naye mshambuliaji Mnyarwanda, Meddie Kagere, alisema kuwa hakuna kisichowezekana endapo watacheza vema na kutumia nafasi watakazozitengeneza.

"Tumefika salama, inawezekana kupata ushindi," alisema Kagere ambaye alitua Simba akitokea kwa mabingwa wa Ligi Kuu Kenya, Gor Mahia. Katika mechi ya kwanza iliyochezwa Aprili 6 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini, timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >